



KIJITABU CHA JINSI YA KUNAWA MIKONO

Mwongozo wa kuandaa
programu ya kuhamasisha hali ya usafi ili
kuongeza mwamko wa watu katika
kunawa mikono kwa sabuni



THE WORLD BANK



© The International Bank for Reconstruction and Development/The World Bank
1818 H Street, NW
Washington DC, 20433, USA
www.worldbank.org
All rights reserved



The findings, interpretations, and conclusions in this paper are entirely those of the author(s) and should not be attributed in any manner to the World Bank, to its affiliated organizations, or to members of its Board of Executive Directors or the countries they represent. The World Bank does not guarantee the accuracy of the data included in this document and accepts no responsibility for any consequences of their use.

Kijitabu cha Jinsi ya Kunawa Mikono

Mwongozo wa kuandaa programu ya
kuhamasisha usafi ili kuongeza mwamko wa watu
kuhusu unawaji mikono kwa sabuni

YALIYOMO

DIBAJI 5

MUHTASARI MAALUMU KWA AJILI YA WAANDAMIZI 7

UTANGULIZI 8

Madhumuni ya Kijitabu Hiki

Muktadha

Sababu Kuu za Vifo vya Watoto

Kunawa Mikono kwa Sabuni:

Kinga Madhubuti Zaidi Dhidi ya Maambukizi kwa Watoto?

Changamoto ya Kuhamasisha Unawaji Mikono

Kuna Upya Gani katika Mtazamo Huu?

SEHEMU YA I 13

Kuweka Msingi wa Programu ya Taifa ya

Kunawa Mikono kwa Sabuni

Mwanzo: Je, Hapa ni Mahali na Muda Mwafaka?

Kufanya Uchambuzi wa Haraka wa Hali Halisi

Ushirika Baina ya Sekta ya Umma na ya Binafsi

Kujenga Hoja ya Kunawa Mikono

Kujenga Hoja kwa Serikali

Kujenga Hoja Viwandani

Kujenga Hoja kwa Wagharamiaji

Masuala ya Ugharamiaji Kifedha

Muundo na Uratibu

SEHEMU YA 2 21

Kumwelewa Mlengwa

Mkabala wa Kimasoko

Kuelewa Tabia

Kubuni na Kutekeleza Utafiti wa Mlengwa

Uongozaji na Usimamiaji wa Utafiti wa Mlengwa

Uchambuzi na Kuripoti Matokeo

SEHEMU YA 3 33

Utekelezaji wa Programu

Kuandaa Kampeni

Kutumia Masoko Mseto

Kutayarisha Uhamasishaji

Walengwa na Ugawaji katika Vikundi

Mashirika, Dhana, na Majaribio

Mikakati Anuwai ya Kubadili Tabia

Uhusiano wa Umma na Ushawishi

Mpango wa Uhusiano wa Umma

Vyombo Mseto vya Habari

Ufuatiliaji na Tathmini

SEHEMU YA 4 43

Muundo wa Programu

Ushirika Mseto

Mfano wa Ushirika wa Jumla

Colgate-Palmolive: Mikono Safi, Afya Njema

Mpango wa Kazi

HITIMISHO 49

MAREJEO NA VYANZO 51

ZANA NA HADIDU ZA REJEA 53

ABBREVIATIONS 76

ORODHA YA MAJEDWALI NA VIELELEZO

- Kielelezo na. 1: Mtawanyo wa Vifo Vitokanavyo na Magonjwa Duniani
- Kielelezo na. 2: Mchoro wa V: Njia Kuu za Magonjwa Yaeneayo kwa Kinyesi-Kinywa
- Jedwali na. 1: Viwango vya Unawaji Mikono kwa Sabuni Vilivyoshuhudiwa katika Nchi Mbalimbali Ulimwenguni
- Jedwali na. 2: Mambo ya Kuzingatia katika Uchambuzi wa Uwezo, Udhaifu, Fursa, na Matatizo
- Jedwali na. 3: Mambo ya Nje ya Uchambuzi wa Uwezo, Udhaifu, Fursa, na Matatizo
- Kisanduku na. 1: Unafuu Kigharama wa Programu za Unawaji Mikono
- Kisanduku na. 2: Juhudi za Amerika ya Kati
- Kielelezo na. 3: Mchakato wa Utafiti wa Mlengwa
- Kielelezo na. 4: Mazingira, Tabia, na Vichochezi
- Kisanduku na. 3: Imani za Kiutamaduni Zinazokwamisha Tabia ya Unawaji Mikono kwa Sabuni Nchini Senegali
- Jedwali na. 4: Vichocheo, Tabia, na Mazingira ya Unawaji Mikono kwa Sabuni (Maeneo Manne)
- Jedwali na. 5: Kubainisha Vikwazo na Vichocheo vya Unawaji Mikono kwa Sabuni katika Matukio Muhimu
- Kisanduku na. 4: Walengwa wa Ghana Wanapendelea Sabuni zenye Matumizi Mengi, Zinazodumu na za Bei Nafuu
- Kisanduku na. 5: Dokezo Kuhusu Shule
- Kielelezo na. 5: Jinsi Kinamama wa Kerala, India Wanavyowasiliana: Taarifa za Mawasiliano kwa Mwezi
- Kisanduku na. 6: Mwongozo wa Njia za Utafiti
- Jedwali na. 6: Mpango Muhtasari wa Utafiti wa Mlengwa
- Kisanduku na. 7: Vidokezo Muhimu katika Kuingia Mkataba wa Utafiti wa Mlengwa
- Kisanduku na. 8: Utafiti wa Mlengwa: Upendeleo wa Kimantiki
- Kisanduku na. 9: Taarifa Kamilifu
- Jedwali na. 7: Faida na Hasara za Mikabala Tofauti ya Mawasiliano
- Kisanduku na. 10: Somo la Uhusiano wa Umma: Unawaji mikono huko Kerala, India
- Jedwali na. 8: Harakati za Kitaifa za Unawaji Mikono Ghana: Matokeo ya Tathmini ya Awamu ya I (Katika asilimia)
- Kielelezo na. 6: Ufuatiliaji na Tathmini: Kazi na Matokeo ya Programu
- Kisanduku na. 11: Utekelezaji wa Unawaji Mikono: Ushirika wa Unawaji Mikono Huko Peru
- Kisanduku na. 12: Shughuli za Sekta Binafsi za Unawaji Mikono
- Kisanduku na. 13: Vipengele vya Mpango wa Kazi

DIBAJI

Usafi ni jambo muhimu sana katika dira ya afya ya jamii ya kupunguza maambukizi na athari za maradhi. Kupungua kwa haraka kwa vifo vinavyotokana na magonjwa ya kuambukiza kulikoonekana katika nchi tajiri mnamo karne iliyopita kusingeweza kufikiwa bila uboreshaji wa hali ya juu wa afya ya jamii. Kupanda kwa viwango vya maisha kuliwawezesha watu kujali zaidi usafi pale ambapo maji safi yaliwafikia majumbani mwao, na bei ya sabuni ilipokuwa nafuu kiasi kwamba ilikuwa rahisi kuweka sabuni katika kila sinki. Hatimaye juhudi za pamoja baina ya harakati za afya ya jamii na sekta binafsi zimewezesha mambo kama vile usafi wa mikono, makazi, na katika maisha kuwa ni sehemu ya maisha ya jamii.

Kwa bahati mbaya, katika nchi maskini hadithi hizi hazijaleta tofauti ya maisha. Hadi kufikia mwishoni mwa karne ya 20, watu bilioni mbili bado hawakuwa na uwezo wa kupata maji safi kadiri inavyotakiwa, na watu bilioni moja hawakuwa na maji safi ya kunywa yanayotosheleza mahitaji yao. Jitihada za kuhamasisha kwa ufanisi hali ya usafi zimekuwa za polepole sana na mara nyingi bila mafanikio. Ingawa maendeleo ya viwanda yamerahisisha upatikanaji wa sabuni majumbani, bado hayajafanikiwa kuhamasisha hali ya usafi au mwamko wa watu kuhusu unawaji mikono kwa sabuni kwa kiwango cha juu ili kwenda sambamba na matokeo ya maendeleo hayo.

Hii ni fursa adimu kwa afya ya jamii. Vyanzo vikuu viwili vya vifo vya watoto katika nchi zinazoendelea kwa sasa ni magonjwa ya kuhara na maambukizi ya mfumo wa upumuaji. Kitendo kidogo cha kunawa mikono kwa sabuni kinaweza kuondoa takribani nusu ya hatari ya kuambukizwa magonjwa ya kuhara na takribani theluthi ya maambukizi ya mfumo wa upumuaji. Hali hii inakifanya kitendo cha kunawa mikono kuwa chaguo bora zaidi la kuzuia maambukizi ya magonjwa kuliko chanjo au kinga nyingine yoyote.

Ikiwa nchi zinazoendelea zinataka kufikia malengo yao ya maendeleo ya milenia ifikapo mwaka 2015 ya kupunguza vifo vya watoto, ajenda hii iliyosahaulika katika karne ya 20 haina budi kutiliwa maanani. Haitoshi tu maji safi na salama kupatikana kote, bali pia tabia ya kunawa mikono kwa sabuni lazima iwe kwa watu wote. Jambo hili linahitaji Wizara za Afya, Elimu, na Maji, pamoja na asasi zisizo za serikali na jumuiya za kijamii, kutumia kila fursa iliyopo kuinua mwamko wa watu kuhusu unawaji mikono kwa sabuni.

Aidha, sekta binafsi, ambayo ilichangia kwa kisasi kikubwa kupandisha viwango vya hali ya usafi katika nchi tajiri, inaweza kufanya vivyo hivyo pale inapopanua shughuli zake katika nchi zinazoendelea.


Kunawa mikono kwa sabuni lazima liwe jambo la kawaida katika nchi zinazoendelea. Ili jambo hili liweze kufanyika ni lazima:

- Kuhakikisha kila mmoja anafahamu umuhimu wa kunawa mikono kwa sabuni;
- Kuanzisha ushirikiano baina ya sekta ya umma na ya binafsi;
- Kuandaa wataalam na raslimali zinazotakiwa;
- Kutumia mawasiliano ya hali ya juu yatakayowezesha watu wengi kadiri iwezekanavyo kupata taarifa ili kuhamasisha unawaji mikono kwa sabuni;
- Kuonesha kwamba mabadiliko ya tabia yanayopimika yanaweza kufikiwa kwa gharama nafuu.

Katika ulimwengu wenye kelele nyingi zinazotokana na ushindani wa kutuma ujumbe kuelekea kwa watu kutoka pande zote za dunia, kampeni madhubuti tu na zilizobuniwa vizuri ndizo zinaweza kuleta mabadiliko ya tabia. Kijitabu hiki kimekusudiwa kuikabili changamoto hii.

Kijitabu hiki kinaelezea mkabala mpya wa kuhamasisha watu kuhusu unawaji mikono kwa sabuni, msingi wake ukiwa ni kazi ya mwanzo ya Ushirika baina ya Serikali na Sekta Binafsi kuhusu Unawaji wa Mikono kwa Sabuni. Kinaelezea jinsi fikra mpya kuhusiana na utafutaji wa masoko zinavyoweza kuunganishwa na utafiti wa sasa katika sekta ya afya ya jamii ili kutoa mwanga mpya kuhusu uendeshaji wa kampeni zenye ufanisi za kunawa mikono kwa sabuni. Kijitabu kina mambo mengi ya kujifunza kutoka nchi za Ghana, Peru, Senegali, na kwingineko. Viashiria vya awali vinaonesha kuwa huu unaweza kuwa mwanzo wa fani ya kusisimua ya sanaa katika uga wa afya ya jamii katika karne ya 21.

Wanachama wengi wa Harakati za Ushirika baina ya Sekta ya Umma na ya Binafsi Duniani katika Unawaji wa Mikono kwa Sabuni hawana budi kupewa shukrani kwa kuwezesha kijitabu hiki kupatikana kama hivi kilivyo. Kwanza kabisa, tungependa kuwashukuru Beth Scott, Valerie Curtis na Jarson Cardos kwa kutunga kijitabu hiki. Shukurani zetu za dhati pia ziwaendee Ali Diof, Rocio Florez, na Nana Garbrah-Aidoo kwa kutoa mifano ya nchi mahususi. Shukurani za pekee ziwaendee Peter Kolsky, Mariam Claeson, Stéphane Legros, na Nancy Lee kwa mapitio yao ya pamoja ya kijitabu hiki. Michango mingine isiyosahaulika ilitoka kwa Steve Luby, Eckhard Kleinau, Suzanne Reiff, Camille Saade, Myriam Sidibe, Barbara Evans, Sandy Callier, Joana Godinho, Wendy Wakeman, Merri Weigner, na Henk Van Norden. Washirika wa sekta binafsi, Yuri Jain kutoka Hindustan Lever, Diana Grina kutoka Colgate-Palmolive, na Tim Long kutoka Procter and Gamble, walitoa msaada wa kitaalamu na kiufundi. Mwisho, tungependa kutoa shukrani zetu kwa viongozi wa Timu ya Kazi hii, Jennifer Sara na Param Iyer.



Jamal Saghir

Mkurugenzi, Nishati na Maji



Jacques Baudouy

Mkurugenzi, Afya, Lishe na Idadi ya Watu

DIBAJI YA TOLEO LA KISWAHILI

Kazi ya kutafsiri kijitabu hiki imefanyika kwa ushirikiano mkubwa kutoka kwa Wadau wa Mpango wa Unawaji Mikono kwa kutumia Sabuni waliopo katika Sekta ya Umma na Binafsi (PPPHW-Tanzania). Tunatoa shukurani za dhati kwa wale wote waliotumia muda wao kuhakikisha kwamba shughuli hii inafanikiwa ya kutafsiri kijitabu hiki cha kuhimiza umawaji wa mikono kwa kutumia sabuni. Hawa ni Ndugu Anyitike Mwakitalima, Yasinta Kisisiwe (wote kutoka Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii), Dorisia Mrashani (Wizara ya Maji) na Dkt Edith Ngirwamungu (ITI-Tanzania).

Aidha tunapenda kuchukua fursa fursa hii kuwashukuru wale wote walitoa mchango na mawazo wakati wa hatua za uhariri wa kijitabu hiki. Miongoni mwa wale walioshiriki katika kuhariri kijitabu hiki ni pamoja na BI Rebeca Budimu (UNICEF-Tanzania) na Wilhemina Malima (Water Aid-Tanzania). Tunachukua fursa hii kutambua mchango iliyofanywa na ndugu Kaposo Mwambuli (WSP-Tanzania) na Bi Rosalie Ferrao (Benki ya Dunia-Tanzania) katika kuratibu na kusimamia zoezi zima la kutafsiri kijitabu hiki.

Mwisho tunapenda kutambua mchango ya mawazo toka kwa wadau mbalimbali nchini wa kutoka sekta za maji, afya na Usafi wa Mazingira kwa mapendekezo ya kuboresha na kufanikisha kazi hii.

MUHTASARI MAALUMU KWA AJILI YA WAANDAMIZI

Kunawa mikono ni njia madhubuti zaidi ya kuzuia au kujikinga dhidi ya magonjwa ya kuhara. Aidha, njia hii huwezesha kuwepo kwa utupaji salama wa takamwili na usambazaji wa maji safi, salama, na ya kutosha majumbani. Ushahidi unaonesha kwamba unawaji mikono ulioboreshwa unaweza kuwa na matokeo au athari kubwa kwa afya ya jamii katika nchi yoyote, na unaweza kwa kiasi kikubwa, kupunguza vyanzo vikuu viwili vya vifo vya watoto—magonjwa ya kuhara na maambukizi ya mfumo wa upumuaji. Kwa sababu kitendo cha kunawa mikono kwa sabuni kinaweza kuzuia ueneaji wa vijidudu visababishavyo magonjwa, kinaweza kuwa kinga madhubuti zaidi kuliko kinga nyingine yoyote au tabia nyingine yoyote ya usafi. Iwapo kutakuwa na uhamasishaji mkubwa, tabia ya kunawa mikono kwa sabuni inaweza kuchukuliwa kuwa ni kinga ya kujipatia mwenyewe. Takribani kila kaya duniani, bila kujali hadhi yake kiuchumi, huwa na sabuni. Hata hivyo, unawaji mikono kwa sabuni katika nyakati muhimu, kwa kiasi kikubwa, haufanyiki kabisa au haufanyiki ipasavyo. Ili malengo ya maendeleo ya milenia ya kupunguza vifo vya watoto yafikiwe, mienendo ya kunawa mikono haina budi kuboreshwa sanjari na upatikanaji wa maji safi na salama.

Harakati za Ushirika baina ya sekta ya umma na ya binafsi Duniani katika Unawaji wa Mikono zimeyakutanisha mashirika na sekta mbalimbali ili kuhamasisha kwa kiwango kikubwa zaidi mwamko wa watu kuhusu unawaji mikono kwa sabuni. Ushirika huu unajumuisha:

- Mashirika ya ufadhili ambayo huhusisha suala la kunawa mikono katika programu zao za maji salama, afya, na elimu;
- Sekta binafsi ambayo imefungua njia ya sanaa ya maarifa na mbinu za masoko;
- Mashirika ya kitaaluma na kisayansi ambayo yanachangia kubuni nadharia zinazotamba za mabadiliko ya tabia, na ushahidi wa kisayansi kuhusu umadhubuti wa unawaji mikono; na
- Mashirika yasiyo ya serikali na jumuiya za kiraia ambayo yana lengo la kuingiza ujumbe wa kunawa mikono katika mipango yao ya kazi.
- Kwa kuwa serikali inaweza kiapa umbele katika kuhimiza usafi, itakuwa rahisi kuenea kwa shughuli za kuhimiza usafi na unawaji wa mikono kwa sabuni kutoka ngazi ya kijiji kufikia ngazi ya kitaifa.

Kijitabu cha Taratibu za Kunawa Mikono kinadokeza uzoefu wa Ushirika huu katika mwongozo wa kiutendaji. Wakati ambapo nchi nyingi zingali zikifanyia majaribio mikabala mbalimbali na kuifanya iwe bora kabisa, ni muhimu kutoa na kusambaza kile kinachofahamika kwa sasa. Kwa njia hii watu wengine wanaweza kuanza kubuni programu mbalimbali na hivyo kuchangia uzoefu na maarifa yao duniani katika mapambano dhidi ya vifo vya watoto. Mwongozo huu ni maalum kwa wafanyakazi wa serikali na mashirika ya maendeleo yaliyo na jukumu la kuendesha programu za unawaji mikono. Kijitabu hiki pia kitakuwa cha msaada kwa watoa maamuzi katika wizara za serikali na mashirika ya ufadhili. Kitawasaidia kuandaa sera na programu zitakazoboresha afya ya jamii.

Mkabala wa kuinua mwamko wa watu kuhusu unawaji mikono unashughulikia vipengele vifuatavyo:

Kuweka Msingi wa Programu ya Taifa ya Kunawa Mikono kwa Sabuni

Ili zifanikiwe, programu za unawaji mikono lazima zishughulikie mahitaji ya kiafya yanayotambulika na ziungwe mkono na wadau wakuu. Serikali, viwanda, na wafadhili wanaweza kutoa raslimali za kipekee ambazo ni muhimu katika kuhakikisha mafanikio ya programu kubwa. Ufanyaji wa uchambuzi wa hali halisi na, pale inapohitajika, kujenga hoja ya kunawa mikono kwa njia ya mada mbalimbali kuanzia zile zinazohusu nafuu wa gharama hadi zile za matokeo ya afya, unaweza kuiwekea programu ya unawaji mikono msingi imara.

Kumwelewa Mlengwa

Ili kuzibadili zile desturi zilizoote mizizi zinazohusiana na tabia kama vile kunawa mikono, ni lazima kuzielewa kwa uthabiti sababu, vichocheo na tabia zinazowahamasisha walengwa. Hii ina maana kwamba, ni muhimu kuzingatia kwa makini mahitaji ya walengwa—hususan kinamama na watunzaji wa watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano pamoja na wale wenye umri wa kwenda shule—na kuacha mtazamo wao uamue namna na mawanda ya shughuli za kuchochea mwamko wa watu kuhusu unawaji kwa sabuni. Kuendesha utafiti wa walengwa kutaweka msingi wa kutathmini na kuwaelewa walengwa kwa kujibu maswali makuu manne: Desturi zipi ni hatarishi? Ni nani huendeleza desturi hatarishi? Ni vichocheo vipi, desturi zipi na sababu zipi za kimazingira huweza kubadili tabia? Watu wanawasilianaje?

Utekelezaji wa Programu

Matokeo ya utafiti wa mlengwa yataongoza utekelezaji wa programu ikiwa ni pamoja na masuala ya kimazingira yanayohusiana na unawaji mikono yanayostahili kushughulikiwa, ni njia ipi inayofaa zaidi na inayovutia katika kuinua mwamko wa kunawa mikono miongoni mwa watu, na mchanganyiko gani wa njia za mawasiliano unaofaa zaidi ili kuweza kuwafikia walengwa. Utekelezaji pia hujumuisha ufuatiliaji makini wa programu na tathmini ya mara kwa mara pamoja na marekebisho.

Muundo wa Programu

Pale ambapo washirika kutoka katika mazingira na sekta tofauti tofauti hawakuzoea kufanya kazi pamoja uwekaji wa malengo ya pamoja na ujenzi wa uaminifu huchukua muda mrefu na jitihada kubwa. Kuwa na mratibu wa programu katika umoja unaoaminika ni mkabala madhubuti wa kuwaongoza washirika wenye tajriba tofauti kuelekea katika lengo la pamoja.

Katika kijitabu chote hiki, marejeo, taarifa za tafiti mahususi, na zana za utafiti vimebainishwa ili kuzisaidia programu za unawaji mikono. Watumiaji wanahamasishwa waunganishe ubunifu wao na maarifa yaliyopo ili kuweza kuvumbua na kuboresha zaidi mikabala ya uhamasishaji mkubwa wa unawaji mikono.

UTANGULIZI

Madhumuni ya Kijitabu Hiki

Kijitabu hiki ni matokeo ya Ushirika baina ya Sekta ya Umma na ya Binafsi Duniani kuhusu Unawaji wa Mikono kwa Sabuni pamoja na Programu tangulizi ya Amerika ya Kati ya Kuzuia Magonjwa ya Kuhara kwa Kunawa Mikono. Jitihada hizi zinaonesha kwamba programu za umma zinazohusisha sekta ya umma na ya binafsi zinaweza kuwa na manufaa katika uhamasishaji wa unawaji mikono na kupunguza magonjwa. Kwa msaada mkubwa kutoka Benki na Ushirika wa Maji wa Uholanzi, Ushirika wa Sekta ya Umma na ya Binafsi katika Unawaji Mikono umeyaleta pamoja mashirika ya umma na ya binafsi duniani ili kuweka mikabala pamoja wakati wa kuanzisha uhamasishaji mkubwa wa unawaji mikono nchini Ghana, Peru, Senegali, na Nepali.

Wakati ambapo mengi yameshajifunzwa kuhusu uhamasishaji wa unawaji mikono katika miaka ya hivi karibuni, hasa katika nyanja za utafiti na kubuni programu, nchi nyingi zingali zikifanyia majaribio mikabala mbalimbali na kuifanya iwe bora kabisa, ni muhimu kutoa na kusambaza kile kinachofahamika kwa sasa ili watu wengine nao waweze kuanza kubuni programu mbalimbali na hivyo kuchangia uzoefu na maarifa yao duniani katika mapambano dhidi ya vifo vya watoto.

Kijitabu hiki kimeandaliwa maalum kwa wafanyakazi wa serikali na mashirika ya maendeleo yaliyo na jukumu la kuendesha programu za unawaji mikono. Kijitabu pia kitakuwa na msaada kwa watoa maamuzi katika Wizara za serikali na mashirika ya ufadhili. Kitawasaidia kuandaa sera na programu zitakazoboresha afya ya jamii.

Muktadha

Kunawa mikono ni njia madhubuti zaidi ya kuzuia au kujikinga dhidi ya magonjwa ya kuhara, pamoja na kuwezesha utupaji salama wa takamwili na usambazaji wa maji safi, salama, na ya kutosha majumbani. Kijitabu hiki kinatilia mkazo katika suala zima la unawaji mikono na kupigania programu za unawaji mikono kwa sabuni ambazo zinajitegemea.

Mwongozo huu haukusudii kudunisha au kukashifu mienendo ya usafi iliyo tofauti na unawaji mikono. Kinyume chake, kila kimoja kina nafasi yake na ni muhimu kishughulikiwe tofauti, kwa uangalifu, na katika muktadha sahihi. Hata hivyo, ni dhahiri katika programu za mawasiliano kwamba ujumbe hauna budi kuwa mfupi na rahisi: utoaji wa ujumbe hauwezi kubanwa kwa kutumia kizio mahususi cha kipimo. Kwa mfano, kutuma ujumbe zaidi ya mmoja katika tukio moja la mawasiliano hupunguza umadhubuti wa kila kimoja kwa nusu. Hivyo basi, haishauriwi kuirundika pamoja mienendo mikuu mitatu ya usafi.

Mkabala wa uhamasishaji wa unawaji mikono unaoelezwa katika kijitabu hiki unahusisha utafiti makini wa mlengwa unaofuatiwa na jitihada za kisasa za utafutaji wa masoko. Mkabala huu unaoana vyema na masuala mengine ya kiafya. Mambo ya kujifunza yaliyotokana na kuendesha programu za unawaji mikono yanaweza kutumiwa katika programu nyingine kwa mikabala ileile ya kiufundi na kiasasi.

Jitihada za sasa za kuhamasisha hali nzuri ya usafi, ikiwa ni pamoja na unawaji mikono, hazijawa na nguvu za kutosha kuleta mabadiliko ya tabia kwa watu wengi. Programu nyingi za afya ya jamii hujumuisha usafi miongoni mwa madhumuni au malengo yao: katika nchi yoyote wakati wowote, mtu anaweza kukuta programu ya kudhibiti ugonjwa wa kuhara, programu ya afya shuleni inayojumuisha usafi, programu ya usambazaji wa maji safi na salama iliyoelekezwa katika kuinua uelewa wa watu kuhusu usafi, pamoja na programu za hapa na pale za elimu ya usafi. Programu zote hizi zinakabiliwa na udhaifu wa kuchukulia usafi kama suala la pembezoni badala ya kuliona kama la msingi. Hakuna raslimali za kutosha; ubunifu, stadi za watu, na shauku zao hazihusishwi kikamilifu; na pengine mikabala inaweza kuwa imepitwa na wakati. Hakuna shirika hata moja linalopigania suala la usafi, na vyombo vya ufadhili havioni umuhimu wake. Malengo yaliyo kwenye maandiko hayatekelezwi ipasavyo, hayapatiwi raslimali za kutosha, hayafanyiwi tathmini na ufuatiliaji. Mafanikio kwa kiasi kikubwa yamekuwa ni ya ngazi ya eneo mojamoya tu, yakiwa yamepatikana kwa kutumia mikabala ambayo haiwezi kupanuliwa nchi nzima. Mbaya zaidi, mkanganyiko hutawala pale linapokuja suala la msingi la usafi-usafi ni nini hasa: watu mbalimbali wanafasili dhana hii kwa namna tofauti, kwa hisia binafsi na kwa upendeleo wa mazingira ya nyumbani ambayo hutawala na kufunika ushahidi.

Mkabala unaofanuliwa katika kijitabu hiki unalenga katika kutatua matatizo yote haya: unaongeza utambuzi, dhamiri ya kisiasa na utengaji wa raslimali kwa ajili ya usafi; unaonesha njia ya kuelekea katika programu ya taifa inayoratibiwa, vyote


hivi vikiwa chini ya mwavuli mmoja. Aidha, mkabala unatumia njia za hali ya juu na za kisasa zaidi kuhusu mabadiliko ya tabia ya usafi ambazo zinaonesha uwezekano mkubwa wa kusisimua uwanja wa afya ya jamii kwa ujumla; unawaji mikono kwa sabuni.

Kama ilivyo kwamba kila mtoto ana haki ya kupata chanjo, vivyo hivyo kila mtoto awe na haki ya kukingwa dhidi ya maambukizi yaenezwayo kwa mikono. Hii ina maana tu ya kunawa mikono kwa sabuni baada ya kutoka chooni au baada ya kumtawadha mtoto na kabla ya kushika chakula.

Sababu Kuu za Vifo vya Watoto

Shirika la Afya Duniani (WHO) linakadiria kwamba magonjwa ya kuhara na maambukizi ya mfumo wa upumuaji yanahusika kwa theluthi mbili ya vifo vya watoto (tazama kielelezo na 1). Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) linakadiria kwamba ugonjwa wa kuhara peke yake hua mtoto mmoja kila baada ya sekunde 30. Vifo vingi vya watoto hutokea kwa watu maskini zaidi katika nchi zenye kipato cha kati au cha chini.

Kielelezo na. 1: Mtawanyo wa Vifo Vitokanavyo na Magonjwa Duniani




Chanzo: Shirika la Afya Duniani 2001

Kunawa Mikono kwa Sabuni: Kinga Madhubuti Zaidi Dhidi ya Maambukizi kwa Watoto?

Vinyesi vya binadamu ni chanzo kikuu cha vijidudu visababishavyo magonjwa ya kuhara. Vilevile ni vyanzo vya maambukizi ya shigela, homa ya matumbo, kipindupindu, pamoja na maambukizi mengine yote ya magonjwa ya tumbo, na baadhi ya maambukizi ya mfumo wa upumiaji: gramu moja tu ya kinyesi cha binadamu inaweza kuwa na virusi milioni 10 na bakteria milioni moja. Vijidudu hivi husafirishwa kutoka kwa mtu aliyeambrukizwa kwenda kwa mwingine kupitia njia mbalimbali kama inavyooneshwa katika kielelezo na. 2. Wakati ambapo njia ni nyingi, zote zinatokana na chanzo kimoja: kinyesi. Wakati ambapo hatua za mwanzo (utunzaji wa chakula, uchujaji wa maji, na udhibiti wa nzi) zinaweza kusaidia, hatua muhimu zaidi ni vizuizi vya msingi—usafi na kunawa mikono—baada ya kushika au kugusa kinyesi. Kwanza kabisa, vizuizi hivi huzuia vijidudu vya magonjwa vitokavyo kwenye kinyesi kufika mazingira ya majumbani.

Unawaji mikono huzuia ueneaji wa vijidudu vya magonjwa na hivyo unaweza kupunguza kwa kiasi kikubwa maambukizi ya mfumo wa upumuaji, magonjwa ya kuhara, pamoja na magonjwa ya ngozi na vikope. Utafiti wa hivi karibuni (Curtis na Cairncross, 2003) unaonesha kuwa kunawa mikono kwa sabuni, hususan baada ya kugusa kinyesi (baada ya haja kubwa na baada ya kuzoa kinyesi cha mtoto), kunaweza kupunguza maambukizo wa magonjwa ya kuhara kwa asilimia 42-47, wakati ambapo, kwa mujibu wa kazi inayoendelea ya Rabie na wenzake kuna uwezekano wa kupunguza maambukizi ya mfumo wa upumuaji kwa asilimia 30. Ukweli huu unabaki pale pale hata katika maeneo yaliyo machafu sana kwa vinyesi. Utafiti mwingine wa hivi karibuni umegundua kuwa watoto wenye umri wa chini ya miaka 15 wanaoishi maeneo yaliyopata uhamasishaji wa unawaji mikono kwa sabuni walipunguza kiwango chao cha kuhara ikilinganishwa na cha watoto wanaokaa mazingira ya jirani (Luby na wenzake, 2004). Kwa sababu kitendo cha kunawa mikono kwa sabuni kinaweza kuzuia ueneaji wa vijidudu mbalimbali visababishavyo magonjwa, kitendo hicho kinaweza kuwa kinga madhubuti zaidi kuliko kinga nyingine yoyote. Iwapo kutakuwa na uhamasishaji mkubwa, tabia ya kunawa mikono kwa sabuni inaweza kuchukuliwa kuwa ni kinga ya kujipatia mwenyewe.

Kielelezo na. 2: Mchoro wa V: Njia Kuu za Magonjwa Yaeneayo kwa Kinyesi-Kinywa



Chanzo: Wagner na Lanois, 1958

Kinyesi ni chanzo cha vijidudu vienezavyo magonjwa ya kuhara, vijidudu vidogovidogo visivyoonekana kwa macho, ila kwa hadubini. Kama kielelezo hicho hapo juu kinavyoonesha, vijidudu hivi huingia katika mazingira tunamoishi iwapo vinyesi havikutupwa kwa namna ya usalama, kisha huenea kwa V nne: Vinyesi, vijidudu (nzi), vidoleni, katika vimiminika (majimaji), na maeneo ya nchi kavu kama vile viwanjani. Kuziba njia hizi za uenezaji wa vijidudu ni jambo la msingi sana katika suala zima la kuzuia magonjwa ya kuhara, lakini je, ni mwenendo upi wa kiusafi, miongoni mwa mingi iliyopo, utaweza kutokomeza magonjwa hayo? Kuchemsha maji au kutia dawa kunaweza kupunguza ugonjwa wa kuhara, lakini kuvizua vijidudu vienezavyo ugonjwa kutoka kwenye vinyesi ili visifike kabisa katika maji ya majumbani mwetu ni vizuri zaidi na gharama yake ni nafuu zaidi. Vivyo hivyo, vyakula vinapaswa vipashwe moto kwa uangalifu ili kuuha vijidudu vyovyote vinavyozaliana wakati wa kuhifadhi, lakini kuvizua vijidudu vienezavyo ugonjwa kutoka kwenye vinyesi ili visifike kabisa katika vyakula vyetu ni njia yenye ufanisi zaidi.

Vitendo vikuu viwili huvitenga na kuvizua vijidudu vitokavyo kwenye kinyesi visifike katika mazingira tuishiyo na katika V nne. Vitendo hivi ni kutupa vizuri vinyesi vya watu wazima na vya watoto pamoja na kunawa mikono kwa sabuni baada ya kugusa vinyesi. Kugusa huko hutokea baada ya kutumia choo au pale tunapowatawadha watoto baada ya kwenda haja kubwa.

Baadhi ya maambukizi ya mfumo wa upumuaji, ikiwa ni pamoja na virusikorona visababishavyo Mafua ya ndege (SARS), huenezwa pia kwa njia ya kinyesi-kinywa au hata mikono tu. Kwa hiyo, kunawa mikono husaidia kuzuia maambukizi haya vilevile.

Je, unawaji mikono ufanyweje? Ushahidi unaonesha kwamba sabuni—sabuni yoyote—na maji huondoa vizuri uchafu wa mikononi unaobeba vijidudu. Sabuni za kujikinga dhidi ya bakteria na teknolojia nyinginezo za kusafisha mikono hazina manufaa ya ziada. Wakati wa kunawa mikono, ni vyema mikono ifunikwe na sabuni kikamilifu, kisha isuuzwe na ikaushwe vizuri baada ya kunawa.

Changamoto ya Kuhamasisha Unawaji Mikono

Kama unawaji mikono kwa sabuni ni muhimu kiasi hiki, kwa nini haufanywi na kila mtu?

Jedwali na. 1 linaonesha kwamba viwango vya unawaji mikono kwa sabuni ulimwenguni kote viko chini sana. Wakati ambapo watu wengi hunawa mikono yao kwa maji, ni asilimia ndogo tu ya watu hawa hutumia sabuni katika nyakati muhimu.

Jedwali na. 1: Viwango vya Unawaji Mikono kwa Sabuni Vilivyoshuhudiwa katika Nchi Mbalimbali Ulimwenguni

Eneo	Kunawa Mikono kwa Sabuni	Utokeaji	Marejeo
Jimbo la Kerala, India	Baada ya haja kubwa	Asilimia 34	USSBUM
	Baada ya kutawadha mtoto	Asilimia 35	
Ghana	Baada ya haja kubwa	Asilimia 3	USSBUM
	Baada ya kutawadha mtoto	Asilimia 3	
Peru	Baada ya haja kubwa	Asilimia 6	USSBUM
	Baada ya kutawadha mtoto	Asilimia 30	
Senegali	Baada ya haja kubwa	Asilimia 31	USSBUM
	Baada ya kutawadha mtoto	Asilimia 26	
Kolkata, India (maeneo ya maskini wa kutupwa)	Baada ya haja kubwa	Asilimia 16	Sircar <i>na wenzake</i> , 1996
Kirigistani (vijijini)	Baada ya kutawadha mtoto	Asilimia 0	Biran, 1999
	Baada ya haja kubwa	Asilimia 18	
Nijeria (vijijini)	Baada ya kutawadha mtoto	Asilimia 10	Omotade <i>na wenzake</i> , 1995
Burkina Faso (mjini)	Baada ya kutawadha mtoto	Asilimia 13	Curtis <i>na wenzake</i> , 2001
	Baada ya haja kubwa	Asilimia 1	
Brazili (vituo vya kulelea watoto)	Baada ya kutawadha mtoto	Asilimia 16	Barros <i>na wenzake</i> , 1999
Lima, Peru (mji usiopimwa)	Baada ya haja kubwa (matumizi ya sabuni kwa “nadra”)	Asilimia 12	Gilman <i>na wenzake</i> , 1993
Uingereza Kaskazini (mji mdogo)	Baada ya kutawadha mtoto	Asilimia 47	Curtis <i>na wenzake</i> , 2003

Zingatia: Utokeaji wote unaoonekana hapa, isipokuwa ule wa Sircar na wenzake, ambao ulitumia vipimo vya sabuni, umeshuhudiwa.

Ni kwa nadra sana ukosefu wa sabuni kuwa sababu ya viwango vya unawaji mikono kuwa vya chini. Kaya nyingi duniani kote huwa na sabuni, lakini kwa kawaida sabuni hizo hutumiwa kwa kuogea na kufulia, si kunawia mikono. Aidha, ukosefu wa maji si tatizo vilevile kwa kuwa unawaji mikono unaweza kufanyika vizuri kwa kutumia kiasi kidogo tu cha maji au hata maji yaliyokwishatumika sehemu nyingine. Katika tafiti mbalimbali duniani, sababu kubwa inayoeleza ni kwa nini viwango vya unawaji mikono kwa sabuni ni vya chini kiasi hicho ni kukosekana tu kwa tabia ya kunawa mikono kwa sabuni.


Kuna Upya Gani katika Mtazamo Huu?

Kijitabu hiki kinaeleza jinsi tabia ya unawaji mikono inavyoweza kubadilishwa kwa kiwango kikubwa au cha kitaifa kwa kutoa masomo kutoka mikabala ya utafutaji masoko viwandani pamoja na mikondo ya sasa ya afya ya jamii. Sifa yake kuu ni uwekaji mkazo kwa mnawaji mikono kama mlengwa, mwenye chaguzi mbalimbali. Kwa kuweka mkazo kwa mnawaji mikono, kijitabu hiki kinaeleza jinsi ya:

- *Kutafiti* mahitaji ya mlengwa katika tabia za unawaji mikono, vikwazo na vichocheo vya mabadiliko ya tabia na njia bora za kuwasiliana na walengwa;
- *Kubuni* ujumbe mzuri na unaofaa;
- *Kutekeleza* uhamasishaji wa programu unaotumia njia nzuri za mawasiliano, ikiwa ni pamoja na watumishi wa nyanjani, mitandao ya wananchi, matukio maalum, wasambazaji wa sabuni, mashule, na vyombo vya habari.

Sehemu ya 1 ya kijitabu hiki inafafanua misingi ya programu ya taifa ya unawaji mikono. Sehemu ya 2 inajadili jinsi ya kumwelewa mlengwa ili kampeni za unawaji mikono ziweze kubuniwa kwa kuegemea uhalisia wa mlengwa. Sehemu ya 3 inaelezea jinsi mwangaza mpya unavyoweza kuwa kampeni madhubuti katika kubadili tabia ya unawaji mikono. Sehemu ya 4 inadokeza mpangilio au uandaaji wa programu ya kunawa mikono, kutoa habari zinazovuka hatua nyinginezo; sehemu hii imeandaliwa isomwe sanjari na sehemu zilizotangulia. Viambatisho vinatoa mifano ya zana, kama vile zana za utafiti na hadidu za rejea.





VALERIE CURTIS

SEHEMU YA I
Kuweka Msingi
wa Programu
ya Taifa ya
Kunawa Mikono
kwa Sabuni

SEHEMU YA I. Kuweka Msingi wa Programu ya Taifa ya Kunawa Mikono kwa Sabuni

Mwanzo: Je, Hapa ni Mahali na Muda Mwafaka?

Programu madhubuti ya unawaji mikono inaweza kutoa mchango mkubwa katika afya ya jamii. Hata hivyo kuandaa programu hiyo huhitaji muda, raslimali, jitihada, na dhamiri. Ili zifanikiwe, programu za unawaji mikono lazima zishughulikie mahitaji ya kiafya yanayotambulika na ziungwe mkono na wadau wakuu.

Kufanya Uchambuzi wa Haraka wa Hali Halisi

Uchambuzi wa hali halisi unaweza kuonesha kama nchi inayohusika ina mazingira yanayounga mkono programu au kama watetezi wa programu wapo au wanaweza kuandaliwa katika serikali, sekta binafsi, na miongoni mwa wafadhili.

Kiashiria cha kwanza cha mafanikio ni mahitaji ya kiafya kama vile:

- Maambukizi ya magonjwa ya kuhara na yale ya mfumo wa upumuaji ni vyanzo vikuu vya magonjwa na vifo vya watoto;
- Viwango vya unawaji mikono kwa sabuni katika nyakati muhimu viko chini, au angalau vinakisiwa kuwa hivyo; au
- Magonjwa ya kipindupindu, homa ya matumbo, au SARS yatambuliwe kama tatizo.

Ikiwa mahitaji ya kiafya yapo, tathmini ya matakwa na uwezo wa wadau wakuu itasaidia kuonesha uwezekano wa kuanza kwa juhudi na namna ya kufanya maandalizi na uratibu. Makundi mahususi ya wadau na masuala ya kuzingatia ni pamoja na:

Serikali

- Nchi imedhamiria kufikia Malengo ya Maendeleo ya Milenia (MMM) na ina Mkakati wa Kupunguza Umaskini;
- Maji safi na salama, na usafi ni vipaumbele vya serikali; na
- Uwezekano wa kuwepo watetezi katika Wizara za Afya, Elimu, na Maji.

Viwanda

- Soko la sabuni lipo;
- Kuna uwezekano wa kukua kwa viwanda vya sabuni na vingine vinavyohusiana navyo (kampuni za plastiki zinazotengeneza matenki ya kuhifadhia maji), hasa katika maeneo ambayo upatikanaji wa masoko ni mgumu; na
- Viwanda vinatazamia kuinua hadhi na majina yao.

Wafadhili na Washirika Wengineo

- Kuna programu za afya, maji au usafi, ambazo zinaweza kujumuisha unawaji wa mikono;
- Mashirika ya wafadhili yanadhamiria kupata namna mpya za ushirikiano;
- Asasi Zisizokuwa za Serikali (AZISE) zinaweza kuingiza unawaji mikono katika programu zao zilizopo; na
- Makundi mengine, kama vile kampuni za maji, watoa matunzo ya kiafya, na vikundi vya kidini na vya kijamii, yanadhamiria kuchangia kwa kiasi kikubwa katika uga wa afya ya jamii.

Uwezekano wa mafanikio ya programu madhubuti, kubwa, na kwa wakati mwafaka utaongezeka kutokana na mambo kadhaa yaliyopo au yanayoweza kubuniwa.

Ushirika Baina ya Sekta ya Umma na ya Binafsi

Kwa kuwa sekta ya umma na ya binafsi kwa pamoja zina dhamira ya kuhamasisha unawaji mikono, programu za nchi kwa kawaida huchukua sura ya ushirika baina ya sekta ya umma na ya binafsi. Wakati ambapo sekta ya umma inaweza kuwa na hadhari katika kufanya kazi na viwanda na sekta binafsi kwa kushuku kwamba kufanya kazi pamoja na serikali kunaweza kuleta matokeo makubwa, sekta zote mbili ni vyema zikanufaika kutokana na ushirikiano baina yao.

Kwanza, kwa kawaida viwanda huwekeza hasa kiasi kikubwa cha nguvu zake katika kumwelewa mlengwa au mtumiaji wa bidhaa zao ili viweze kuzalisha na kutangaza bidhaa zinazotakiwa. Uhamasishaji wa usafi, kwa ujumla, hukosa utaalumu huu, ambao haupatikani kwa mapana katika sekta ya umma.

Pili, viwanda tayari vimeshawezesha upatikanaji wa sabuni za kuogea na kufulia katika zaidi ya asilimia 90 ya kaya ulimwenguni, vikidhihirisha mafanikio yanayoweza kupatikana kwa kuoanisha utengenezaji wa sabuni na ujenzi wa tabia ya matumizi yake katika jamii. Katika nchi zilizoendelea, viwanda vilifanya kazi kubwa sana katika kubadili mienendo ya kiusafi. Hivyo, vinaweza kufanya vivyo hivyo katika nchi maskini huku vikinufaika na upanuzi wa soko.

Sekta binafsi ina nafasi nzuri ya kunufaika kutokana na ushirikiano baina yake na sekta ya umma, hususan kupitia kupanuka kwa soko. Aidha, faida za kuonekana kama sekta inayochangia katika ufanikishaji wa malengo ya kijamii na inayofanya kazi pamoja na washirika wa maendeleo na wataalamu wa

kimataifa zinaweza kuwa kubwa. Vilevile, viongozi wengi wa kampuni za sabuni hufurahia kuhushwa katika jitihada za kuboresha ustawi wa jamii.

Kwa muhtasari, sekta ya umma hunufaiika kutokana na utaalumu wa masoko na raslimali za viwandani. Zikiungana, pande hizi mbili zinaweza kuanzisha kampeni za afya ya jamii za ushindani—au zinazozidi kabisa—jitihada za masoko za viwanda.

Tayari viwanda vinafanya jitihada za kuhamasisha unawaji mikono kama sehemu ya programu zinazoendelea za masoko au majukumu ya kijamii. Kampuni za *Colgate-Palmolive*, *Procter and Gamble*, na *Hindustan Lever* zina programu za mashuleni katika nchi nyingi zinazoelimisha watoto kuhusu unawaji mikono (kwa maelezo zaidi tazama kisanduku na. 11). Kampuni hizo tayari zinaweza kuwa ni wafuasi wa kuhamasisha unawaji mikono na zikawa tayari kushirikiana na sekta ya umma. Masuala ya majina ya bidhaa na hakimiliki yatahitaji kujadiliwa na kukubaliana.

Viwanda vingine vinaweza kuwa tayari pamoja kuwa na uwezo wa kuchangia raslimali, utaalumu au michango ya hali kwenye ushirika wa sekta ya umma na ya binafsi. Sekta hizi ni pamoja na viwanda vya maji, kampuni za utangazaji na habari, wazalishaji wa matenki na mabomba, kampuni za usafirishaji na uchukuzi n.k. Kwa mfano, nchini Ghana, *Polytank*, kampuni ya plastiki itengenezayo matenki ya kuhifadhia maji, inakusudia kutoa matenki kwa shule mbalimbali kwa bei ya gharama za uzalishaji au ya chini zaidi. Kampuni ambazo hazichangii moja kwa moja zinaweza kuhamasishwa kuweka ujumbe unaohusu unawaji mikono katika bidhaa zao kama vile sabuni, ndoo za kunawia, au karatasi za msalini. Hali hii itaongeza nguvu ya ujumbe wa kunawa mikono katika mazingira yanayohusika. Pale ambapo mashaka yanaweza kuwa kikwazo kwa ushiriki

wa sekta binafsi, itakuwa ni manufaa kuuita ushirika wa sekta ya umma na ya binafsi 'Muungano wa Kunawa mikono'.

Kujenga Hoja ya Kunawa Mikono

Ili programu ya unawaji mikono ifanikiwe, watetezi wake hawana budi kujenga hoja kwa wadau, ambao ni pamoja na serikali, viwanda, na watoaji wa fedha. Uchambuzi wa uwezo, udhaifu, fursa, na matatizo unaweza kuonesha masuala au maeneo gani yanahitaji kushughulikiwa unapotokea uamuzi wa kuwashirikisha wadau hawa. Kwanza, uchambuzi wa uwezo, udhaifu, fursa, na matatizo huangalia masuala ambayo yanaweza kudhibitiwa na wadau ambao ni washirika tarajali katika juhudi hizo (tazama jedwali na. 2).

Pili, mambo mengine yasiyo ya moja kwa moja hutathminiwa. Mambo haya yako nje ya juhudi zenyewe lakini huweza kuleta matokeo chanya kwa walengwa. Jedwali na. 3 litawasaidia wahusika wa harakati kuandaa orodha ya mambo au maeneo ya nje.

Tatu, wadau wanaweza kushirikishwa katika ushirikiano huo ili waweze kushughulikia udhaifu, kujenga au kuongeza uwezo, kutambua fursa mbalimbali, na kupunguza matatizo.

Kujenga Hoja kwa Serikali

Masuala muhimu ambayo yatavuta makini ya serikali ni ukubwa wa matatizo ya kiafya na uhusiano wake na malengo kama vile Malengo ya Maendeleo ya Milenia, gharama za kiuchumi za magonjwa yanayosababishwa na kutonawa mikono, na uhusiano wake na upunguzaji umaskini, na gharama za matibabu na muda wa kazi unaopotea. Uchunguzi wa masuala haya utasaidia kujenga hoja zitakazowashawishi watoa maamuzi kuunga mkono programu za unawaji mikono. Vyanzo



Jedwali na. 2: Mambo ya Kuzingatia katika Uchambuzi wa Uwezo, Udhaifu, Fursa, na Matatizo

Mambo yaliyo katika Udhibiti wa Ndani	Uwezo	Udhaifu
Chanzo cha mapato		
Uzoefu		
Utaalamu		
Uwezo wa kufikia na kuhudumia walengwa		
Uongozi na msaada wa kisiasa		
Suala la vipaumbele katika uandaaji		
Washirika waliopo		
Mengineyo		

Jedwali na. 3: Mambo ya Nje ya Uchambuzi wa Uwezo, Udhaifu, Fursa, na Matatizo

Mambo ya nje	Fursa	Matatizo
Nguvu za kiutamaduni (ikiwa ni pamoja na mielekeo na matukio yanayoathiri amali na mila za nchi)		
Nguvu za kiteknolojia (kuzingatia uwezekano wa teknolojia mpya ambazo zinaweza kuwa nguvu ya ushawishi)		
Mielekeo ya idadi ya watu (inayohusika na kampeni)		
Nguvu za kiuchumi (zinazoweza kuathiri mafanikio)		
Nguvu za kisiasa na kisheria (zinazoweza kuathiri jitihada za kampeni au walengwa)		
Watu wa nje (makundi ambayo yako nje ya harakati na washirika wake ambayo yanaweza kuwa na athari kwa walengwa au mpango mzima)		

vizuri vya taarifa kuhusu viwango vya ugonjwa ni pamoja na tafiti za jumuiya, kama vile tafiti za hali za watu kiafya. (Kutoa taarifa za sehemu na vifaa vya kutolea huduma za afya ni chanzo dhaifu cha data kwa sababu hakiwezi kuonesha viwango vya magonjwa ya kuambukiza kwa jamii.) Gharama za kutonawa mikono kwa jamii na kwa uchumi huweza kukadiriwa kwa kukokotoa gharama za (a) matibabu ya maambukizi yatokanayo na kutonawa mikono; (b) siku za kazi zinazopotea; na (c) vifo vitokanavyo na magonjwa ya kuhara na maambukizi ya mfumo wa upumuaji. Kwa kuongezea, programu ya taifa inaweza kuokoa mamilioni ya fedha kwa kutumia mkabala mpana zaidi, na wenye gharama nafuu badala ya kutumia juhudi za hapa na pale za kuhamasisha usafi (tazama kisansuku na. I).

Programu za maji safi na salama zina mvuto kwa serikali kwa sababu zinahusisha ununuzi na ufungaji au uwekaji wa vifaa. Inaweza kuwa vigumu kujenga hoja kwamba kiasi cha fedha kinachotumika kwa shughuli hii kipelekwe katika suala linaloonekana kama 'laini', la kunawa mikono. Ingawa baadhi ya serikali na mashirika ya kimataifa yanajaribu kuongeza uwekezaji katika suala la usafi, kukubalika kwa suala hili ni kwa polepole sana. Jitihada za uhamasishaji kuhusu umuhimu wa masuala laini ni vyema zikafanyika mara kwa mara na kwa kila fursa inayopatikana.

Kujenga Hoja Viwandani

Ingawa viwanda hupenda kuwa raia mwema, kinachoongoza shughuli za kiwango cha nchi ni faida. Viwanda huwekeza muda, utaalumu, na rasimali pale vinapoonana pana uwezekano wa kupata faida. Kwa hiyo, ni muhimu kufanya makadirio ya uwezekano wa ukuaji wa soko zima la sabuni. Kwa mfano, mtu anaweza kukadiriwa kuwa kila tukio moja la kunawa hutumia gramu 0.5 za sabuni; hii inaweza kuzidishwa kwa idadi ya watu katika eneo lengwa, wastani wa safari ambazo mtu anaweza kunawa mikono kwa kila siku, na idadi ya siku kwa kipindi kinachokadiriwa. Matokeo ya makadirio haya yataonesha ni kiasi gani cha sabuni kinaweza kuuzwa kwa kila mtu. Ikumbukwe kwamba, aina za sabuni zitakazoweza kufaidika ni pamoja na miche ya sabuni ya kufulia, sabuni zinazotengenezwa kienyeji, si zile tu zinazotengenezwa maalum kwa kuogea au kunawia mikono.

Faida nyingine ambazo viwanda vinaweza kupata ni pamoja na kuwa na uwezo wa kuongeza aina ya sabuni zilizopo, kupanua aina zilizopo za sabuni ya kunawia mikono, kuinua hadhi na kuboresha mikataba ya kisiasa. Biashara, zote kubwa na ndogo, zitaweza pia kunufaika na tafiti za masoko na mahusiano ya kimataifa.

Mashirika ya kimataifa yanaweza kuona manufaa makubwa ya kushiriki katika ushirika wa sekta ya umma na ya binafsi, na kuhusisha makao makuu ya kimataifa kunaweza kusaidia katika kuchochea uwekezaji kwa kiwango cha nchi. Kama ilivyokwisha tajwa, viwanda vinaweza, na havina budi,

kufanya kazi kubwa ya kuhamasisha unawaji mikono katika nchi ambamo unahitajika zaidi. Kuvutia msaada wa viwanda hakujathibitika kuwa kazi rahisi kama ilivyokuwa ikitarajiwa. Wakati mapato kiuchumi yanapokuwa mazuri, kampuni za sabuni hujaribu kutoa misaada, lakini mapato yakishuka rasimali zote zilizopo huelekezwa katika maendeleo ya bidhaa.

Kwa kuwa nadharia ya sasa ya ushirikiano wa sekta ya umma na ya binafsi inakataza matumizi ya nembo za kibiashara katika programu zinazofadhiliwa na serikali, matamania ya viwanda kushiriki katika programu hizo yanapungua.

Tatizo hili linaweza kutatuliwa kwa njia mbalimbali. Msaada na dhamiri ya uongozi wa juu vinaweza kuwa muhimu sana katika kuhakikisha utoaji wa fedha na rasimali katika ngazi ya kitaifa. Kampuni aghalabu huomba kuwa na uhusiano pekee wa kibiashara na washirika ambapo hulipa fadhila kwa kuchangia kiasi kikubwa cha msaada. Inawezekana kufungua mlango wa chanzo hiki cha rasimali kwa kuzigawa baadhi ya shughuli na kuruhusu kuzipatia majina ya kibiashara. Hivyo, kwa mfano, nchini Ghana, kampuni ya *Unilever* ingeweza kusaidia programu za mashuleni na kampuni ya *PZ-Cussons* ingeweza kusaidia mpango wa vifurushi vya zawadi kwa hospitali ya wazazi.

Kujenga Hoja kwa Wagharamiaji

Ingawa kiutaratibu hufanya kazi kupitia serikalini, mara nyingi mashirika ya nje ya misaada huwa na ajenda zao na aghalabu vyanzo vyao vya mapato. Kadiri unawaji mikono unapozidi kupanuka katika orodha ya vipaumbele vya kimataifa, viwanda zaidi na zaidi hujiandaa kuwekeza katika uhamasishaji wa unawaji mikono. Ili kuungwa mkono na wafadhili, ni muhimu kutambua vipaumbele vya wafadhili hao, uwezo wa kutoa maamuzi ulipo, pamoja na taratibu za kupata fedha.

Ufanyaji maamuzi kuhusu matumizi ya fedha kutoka mashirika ya misaada ya nchi kama vile Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Denimaki (DANIDA) na Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza (DFID), unaelekezwa zaidi katika ngazi ya kitaifa, na upatikanaji wa misaada yake unaweza kuhitaji ushawishi wa hali ya juu katika ngazi za serikali za mitaa, serikali kuu, na za kimataifa. Mashirika ya kimataifa kama vile Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), yanaweza kuwa na programu zinazoweza kusaidia uhamasishaji wa unawaji mikono katika baadhi ya maeneo ya nchi inayohusika. Mwisho, mikopo ya Benki ya Dunia kwa ajili ya maji safi na salama inaweza kubainisha matumizi katika kipengee cha usafi.

Masuala ya Ugharamiaji Kifedha

Awali ya yote, fedha zinahitajika kugharamia uanzishaji wa programu, ambao kwa kawaida hujumuisha mtu mmoja na/au shirika linaloongoza harakati na linalofanya kazi kama mratibu. Pili, fedha zinahitajika kwa ajili ya utafiti wa mlengwa,



na halafu kukodi shirika la au kampuni ya mawasiliano. Shirika linahitaji bajeti ya vyombo vya habari, mawasiliano ya moja kwa moja na mlengwa, na programu za kiserikali. Hivyo, ahadi za uchangiaji fedha ni lazima zitolewe mapema. Ukusanyaji wa fedha unajadiliwa kama sehemu ya jitihada za ushawishi na uhusiano wa umma katika sehemu za 3 na 4.

Ugharimiaji wa shughuli za vyombo vya habari umekuwa ni changamoto katika nchi nyingi. Sekta binafsi ina fedha

kidogo za ziada. Serikali na wafadhili hutenga fedha chache kwa ajili ya shughuli kama hizi ambazo hazijazoeleka. Hata hivyo, inawezekana kutumia fursa ya serikali au shirika kutataka kuonekana kama mtetezi, hasa pale panapotokea matatizo ya kiafya kwa wananchi, kama vile mlipuko wa kipindupindu au majanga ya asili. Vivyo hivyo, mashirika yanaweza kuwa mstari wa mbele iwapo yatapewa sifa zinazostahili kwa kuchangia kifedha au kivifaa katika shughuli za uhamasishaji.

Kisanduku na. I: Unafuu Kigharama wa Programu za Unawaji Mikono

Ni nadra kwa miradi ya afya kutilia mkazo katika suala la unawaji mikono ili kupunguza gharama za matumizi ya fedha. Hata hivyo, kuna ongezeko la ushahidi kimataifa unaonesha kwamba, uwekezaji katika afya na usafi unaotilia mkazo katika programu za uhamasishaji wa unawaji mikono na nyinginezo za kiafya ni miongoni mwa uwekezaji wa gharama nafuu unaoweza kufanywa kwa kutumia rasimili za umma na za binafsi. Ersey (1991), kwa mfano, anaonesha kwamba uhamasishaji wa usafi aghalabu huhitajika kwa miradi ya usambazaji wa maji na uondoshaji majitaka ili kuifanya miradi hiyo iwe na matokeo bora kiafya kwa watumiaji.

Utafiti wa hivi karibuni wa unafuu kigharama wa programu za unawaji mikono umebuni mbinu sanifu ya kufanyia programu za unawaji mikono uchambuzi wa kiuchumi. Kwanza, uchambuzi wa unafuu kigharama wa miradi ya unawaji mikono hufanywa ili uweze kulinganishwa na umadhubuti wa miradi mingine inayohusiana nayo, pamoja na miradi katika sekta zingine. Kisha, uchambuzi wa gharama na faida ya miradi ya unawaji mikono huandaliwa ili kulinganisha matokeo yake katika muktadha mpana zaidi.

Mbinu hii ilibaini kuwa Programu ya Amerika ya Kati ya Kuzuia Magonjwa ya Kuhara kwa Kunawa Mikono (tazama kisanduku na. 2) ni ya gharama nafuu; inazuia magonjwa ya kuhara kwa Dola za Kimarekani chini ya 10 kwa kila mgonjwa na kuepusha gharama ya Dola za Kimarekani 91.30 kwa DALY*. Hata bila ya uingiliaji kati, upatikanaji wa sabuni, maji, na vifaa vinginevyo katika nchi hizi ni wa kiwango cha juu. Kwa hiyo, uchambuzi wa kiuchumi unaweza kutozingatia gharama hizi na hivyo kupunguza gharama binafsi. Uchambuzi wa unyeti unaonesha kwamba hata tukiangalia kiwango kidogo cha upunguzaji wa magonjwa ya kuhara, miradi ya unawaji mikono bado ina gharama nafuu.

Makadirio yaliyofanywa kwa kutumia mbinu hii kwa mradi wa unawaji mikono wa Peru (tazama kisanduku na.10) katika kipindi cha mwaka 2003 yanaonesha kwamba kuzuia maambukizi ya magonjwa ya kuhara kwa

mgonjwa mmoja pia kuligharimu Dola za Kimarekani chini ya 10, na gharama zilizoepushwa kwa kila DALY zilikuwa ni Dola za Kimarekani 122,70. Kwa tathmini hii, watunga sera sasa, kinadharia, wanaweza kukokotoa na kubadili makisio yao ya awali kuhusiana na unafuu wa gharama wa miradi. Hili linaweza kufikiwa kwa kuweka makundi ya majaribio yatakayotumika katika kubainisha upunguaji wa ugonjwa katika eneo la mradi wa uingiliaji kati.

Matokeo muhimu ya uchambuzi wa gharama na faida yanaonesha kuwa miradi yote miwili ya unawaji mikono huokoa gharama kwa jamii husika. Thamani halisi ya sasa kifaida ya Mradi wa Amerika ya Kati ni Dola za Kimarekani milioni 4.3 katika utaratibu wa kizio cha kiwango cha faida ya ndani ya kiwango cha asilimia 226. Kwa mradi wa Peru, thamani halisi ya sasa kifaida ni Dola za Kimarekani milioni 8.1, katika utaratibu wa kizio cha kiwango cha faida ya ndani ya kiwango cha asilimia 533. Uchambuzi wa unyeti katika miradi yote miwili ni chanya na unathibitisha uokoaji wa gharama kutokana na miradi hii.

Ulinganisho uliofanywa unaonesha kuwa miradi ya unawaji mikono haiwakilishi mizigo mikubwa kwa Wizara za Afya, na kwamba mchango wa washirika binafsi unapendekezwa kwa manufaa ya pande zote. Uhamasishaji wa miradi hii na ushiriki wa baadaye wa sekta binafsi unawezekana kwa makadirio ya faida kwa kila mshirika kwa kuzingatia kile alichowekeza. Wakati ambapo mradi wa Amerika ya Kati unaonesha kwamba upatikanaji wa sabuni uko duniani kote, utumiaji wa sabuni bado unahitaji kuboreshwa, kwa kupendekeza kampeni za unawaji mikono ambazo hatimaye zitaongeza mauzo ya sabuni.

* DALY, *Disability Adjusted Life Year*, ni kiashiria cha mzigo wa maradhi unaodhihirisha jumla ya upotevu wa maisha ya afya, ama kutokana na kifo kisichotarajiwa au ulemavu wa kiasi fulani katika kipindi fulani.

Imedondolewa kutoka kwa Cercone na wenzake, 2004

Kisanduku na. 2: Juhudi za Amerika ya Kati

Juhudi za Amerika ya Kati za kuhamasisha Unawaji Mikono zilianzishwa maalumu kwa lengo la kupunguza maradhi na vifo vya watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano kwa njia ya kampeni ya kuhamasisha unawaji mikono kwa sabuni ili kuzuia magonjwa ya kuhara. Juhudi hizo ambazo zilianzishwa katika nchi tano, zilihusisha hasa ushirika wa sekta ya umma na ya binafsi ambao ndani yake kulikuwa na watumishi kadhaa wa sekta ya umma na wazalishaji wa sabuni wa sekta binafsi. Juhudi zilihamasisha upatikanaji zaidi wa sabuni kwa kusambaza sampuli za sabuni bure, kuendesha matukio ya uhamasishaji na uelimishaji, na kufadhili shughuli kadha wa kadha za vyombo vya habari ili kutoa taarifa na kusambaza habari kuhusiana na uhusiano uliopo baina ya usafi na uzuiaji wa magonjwa ya kuhara.

Sekta ya umma ilitoa msaada wa kiufundi na utafiti wa soko kwa ajili ya kampuni za sabuni, kutangaza ushiriki wa mashirika mbalimbali, na ilisaidia kuunda kikosikazi cha kuratibu na kuelekeza jitihada za wahusika mbalimbali. Mwishowe, mchango mkubwa zaidi wa programu hii ni kule kudhihirisha jinsi malengo ya afya kwa umma yanavyoweza kuoanishwa na malengo ya kibiashara.

Nchini Guatemala, ambapo kumbukumbu za juhudi hizo zilitunzwa vizuri, matokeo yalikuwa:

- Asilimia kumi ya kinamama iliongeza kiwango cha unawaji mikono kutoka 'hatua ya chini kabisa' hadi ama hatua ya 'kati' au ya 'juu kabisa'.
- Kushuka kwa asilimia kumi kwa idadi ya kinamama waliokubaliana na kauli: "Mara nyingi kunawa mikono kwa maji inatoshia."
- Ongezeko la asilimia kumi la kinamama waliokubaliana na kauli: "Nisipotumia sabuni, najisikia siko safi."

Kwa kubashiri kutokana na matokeo haya na mengine ya kutoka vitabuni na makala kuhusu uhusiano uliopo baina ya unawaji mikono na ueneaji wa magonjwa ya kuhara, ilikadiriwa kwamba, "katika kipindi cha uingiliaji kati ueneaji wa magonjwa ya kuhara ulipungua kwa asilimia 4.5 miongoni mwa watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano."

Chanzo: Environmental Health Project (EHP), UNICEF/WES, United States Agency for International Development (USAID), na Benki ya Dunia/WSP na WSSCC, Mei 2004

Muundo na Uratibu


Iwapo tathmini itabaini mazingira yanayofaa, mkutano au warsha ya kwanza na wadau muhimu inaweza kusaidia kuimarisha mawazo pamoja na yale yanayopaswa kuzingatiwa. Ajenda inaweza kujumuisha wataalamu kuonesha umuhimu wa unawaji mikono; kubadilishana mawazo kuhusu dira na matarajio ya mwanzo ya wadau muhimu; na kuweka dhamiri za mwanzo, muundo wa ushirikiano na misingi yake.

Wakati wa kuandaa dira na kuongoza programu, inasaidia kuwa na mratibu au mchocheaji wa nchi. Mtu huyo au shirika hilo

litazamwe kama chombo halali au cha wote na kitoe uelekeo; shauku; stadi za utafutaji masoko; na maarifa ya afya ya jamii, uongozi, na mawasiliano. Mratibu anaweza kuwa katika shirika la serikali, chombo cha sekta binafsi (kama vile shirika mama la ndani la uzalishaji wa sabuni), chama, au asasi isiyo ya kiserikali. Huko Amerika ya Kati, shirika kichocheo lilianzishwa ili kuunganisha washirika wa sekta ya umma na ya binafsi na hatimaye kujiiondoa (tazama kisanduku na. 2).

Sehemu hii imedokeza vipengele muhimu vya kuanzisha programu. Taarifa zaidi kuhusu uongozi na muundo zinaweza kupatikana katika Sehemu ya 4.





SEHEMU YA 2
Kumwelewa
Mlengwa

SEHEMU YA 2

KUMWELEWA MLENGWA

Mkabala wa Kimasoko

Mara baada ya msingi wa kuendeleza mradi wa kunawa mikono kukamilika na muafaka kufikiwa, msisitizo huhamia kwa wanawa mikono wanaoitwa “walengwa” kwa istilahi ya kisoko. Njia pekee ya kubadili mienendo ya muda mrefu inayohusiana na tabia kama vile kunawa mikono ni kuwa na uelewa madhubuti wa sababu zinazochochea na kuwezesha unawaji mikono miongoni mwa walengwa. Mkabala wa kisoko maana yake ni kuyafanya mahitaji ya walengwa kuwa kiini na kuufanya mtazamo wao uamue aina na mawanda ya shughuli zote za uhamasishaji.

Kukidhi haja ndio msingi katika suala zima la soko. Kwa mujibu wa Profesa wa Masoko wa Chuo Kikuu cha Northwestern ambaye pia ni mwandishi, Philip Kotler, “Soko maana yake ni kukidhi mahitaji na matakwa kupitia mchakato wa kubadilishana”.


Watoa huduma huwapatia walengwa kitu wanachohitaji na ambacho wamejiandaa kujitoa, ama kwa matumizi ya pesa, muda, au juhudi. Hivyo basi, kiini cha shughuli ya soko ni kutafiti mambo ambayo walengwa huyahitaji kisha kuwapatia mahitaji hayo kwa njia ambayo itawavutia zaidi.

Kuelewa Tabia


Mahitaji ya mlengwa ni mengi na yanatofautiana. Yanaweza kujumuisha mambo kama kuheshimiwa, kuwa safi, kuridhika na kujisikia vema, na kuhudumia vizuri familia zao. Wakati ambapo mahitaji ya kiafya yanaweza kuonekana kuwa ni mahitaji ya wazi kwa mtazamo wa wataaluma wa afya, kwa walengwa huweza kuwa si jambo muhimu au la kila siku. Kampuni inawekeza zaidi katika kuelewa maisha, matamania na njia za mawasiliano za walengwa ili kuendeleza na kutoa bidhaa bora pamoja na ujumbe mzuri unaohamasisha. Ili kutangaza huduma ya kunawa mikono kwa mafanikio, maswali haya manne hayana budi kujibiwa:

- Tabia hatarishi ni zipi?
- Tabia hatarishi hufanywa na nani?
- Ni vichocheo, desturi, tabia, na/au mazingira gani yanaweza kubadili tabia?
- Watu huwasilianaje?

Majibu ya maswali haya yanatoa vidokezo muhimu vya utafiti wa mlengwa. Mchakato mzima unajumuisha mitazamo ya wataalamu kuhusiana na tabia ya mlengwa, afya, na shughuli ya unawaji mikono; pamoja uelewa uliotolewa na walengwa wenyewe. (Kielelezo na. 2).¹



¹ Zana (kama vile Uchunguzi Pangilifu na Majaribio ya Tabia) miundo na hadidu za rejea (HaRe) zilizotumika katika sehemu hii zinaweza kupatikana katika kiambatisho.



Kielelezo na. 4: Mazingira, Desturi, na Vichochezi

1. *Tabia hatarishi hufanywa na nani?* Programu za unawaji mikono zinalenga makundi ya waltu ambao tabia ya kunawa mikono huweza kuwa ya manufaa makubwa katika kupunguza magonjwa: aghalabu mwangalizi ambaye humpatia mtoto ‘mazingira ya usafi’. Katika maeneo mengi mwangalizi wa kwanza ni mama wa mtoto mdogo; hata hivyo, ni muhimu pia kuweka kumbukumbu za mtu mwingine anayehusika—bibi, dada, baba (katika jamii zingine), shangazi n.k. Watoto wenye umri wa kwenda shule pia huweza kuwa walengwa, si tu kwa sababu wao pia huweza kuwatumia watoto, bali kwa sababu wao ni waangalizi wa baadae. Vilevile, wao huathiriwa kirahisi na mabadiliko ya tabia na ni wepesi kuelewa mwenendo mpya wa afya. Pia wao huweza kuwa wahamasishaji wazuri wa tabia ya unawaji mikono. Wakati mwingine kundi la pili la walengwa (majirani, baba [katika jamii zingine], watoto wakubwa, na watu wengine katika familia) watahusishwa kwa sababu ya athari walizo nazo kwa walengwa wa kundi la kwanza. Mathalani, katika jamii nyingine wanaume huamua ni kiasi gani cha fedha kitumike au kitengwe kwa ajili ya kununulia sabuni kwa kuwa wao ndio wanunuzi wa vitu hivi katika kaya zao.

2. *Tabia hatarishi ni zipi?* Kama ilivyodokezwa, kunawa mikono baada ya kushika kinyesi daima ni njia bora ya kupunguza hatari ya kueneza vijidudu vya magonjwa kwa njia ya kinyesi kilichopitia mdomoni. Hata hivyo, kwa kuwa tabia hii haiko kila mahali, na kwa kuwa usafi huweza kuwa duni, ni muhimu kunawa mikono kwa sabuni kabla ya kugusana, kula, au kumlisha mtu chakula. Hii ina maana kwamba unawaji mikono katika maeneo matatu ni muhimu sana: baada ya kutoka chooni, baada ya kutawadha mtoto aliyejisaidia haja kubwa, na kabla ya kushika chakula. Wakati maeneo muhimu ya unawaji mikono ili kuzuia maambukizi ya mfumo wa upumuaji bado hayajabainishwa, kunawa mikono mara kwa mara ni njia pia ya kujikinga na maradhi yatokanayo na mfumo wa upumuaji.

Ni muhimu kuwa na data sahihi na za kuaminika kuhusu viwango vya unawaji mikono kwa sabuni katika eneo lolote mahususi ili kujua uzito wa tatizo na kuweka malengo yanayopimika ya uboreshaji. Data za msingi kama hizo pia huonesha sehemu ya kupimia mabadiliko ya tabia ya kunawa mikono kwa sabuni katika kipindi chote cha uhai wa programu.

Kwa bahati mbaya, ni vigumu sana kutathmini kwa uhakika unawaji mikono. Tabia za unawaji mikono kwa ujumla ni za kisiriri na ‘zinafungamana na maadili’: watu huhofia kuwa watatazamwa visivyo ikiwa watakiria mapungufu katika tabia zinazohusiana na usafi. Kuwauliza watu kama wananawa mikono yao kwa sabuni wakati wote hutoa majibu mazuri kuliko tabia yenyewe halisi. Mathalani, nchini Ghana asilimia 75 ya kinamama walioulizwa kuhusu kunawa mikono kwa sabuni baada ya kutoka chooni, walijibu ‘ndiyo’, lakini uchunguzi pangilifu ulibaini kuwa ni asilimia 3 tu waliokuwa wanafanya hivyo. Njia pekee ya kuaminika na ya kutegemewa ya kupata kipimo sahihi cha tabia ya kunawa mikono ni uchunguzi wa moja kwa moja, ambapo mchunguzi aliyepata mafunzo hutakiwa kutumia saa kadhaa nyumbani akichunguza na kuweka kumbukumbu za matukio husika nyumbani kwa mlengwa. Ili kupata matokeo sahihi ni vema kuwatumia watafiti wa uwandani waliopewa mafunzo mazuri na wanaosimamiwa vema.

3. *Ni nini huweza kubadili tabia?* Mambo makuu matatu huhusika katika mabadiliko ya tabia: vichocheo, tabia, na mazingira, yanayoweza au kukwaza mabadiliko ya tabia. Kama Kielelezo na. 4 kinavyoonesha, kubadili tabia kutoka hali moja hadi nyingine huhitaji jambo moja au zaidi ya yafuatavyo:

- Kupunguza vikwazo kwenye *mazingira* ili kuwezesha mabadiliko;

- Kubadili *tabia* za zamani kuwa mpya; na
- Kutafuta *vichocho* vinavyoweza kuunda *tabia* mpya.

Kielelezo na. 4: Mazingira, Tabia, na Vichocho

Utafiti wa mlengwa unahusu kuchunguza nafsi ya mlengwa ili kubaini matamano makuu na mambo yanayoweza kuchochea mabadiliko ya *tabia*, kubaini chanzo cha *tabia* na kutafiti namna bora zaidi ya kuanzisha *tabia* mpya, na kuchunguza mambo yaliyopo katika mazingira yanyoweza kukwaza au kuhamasisha mabadiliko ya *tabia*. Mambo haya yanaweza kufikiwa kwa kutumia zana mbalimbali, yakiwemo majaribio ya *tabia* na mahojiano ya kina.

Vichocho na *vikwazo vya kimazingira* ni mambo yanayowezesha au kuzuia *tabia* ya unawaji mikono kwa sabuni. *Vichocho* vinaweza kujumuisha upatikanaji rahisi wa maji na gharama nafuu za sabuni. *Vikwazo* huweza kujumuisha bei ghali za sabuni au sabuni zisizovutia, ukosefu wa vifaa vya kunawia mikono, na vizuizi vya kiutamaduni vinavyokatiza kunawa mikono kwa siku fulani. Kisanduku na. 4 kinaonesha umuhimu wa sifa mahususi za sabuni ambazo zinafanya sabuni ikubalike katika unawaji wa mikono nchini Ghana.

Utafiti wa kiidadi hutoa taarifa za msingi kuhusu mazingira, kama vile upatikanaji wa sabuni, umbali kutoka katika chanzo cha maji, na uwepo wa mazingira ya usafi. Mahojiano ya kina baada ya majaribio ya *tabia* pia yanaweza kusaidia kuonesha *vikwazo* au *vichocho* (angalia zana ya. 1).

Vikwazo vinapaswa kuelewek mapema kisha vishughulikiwe kadiri programu ya mawasiliano inavyoendelea. Mathalani, ikiwa umbali toka katika chanzo cha maji ni kikwazo katika upatikanaji wa maji safi, programu ya mawasiliano inaweza kuonesha kuwa kiasi kidogo cha maji yanayopatikana au yaliyosafishwa baada ya kutumika kinatosheleza. Zaidi ya hayo, wakati ambapo kampeni za mawasiliano zinaweza kushindwa kushughulikia moja kwa moja *vikwazo* bainifu kama vile vya ukosefu wa vifaa vya kunawia mikono shuleni, shughuli za uhusiano mwema na uhamasishaji zinaweza kushawishi wale wenye uwezo wa kusaidia katika kupunguza *vikwazo* kama hivi. Mahitaji ya walengwa wa kundi la kwanza—kinamama na watoto—wanaweza pia kuhimiza kupatikana kwa vifaa vya kunawia mikono inapobidi.

Tabia ni mienendo inayojengeka na kuendelezwa, mara nyingi hukuzwa tangu utotoni. Utafiti umeonesha kuwa mara tu watu mahali popote wanaposharabu *tabia* jengefu na desturi, *tabia* na desturi hizo haziachiki kirahisi. Lengo la uhamasishaji wa unawaji mikono si kufanikisha tukio moja la unawaji mikono, bali ni kupandikiza *tabia* ya kila siku na endelevu itakayojitokea yenyewe kila wakati kunapotokea tukio la uchafu. Wakati ambapo mara nyingi watu hujifunza *tabia* utotoni, kuna fursa za mabadiliko, hususani wakati wa matukio ya mabadiliko ya maisha. Tukio muhimu kwa mama ni kuzaliwa mtoto.

Kinamama wengi hueleza kuwa usafi wa mikono haukuwa jambo muhimu kwao hadi mtoto alipozaliwa na kwamba wakunga au watu wengine waliohusika na kulea mimba au uzalishaji walipopendekeza mama anawe mikono basi alifanya hivyo. Tukio jingine la mabadiliko ya maisha kwa kinamama wengi ni kuhamia nyumbani kwa mume baada ya kuolewa na kujifunza *tabia* mpya za mazingira ya nyumbani.

Tabia huchunguzwa vizuri zaidi kwa kutumia uchunguzi pangilifu (zana ya. 2). Vyanzo vyake vinaweza kuchunguzwa kwa njia ya mahojiano ya kina na mchakato wa kufuata *tabia* mpya zinaoeleweka kwa njia ya majaribio ya *tabia*.

Vichocho ni moduli za asili na za kujifunzwa zilizomo ndani ya akili ambazo huchochea *tabia* mahususi. Hutokea kama hisia na miguso ambayo mtu huibainisha wakati wanapotekeleza *tabia* mahususi. Kugundua *vichocho* ni muhimu katika kuhamasisha kwa mafanikio unawaji mikono.

Kama ilivyo kwa mienendo hatari, kubainisha *vichocho* kunaweza kuwa kazi ngumu kwa sababu (1) Vinaweza kujificha utourazini (Zaltman, 2003); na (2) huweza kuwa fikra za aibu au ghasia kuzibainisha, kwa mfano, kutumia sabuni ili kuongeza mvuto wa kimapenzi. Zaltman anadai kuwa kiasi cha asilimia 95 cha fikra za mwanadamu hufanyika katika uturazini.

Utafiti wa *kitabia* wa kina kuhusu motisha kwa walengwa katika nchi nyingi huonesha ruwaza bainifu za *vichocho* vya *tabia* ya unawaji mikono, kama inavyooneshwa katika jedwali na. 4. Kinamama husukumwa kunawa mikono kwa kuchochewa na ufahari, hadhi, kukubalika kijamii, kuondoa kero ya harufu hali kadhalika uchafu. Pia huchukulia kitendo cha kunawa mikono kama kitendo cha malezi, sehemu ya kuwapenda, na kuwajali watoto. Mara nyingi wanawake huchukulia kuwa uchafu unaoonekana mikononi tu au kuwa na mikono inayonuka ndiyo vyanzo vikuu vya afya duni, na hata hivyo uhusiano bayana kati ya mikono michafu, ugonjwa wa kuhara, na magonjwa huonyeshwa mara chache sana.

Japokuwa inaonekana kuwa kuna baadhi ya motisha zinazokubalika katika tamaduni mbalimbali kuhusu unawaji mikono pamoja na *tabia* pana za usafi, tofauti ndogondogo na jinsi motisha hizo zinavyochukuliwa hutegemea nchi husika, kama ilivyo kwa umuhimu wa kila motisha. Ni kweli pia kwa wahusika tofautitofauti katika walengwa. Kwa mfano, malezi yanaweza yasiwe motisha kuu kwa watoto wa shule. Kwa hali hiyo, utafiti wa walengwa kinchi unahitajika ili kuongoza kampeni thabiti ya kisoko. Jedwali namba 5 linaonesha muundo rahisi wa kubainisha na kuamisha *vikwazo* na *vichocho*, wakati kisanduku namba 3 kinaelezea ripoti ya kinamama kuhusu desturi za kiutamaduni zinazoleta athari juu ya matumizi yao ya sabuni nchini Senegali (zingatia kuwa *vikwazo* hivi ni vya kiimani tu na havina ukweli). *Vikwazo* na *vichocho* vya unawaji mikono kwa sabuni vinaweza kuwa tofauti katika muda maalum wa kunawa mikono. *Vikwazo* hivi vinaweza

Kisanduku na. 3: Imani za Kiutamaduni Zinazokwamisha Tabia ya Unawaji Mikono kwa Sabuni Nchini Senegali

Utafiti wa walengwa nchini Senegali unatoa mifano ya tabia na vikwazo kuhusiana na unawaji mikono kwa sabuni.

Imani za Wahenga na za Kidini

Ingawa haiaminiki sana tena, baadhi ya Wasenegali wana mtazamo wa “bora salama kuliko majuto” kuhusiana na utamaduni wa tabia ya kunawa mikono. Kutumia sabuni wakati wa kutawadha kabla ya kusali msikitini huondoa sehemu ya usafi wa kiroho kwa sababu maji yaliyobarikiwa hayapatani na sabuni.

Baadhi ya wanawake, hasa wa vijijini, bado wanashikilia mazoea ya kutomwogeshwa mtoto chini ya umri wa mwaka mmoja kwa kuhofia kupunguza siku zake za kuishi. Pia wanaamini kuwa kwa kupunguza matumizi ya sabuni wakati wa ujauzito wanaweza kumwepushia madhara mtoto aliyemo tumboni. Aidha baadhi ya wanawake wanaamini kuwa kunawa mikono kwa sabuni kunaweza kupunguza uwezo wa kuzaa.

Falsafa ya Jaala

Kikwazo kikubwa ni mtazamo kuwa mtu hawezi kukwepa lililokwishapangwa: hivyo, kuwa maskini kumepangwa, basi uchafu nao ni sehemu ya umaskini.

kuelezewa vizuri kwa kutumia mfano kwenye jedwali namba 4.

Majaribio ya kitabia ambapo kinamama wa kujitolea (na/au watoto wa shule) wanapewa sabuni na kuambiwa wazitumie kunawia mikono kwa siku saba hadi 10, ni njia nzuri ya kuanza kuelewa motisha za kienyeji za unawaji mikono. Baada ya jaribio kinamama huhojiwa kwa kina kuhusu uzoefu wao, ni jambo gani lilikuwa rahisi, ni jambo gani lilikuwa gumu, jambo gani walilipenda, jambo gani hawakulipenda, n.k. Majadiliano ya kundi lengwa la kinamama na/au watoto wa shule yanaweza kutumiwa kama nyongeza ya majaribio haya ili kuelewa vizuri tofauti ndogondogo za kijamii za unawaji mikono na sababu zinazoambatana nazo pamoja na njia za mawasiliano zinazopendelewa.

Watu wanawasilianaje? Hatimaye, utafiti lazima ubaini walengwa hupata wapi taarifa; ufikiwaji wa njia mbalimbali za mawasiliano—zote mbili, za asili na za kisasa; njia gani huaminika na kukubalika; na lugha zinazofaa zaidi kutumia. Ufanisi wa njia mbalimbali za mawasiliano utatofautiana miongoni mwa walengwa.

Kuna vyanzo vikuu viwili vya taarifa katika njia za mawasiliano. Chanzo cha kwanza ni data zilizopo. Katika nchi nyingi, asasi za kibishara zinakuwa zimeshakusanya maelezo ya kina kuhusu matumizi ya vyombo vya habari, inawezekana ikijumuisha hata mienendo ya kinamama na ya watoto ya kusikiliza na kutazama vyombo hivyo Uchunguzi wa Idadi ya watu na Afya pia ni hukusanya taarifa hizi. Nchini Peru, vyombo vya habari vilikuwa ni vyanzo vikuu vya data kuhusu ufikiwaji na usikilizaji wa habari.

Jedwali na. 4: Vichocho, Tabia, na Mazingira ya Unawaji Mikono kwa Sabuni (Maeneo Manne)

	Ghana	Kerala, India	Senegali	Wirrali, Uingereza
Vichocho	Kumlea mtoto Kuchukia uchafu Kukubalika na jamii	Kuchukia Kukubalika na jamii Kuilea familia	Fahari/hadhi Chukizo Malezi Ushawishi	Chukizo Hadhi/fahari Malezi Ujumi
Tabia	Kichanga Kufundishwa na mama	Kuhamisha kaya Kichanga	Maji tu, bila sabuni, ni mazoea	Kichanga Kujifunza toka kwa mkunga
Mazingira: Viwezeshaji/ Vikwazo	Umbali kwenda choo cha umma	Wanaume hudhibiti sabuni	Mila za kienyeji	Hali inayofaa Kusahau

Jedwali na. 5: Kubainisha Vikwazo na Vichocheo vya Unawaji Mikono kwa Sabuni katika Matukio Muhimu

	Tabia Lengwa (kwa Kinamama)		
	Nawa mikono kwa sabuni baada ya kutumia Choo	Nawa mikono kwa sabuni baada ya Kumtawadha Mtoto aliyepata Haja kubwa	Nawa mikono kwa sabuni kabla ya Kushika Chakula
Vikwazo			
Vichocheo/ faida			

Kisanduku na. 4: Walengwa wa Ghana Wanapendelea Sabuni zenye Matumizi Mengi, Zinzodumu na za Bei Nafuu

Kwa manufaa ya utafiti, wanawake nchini Ghana waliulizwa ni mambo gani huyapendelea katika sabuni za kunawia mikono. Katika kueleza sifa wanazozipendelea kwenye sabuni walitaja sifa mbalimbali—harufu, gharama, umbo na uimara—uwezo wake wa kutumika kwa madhumuni mengi.

Harufu ilikuwa sifa muhimu kuliko nyingine zote. Kwa ujumla, harufu ya ndimu ilikuwa maarufu sana. Hata hivyo, sabuni zenye harufu kali zilikuwa zinapendwa kwa matumizi ya kunawia baada ya haja kubwa, ambapo sabuni zisizo na harufu kali zilipendwa sana kwa matumizi kabla ya kula: wanawake walihofu kuwa sabuni zenye harufu kali zitapunguza raha ya kula. Mmoja alisema, “Hutakuwa na hamu ya kula ikiwa chakula kitanukia sabuni.”

Gharama: Kwa ujumla, sabuni za gharama nafuu zilipendwa zaidi, ingawa wakati mwingine wanawake walikuwa tayari kulipa gharama kubwa kama sabuni ilikuwa kubwa au walidhani kuwa ingedumu.

Umbo/uimara: Kuhusiana na gharama, wanawake walipendelea sabuni ngumu za mche au za maji za aina

mbalimbali, kwani walidhani kuwa zilikuwa zinadumu. Upendeleo wa sabuni ngumu ulikuwa thabiti kiasi kwamba wengi walihifadhi sabuni zao sehemu za baridi au zenye jua kali ili kuzifanya ziwe ngumu zaidi kabla ya kuzitumia. “Hukata katika vipande na kuziweka katika sakafu ya baraza ili kuzikausha na kuzifanya ziwe ngumu ili zidumu.”

Sabuni za maji, mbali ya kuwa za gharama nafuu—hutumika kwa kiasi kidogo tu kila mara mikono inapooshwa. “Kwa kutumia sabuni ngumu, unahitaji kumwomba mtu wa kukumiminia maji mikononi, lakini kwa kutumia hii huhitaji msaada wa mtu yeyote.”

Hizo ndizo sababu madhubuti zilizowafanya wanawake kununua sabuni ya maji kwa gharama kubwa kuliko ya mche: “Ninailoweka kwenye maji, ninaikoroga, na kuimimina kwenye chupa ya zamani ya kunyonyeshea.”

Matumizi mengi: Kwa sababu inahusiana na uchumi, wanawake wengi walipendelea sabuni za kufulia za mche ambazo zinaweza kutumika kwa madhumuni mengi. “Hii ni sabuni pekee ninayonunua, kwani ninaweza kuitumia kuoshea vitu vyangu na wakati huohuo kuogea pia.”

Hata hivyo, unapotumia data zilizopo, ni muhimu kuzikamilisha kwa utafiti wa uwandani ili kujifunza zaidi kuhusu njia za kienyeji na kubaini mitandao ipi ya mawasiliano—ya kienyeji au ya kisasa—huaminika na/au hukubalika. Watu huweza kuvitilia mashaka vyombo vya habari, hasa pale ambapo kuna udhibiti mkubwa wa serikali wa vyombo hivyo, na viwango vya msambao huweza kuwa chini miongoni mwa wanawake. Hivyo basi, chanzo cha pili cha taarifa ni mahojiano na sampuli wakilishi ya walengwa. Mahojiano kama hayo hulenga katika maingiliano ya watu na njia mbalimbali za mawasiliano, iwe kwa mdomo, njia za kienyeji, njia za kiserikali, mashirika ya kijamii, vyombo vya habari n.k. Kielelezo namba 5 kinaonesha njia mbalimbali za wanawake kijijini Kerala, India.

Utafiti wa kitabia unaweza kusaidia kutoa picha ya njia za mawasiliano kwa mtazamo wa kinamama, hasa kuhusiana na njia za kienyeji za mawasiliano (ambazo zinaweza zisipatikane katika data za kitaifa). Utafiti huu huweza kuchunguza njia zenye ushawishi mkubwa na za kuaminika kuhusiana na mawasiliano ya unawaji mikono. Mathalani, nchini Burkina Faso, ilibainika kuwa ingawa wapigambiu wa kienyeji walikuwa ndio wapelekaji wazuri wa taarifa walionwa na jamii kuwa si wasafi, matokeo yake hawakufaa kubeba ujumbe wa unawaji mikono.

Kubuni na Kutekeleza Utafiti wa Mlengwa

Malengo ya Utafiti wa Mlengwa ni kujibu, kwa njia inayofaa na rahisi, maswali manne ya hapo juu. Tabia hatarishi ni zipi?


Kisanduku na. 5: Dokezo kuhusu Shule

Kwakuwa hutoa njia rahisi na ya kudumu kuhusiana na mabadiliko ya tabia, shule ni lengo zuri la programu za unawaji mikono. Shule ni mazingira muhimu, si tu kwa kujifunzia kunawa mikono, bali kwa kuanzisha tabia kwa vitendo. Watoto mara nyingi huwa na shauku ya kubadili tabia, na maswali ya utafiti yanawahusu watoto wenye umri wa kwenda shule, walimu, watawala, hali kadhalika kwa walengwa wengine.

Katika nchi nyingi, shule ni sehemu ya pili ya kujenga tabia baada ya kaya. Watoto huweza kutumia hadi saa nane kwa siku kwa miezi zaidi ya minane kwa mwaka shuleni, na muda mwingine wakiwa na marafiki zao. Maandiko kuhusu tabia za walengwa huonesha kuwa watoto hawafurahii kuitwa majina mabaya au mawasiliano ya kiutani kwa kiwango sawa na watu wazima, hivyo mbinu tofauti ya mawasiliano shuleni huhitajika. Mienendo hatarishi inayofanyika shuleni pia ni tofauti na za nyumbani. Vifaa maalumu vya kutafiti tabia za watoto wa shule na sababu zake vinabuniwa na baadhi ya vidokezo kuhusu kuatafiti watoto wenye umri wa kwenda shule vimeoneshwa katika zana ya 4.



Kielelezo na. 5: Jinsi Kinamama wa Kerala, India Wanavyowasiliana: Taarifa za Mawasiliano kwa Mwezi



Kisanduku na. 6: Mwongozo wa Njia za Utafiti

Uchunguzi pangilifu ni kuchunguza moja kwa moja tabia inayolengwa (unawaji mikono kwa sabuni na njia zinazofaa zaidi katika kufikisha ujumbe) na wafanyakazi wa uwandani wakiantika kumbukumbu ya kile wanachokiona kwa kutumia muundo unaokubalika. Njia hii inaweza kuwa ngumu, ghali, na ya ghafla, lakini inayotoa matokeo sahihi ya upimaji wa tabia kuliko njia nyingine yoyote ile. Watafiti hufika asubuhi sana, hukaa kimya sehemu wanayoweza kuona tabia za majumbani za kinamama na watoto kisha kuziandika, mathalani, kile kinachotokea hasa baada ya tukio la mtoto kujisaidia haja kubwa. Aghalabu tabia hubadilika kutokana na uchunguzi, lakini kama kinamama huambiwa kuwa wafuatiliaji wanachukua kumbukumbu ya kazi za nyumbani, au afya ya mtoto, hubadili kidogo tabia ya unawaji mikono. Watafiti wa uwandani huhitaji mafunzo makini, msaada na usimamizi ili kuleta uwiano wa mkabala. *Mahojiano ya mlengwa* yanahusu mahojiano sanifu ya kiidadi na husaidia kufafanua walengwa na mazingira yao. Maswali yahasuyo uchumijamii pamoja na yale yahasuyo maji, usafi na vifaa vya kunawia mikono huulizwa, na yote huchunguzwa. Seti ya maswali sanifu kuhusu fursa za aina zote za mawasiliano pia huulizwa. Maswali yote hupangwa na hutumia majibu yaliyoandaliwa kabla. Miundo huhitaji kufanyiwa majaribio kwanza ili ikubalike katika hali husika. Mahojiano ya mlengwa hufanywa vema na waangalizi wa watoto mara tu baada ya uchunguzi pangilifu. *Mijadala ya kundi lengwa* huhusisha kuwaomba idadi ndogo ya watu kujadili mada zinazohusiana na tabia

husika. Kwa kuwa walengwa hujumuisha kinamama na watoto, kila kundi litajumuishwa kivyake katika mijadala ya kundi lengwa. Pengine mijadala ya kundi lengwa ni vizuri zaidi ikitumiwa katika shughuli za kupanga madaraja (kupanga kimadaraja shughuli za nyumbani, vitu muhimu katika maisha, matumizi ya sabuni, aina za sabuni za kunawia mikono, njia bora za mawasiliano n.k.) ili kufikia muafaka wa masuala yanayoweza kuathiri tabia za unawaji mikono na kubainisha uwiano wa watu wanaoegemea mitazamo fulani.

Majaribio ya kitabia na mahojiano ya kina: watu wanaojitolea kwa ajili ya majaribio ya kitabia, ambao kwa kawaida huchaguliwa miongoni mwa wanakikundi lengwa, hupewa sabuni na kuambiwa waitumie mara kwa mara kunawia mikono. Mama hutembelewa mara kwa mara ili kukumbushwa. Baada ya siku saba mpaka 10, huhojiwa kwa kina kuhusiana na uzoefu wake katika kutumia sabuni: alipenda jambo gani na hakupenda nini, jambo gani lilikuwa rahisi na lipi lilikuwa gumu na alitumia suluhisho gani kwa matatizo aliyokumbana nayo. Majaribio haya huweza kurudiwa tena baada ya siku saba au kumi zingine kwani tabia hubadilika. Majaribio kama haya yanayofuatiwa na mahojiano ya kina yakifanywa ipasavyo, yanaweza kuonesha sababu na vikwazo vya kunawia mikono kwa sabuni. Udadisi wa kina ni muhimu katika kujua chanzo cha tabia. Ili kujua chanzo hiki, mtafiti hurudia swali “Kwa nini?” mpaka itakaposhindikana kabisa kupata sababu nyingine ya chanzo cha tabia.

Jedwali na. 6: Mpango Muhtasari wa Utafiti wa Mlengwa

Lengo	Maswali Mahsusi (siyo yote)	Njia	Sampuli inayopendekezwa
1. Nani hutekeleza tabia hatarishi?	1.1 Sifa za walengwa ni zipi (sifa oza kiuchumi-jamii, kiidadi ya watu, au za kielimu n.k)	Mahojiano yanayoongozwa na madodoso Kama inavyooneshwa kwenye matini	Kama ilivyo hapo chini
2. Tabia hatarishi ni zipi?	2.1 Kiasi gani cha sabuni hutumiwa na mtu mmoja kwa wastani? 2.2 Sabuni hutumika kwa kazi gani, na nani? 2.3 Aina gani za sabuni hutumika kwa kazi gani? 2.4 Mikono huoshwa katika mazi mazingira gani na mara ngapi? Kwa/bila sabuni? 2.5 Sabuni inanunuliwa wapi? 2.6 Upatikanaji wa vifaa vya kunawia mikono	Uchunguzi pangilifu Mahojiano yanayoongozwa na madodoso baada ya uchunguzi pangilifu Mijadala ya kundi lengwa juu ya sifa za sabuni	Sampuli wakilishi katika mafungu manane, jumla ya kaya 400 Kaya 400 Mijadala ya makundi lengwa 5
3. Nini kinaweza kuchochea mabadiliko ya tabia?	3.1 Kwa nini wale ambao kwa sasa hawanawi mikono kwa sabuni na wale hufanya hivyo? 3.2 Ni faida na hasara zipi huhusishwa na kunawa mikono kwa sabuni? 3.3 Nini hukwaza matumizi ya sabuni? 3.4 Mambo gani huhamasisha matumizi ya sabuni ya mche? 3.5 Muktadha: Tabia za mahali husika: vyanzo vya maji, huduma za usafi	Majaribio ya tabia Mahojiano ya kina baada ya majaribio ya tabia	Kaya 40 za kujitolea Kaya 40 za kujitolea
4. Watu huwasilianaje?	4.1 Ufikiaji wa njia za mawasiliano zilizopo (mf. vyombo vya habari, njia za kiserikali, njia zisizo za kiserikali, njia za kienyeji) 4.2 Kufaa kwa njia za mawasiliano zilizopo	Mahojiano yanayoongozwa na madodoso, data za kitaifa zilizopo Mahojiano ya kina	Waangalizi 400 wa watoto Sampuli ndogo za wanakaya wanaume 200 na watoto 200 wenye umri wa kwenda shule Kaya 40 za kujitolea kama hapo juu
5. Uchunguzi wa shule	5.1 Tabia zi lizopo 5.2 Motisha 5.3 Vikwazo 5.4 Wahusika wakuu	Makundi lengwa yenye watoto, mahojiano ya kina na wahusika wakuu	Shule 20

Kisanduku na. 7: Vidokezo Muhimu katika Kuingia Mkataba wa Utafiti wa Mlengwa

Lazima ifahamike wazi kutoka mwanzo na isisitizwe kila mara kwamba programu za uhamasishaji wa unawaji mikono si miradi ya kienyeji ya afya ya umma. Bali ni programu zinazomlenga mlengwa zinazokusudia kujua vichocheo vya kina vya mlengwa dhidi ya unawaji mikono kwa sabuni. Mahojiano ya juujuu hayatoshelezi. Kwa mfano, anayeshinda mkataba anapaswa kufahamishwa kwamba, pale walengwa wanapoulizwa kama wananawa mikono yao kwa sabuni jibu lao mara nyingi ni “ndiyo”. Kwa kawaida watu hujibu maswali ya dodoso kama vile walikuwa wanajibu mtihani au wanapimwa ubora wao, hivyo humweleza mhojaji kile wanachoamini kuwa ni jibu “sahihi”.

Timu iliyo na uzoefu wa utafiti wa kibiashara wa mlengwa ndiyo inayopendekezwa zaidi kuliko ile yenye uzoefu katika kufanya kazi zinazohusu programu za afya za umma.

Watafiti wa uwandani wanatakiwa kutumia lugha za wenyeji.

Mara tu baada ya kuajiriwa, watafiti wanahitaji mafunzo ya kina ili kuhakikisha kuwa maswali yanayotakiwa yanaulizwa kwa kwa kina maridhawa. Mathalani, tafiti nyingi kuhusu unawaji mikono zinaonesha kuwa walengwa hunawa mikono yao kwa sababu ili wawe “safi”. Hata hivyo, haya si matokeo mazuri. La muhimu hapa ni kuelewa maana ya “usafi” katika muktadha huu na vipengele vyake vyote—mwonekano, saikolojia, na kijamii—ni muhimu zaidi.

Mtafiti lazima azingatie maswali manne na taarifa mahususi zinazohitajika. Wakala achunguze undani wa kila swali na kuhakikisha kuwa anapata matokeo ya kina ili kutoa nafasi ya mkakati wa kisasa, na mchakato wa kiubunifu wa kuhamasisha mabadiliko ya tabia miongoni mwa walengwa.

Kama ilivyo kwa kazi zote za mikataba, ubora wa kazi ni kutimiza matakwa ya mteja. Mteja lazima aelewe masuala yote kwa kina, ajue nini hasa kinahitajika, na amsisitizie mtafiti wake umuhimu wa kutimiza anayoyataka. Wateja lazima watembelee

uwandani ili kuhakikisha kuwa utafiti inaendelea uwandanini kulingana na malengo mahususi. Ziara za kushtukiza zitasaidia kuibua umakini katika timu ya watafiti.

Uchunguzi wa kitabia (mf. Mahojiano ya kina) hayawezi kufanywa na watafiti lakini lazima ufanywe uwandanini na wataalamu wa anthropolojia au saikolojia wenye sifa na ambao wamepata mafunzo. Msaada toka katika timu ya kimataifa ya ufundi ya wafanyakazi wa afya katika sekta ya umma na ya binafsi unaweza kuhitajika ili kuhakikisha kunakuwepo utafiti madhubuti na ubora unaokubalika.

Data zote, za kiidadi na kitabia, ni muhimu. Mahojiano ya kitabia lazima yarekodiwe kwenye kanda za sauti, yatafsiriwe na yanukuliwe; yaandikwe na tarehe, muda na maelezo ya wahojiwa; kisha zirudishwe kwa mteja kwa ajili ya kuhifadhiwa. Data za kitabia zote lazima zihakikishwe na nakala ya seti ya data ipelekwe kwa mteja.

Uchambuzi wa data pamoja na kuziripoti lazima zingatie maswali yaliyooneshwa katika hadidu za rejea. Uchambuzi na kuripoti ya data lazima kujibu maswali manne ya msingi.

- Sifa za walengwa ni zipi?
- Kuna tabia na desturi zipii?
- Vichocheo, tabia na mazingira ya unawaji mikono kwa sabuni ni yapi?
- Njia kuu za mawasiliano zinazotumiwa na walengwa ni zipi?

Wakati wa kuchambua data na kuandika ripoti ya mwisho, wakala lazima alenge kazi yake katika maswali manne makuu ya utafiti kama yaliyooneshwa hapo juu. Inapendekezwa pia kutumia jedwali namba 5 kufupisha vikwazo na vichocheo muhimu vya mabadiliko ya tabia.

Kutegemeana na kiwango cha uzoefu wa timu, mteja anaweza kuhitaji kupanga uchambuzi wote unaohitajika na wakala.

Kisanduku na. 8: Utafiti wa Mlengwa: Upendeleo wa Kimantiki

Tunajua kuwa tabia ni matokeo ya vichocheo au motisha. Huzinduka wakati ubongo unapopokea taarifa kutoka kwenye mazingira (mfano kuona juisi ya tofaa) au mwili (mf. kuishiwa nguvu, njaa). Vichocheo vingi huweza kufanya kazi mara moja, na ubongo huruhusu kimoja au kingine kufanya kazi. Vitendo rahisi (vinavyohitaji juhudi ndogo) vitapewa nafasi zaidi kuliko vile vigumu. Ijapokuwa, mara nyingi inadhaniwa kuwa mawasiliano yahusuyo faida ya kiafya ya unawaji mikono hutoshia kuchochea tabia, ni kichocheo kimoja tu miongoni mwa vichocheo vingi muhimu na mara nyingi si madhubuti, ingawa watu huweza kujaribu kuvihalalisha na kuelezea tabia zao kwa maneno ya kiafya.

Utafiti wa mlengwa unakuwa mgumu kutokana na tabia iliyoenea ya kuhalalisha na kuelezea tabia kwa namna ambayo inamfanya mtu kuvutia mbele mhojaji. Hata hivyo, vichocheo vikubwa vya tabia ya mwanadamu si razini. Watu huvisikia baadhi ya vichocheo kwa njia ya hisia. Akikumbana na mhoji, mama hujisikia kama amelazimika kujieleza. Huweza kujisikia kama vile yuko shuleni tena akijaribu kutoa jibu sahihi katika jaribio. Anaweza akajaribu kukumbuka masomo kuhusu usafi, vimelea, na magonjwa. Akiulizwa kwa nini hunawa

mikono, atajitahidi kutoa maelezo ya kimantiki: “Kujikinga dhidi ya magonjwa”. Programu za kawaida zinazohamasisha masuala ya afya zinarithika na majibu ya aina hiyo na kusahau kuwa yanaweza kuwepo mengine mengi pamoja na vichocheo vingi vyenye nguvu ya kubadili tabia kuliko hofu ya maradhi.

Hata kama mhojiwa anajua sababu zake mwenyewe, kunaweza kuwepo sababu nzito za kijamii za kutozikubali sababu hizo: Nani atakiri kuwa anataka kuwa na mvuto kwa watu wa jinsia tofauti au kuwa na hadhi ya juu katika jamii?

Watafuta masoko wanalijua hili na wanahakikisha kuwa matangazo yao yanakuwa na ujumbe wa kidhima na ujumbe wa kihisia. Wanatoa sababu za kimantiki za kwa nini wanamvutia mlengwa anunue bidhaa zao au abadili tabia. Mfano mzuri ni aina moja kubwa ya karatasi za msalani ya huko Uingereza: matangazo yake hudai kuwa ni aina hiyo ni bidhaa bora kuliko zote na hutumia kitoto kizuri cha mbwa kuwasilisha ujumbe huu. Ukweli ni kwamba karatasi hizi hazina tofauti na zingine, na ni ghali lakini watumiaji wanavutiwa nazo kutokana na mwitikio wa hisia zinazosababishwa na hiki kitoto kizuri cha mbwa (Buchholz na Wordemann, 2001).

Tabia hatarishi hufanywa na nani? Ni vichocheo, desturi, tabia, na/au mazingira gani yanaweza kubadili tabia? Watu huwasilianaje?

Jedwali namba 6 linatoa ufupisho muundo wa utafiti wa mlengwa katika programu ya taifa ya unawaji mikono. Muundo unajumuisha (a) uchunguzi pangilifu 400 wa tabia ya kinamama; (b) mahojiano yanayoongozwa na madodoso 400 na kinamama walewale baada ya uchunguzi pangilifu; (c) mahojiano yanayoongozwa na madodoso 200 kwa walengwa wengine wakiwemo wanaume viongozi wa kaya na watoto wenye umri wa kwenda shule; (d) makundi lengwa 5 yenye kinamama walengwa kuhusiana na sifa za sabuni na mawasiliano; (e) majaribio ya kitabia 40 yakifuatiwa na mahojiano ya kina; na (f) moduli ya kuchunguzia shule.

Uchunguzi pangilifu ni ghali. Idadi inaweza kupunguzwa toka 400 hadi 200 hivi kama zimekusudiwa mahususi kutoa taarifa kwa programu tu na si kwa ajili ya msingi wa kupimia mabadiliko. Idadi kubwa ni muhimu na hufaa sana kutolea mamlaka ya kitakwimu katika kugundua mabadiliko muhimu

ya tabia. Kama utafiti umelenga kuweka msingi, mahesabu yenye maelezo toshelevu lazima yafanywe kwa kuzingatia makisio ya viwango vya unawaji wa mikono kienyeji na athari tarajiwa za programu. Kiambatisho kinaonesha fomula na maelekezo ya jinsi ya kufanya mambo haya.

Kiasi kilichopendekezwa kitatoa picha nzuri ya hali ya nchi kuhusiana na mienendo ya unawaji mikono na sababu zinazokwamisha, kuwezesha, na kuhamasisha mienendo ya unawaji mikono kwa sabuni katika hatua muhimu, ili mradi tu njia zilizomo katika jedwali namba 6 zihitaji wataalamu wa kutoa utaalumu wao wenye misingi ya uchumi-jamii, jiografia na utamaduni. Uchunguzi pangilifu na mahojiano yanayoongozwa na madodoso hutoa picha ya haraka ya tabia ya unawaji mikono, sababu za kijamii kiidadi ya watu, na njia za mawasiliano. Baada ya uchambuzi, data hizi huripotwa kwa kiuwiano na kiasilimia. Makundi lengwa na majaribio ya kitabia hutumia mkabala tofauti; lengo ni kudadisi kwa kina idadi ndogo ya watu kuhusiana na vichocheo, tabia pamoja na mazingira ya unawaji mikono. Data hizi huandikwa kama

nyaraka huwasilisha mawazo makuu katika nafsi ya mlengwa katika muktadha wa nyumbani. Njia zimefafanuliwa kwa kina hapa chini.

Tafiti huchukua miezi miwili ya uwandani zikiwa na timu ya watu wanane hadi 14, ukijumuisha eneo lote lililokusudiwa/nchi nzima, na huweza kugharimu dola za Kimarekani 20,000-hadi 80,000.

Uongozaji na Usimamiaji wa Utafiti wa Mlengwa

Wakala aliyechaguliwa kufanya utafiti anahitaji kuwa na historia katika utafiti wa mlengwa na lazima aoneshe uwezo wake wa kupata sampuli wakilishi ya taifa na aweze kushughulikia data za kitabia. Utafiti utaboreshwa zaidi kwa kutumia michango ya wataalamu wa masoko wa sekta binafsina/au wataalamu wa kimataifa wa unawaji mikono ambao watasaidia katika kutoa mafunzo kwa timu inayohusika na utafiti wa mlengwa; kusaidia kazi inayohusu ubora pale ambapo hakuna uzoefu wa kazi hii; na kuchambua matokeo.


Uchambuzi na Kuripoti Matokeo

Mara baada ya ukusanyaji wa data kukamilika na kuhakikishwa, data huchambuliwa na shirika la utafiti. Data hizo hutumika kujibu maswali yale manne. Data za kiidadi huwasilishwa kwa

kutumia majedwali, na zile za kitabia huchambuliwa kulingana na mada kuu: vichocheo, tabia; na sababu za kimazingira, vikwazo, na viwezesaji. Awamu kadhaa za uchambuzi wa data na utoaji wa ripoti huweza kuhitajika ili kuandaa ripoti itakayokidhi mahitaji ya programu. Data za uwandani pamoja na nyaraka za majadiliano ya makundi lengwa na za mahojiano ya kina lazima zitolewe pia, kwa kuwa, hususani kuhusiana na nyarakawa, huweza kuwa malighafi bora kabisa ya kuandalia mkakati bunifu.

Ni muhimu kwa kamati kuu au kamati ya ushauri kujumuisha watu wanaoweza kupitia ripoti kwa makini. Wataalamu wanashauri kupitia ripoti ya kiidadi, angalau, kuangalia kuwa data ni sahihi na kwamba uchambuzi wa pili kuhusiana na baadhi ya vipengele vya utafiti kwa njia ya maelezo na ya majedwali unatoa matokeo sawa na yale ya mtafiti. Kuhusiana na data za kitabia ni muhimu kusoma baadhi ya nakala ambazo hazijachambuliwa na kujenga hisia za kile kinachoelezwa na watu. Ufafanuzi unaweza kutofautiana toka kwa mtu mmoja hadi mwingine, kwa hivyo inawezekana mtafiti akakosa mambo madogomadogo muhimu. Katika tafiti zote mbili, za kiidadi na za kitabia, nii kawaida kwa watoa huduma kufanya tena uchambuzi wao wenyewe kwa kutumia data zilizotolewa na wakala wa utafiti wa masoko. Ni vigumu sana kwa utafiti wa uchambuzi wa kitabia kufanyika vizuri, hivyo ni muhimu upitiwe kwa makini.





SEHEMU YA 3
Utekelezaji
wa Programu

SEHEMU YA 3

Utekelezaji wa Programu

Kuandaa Kampeni

Upangaji wa Kampeni za unawaji mikono kwa sabuni unaweza kuanza baada ya kukamilika kwa kiunzi cha ushirikiano pamoja matokeo ya utafiti. Matokeo ya utafiti yanapaswa kutoa taarifa zote zinazohitajika: mienendo mikuu itakayolengwa; walengwa ni nani; vikwazo ni vipi; desturi na mazingira ni yapi; maelezo kuhusu njia sahihi za mawasiliano. Wataalamu wazoe fuu wa masoko wa viwanda vya sabuni wanaweza kutoa utaalumu na kusaidia shughuli zote zilizoenezwa katika sehemu hii.

Kutumia Masoko Mseto

Masoko mseto mara nyingi yakitambulishwa kama Bidhaa, Bei, Mahali, na Uhamasishaji—huweka kiunzi kwa ajili ya kubuni programu madhubuti ya unawaji mikono.

Bidhaa humaanisha vitu halisi au huduma inayoweza mabadiliko ya tabia; huweza kujumuisha mabadiliko ya kimazingira au misaada. Bidhaa zihusianazo na unawaji mikono hujumuisha vifaa vya kumiminia sabuni, na maji, pamoja na mabeseni.

Bei humaanisha vivutio vya kifedha na visivyo vya kifedha kama vile gharama za sabuni na maji na muda unaohitajika kunawa mikono.

Mahali humaanisha usambazaji wa bidhaa na hali za kufaa, kama vile umbali wa vyanzo vya maji na upatikanaji wa sabuni.

Uhamasishaji humaanisha mawasiliano ya ushawishi, na hujumuisha ujumbe muhimu, aina za vyombo vya habari, na vichocheo vya kimazingira.

Wakati andiko hili kwa kiasi kikubwa huhusika na ‘P’ ya nne—uhamasishaji, programu ya nchi huweza pia kulenga kuhamasisha suluhu za kibidhaa (mfano, kuwezesha upatikanaji wa vimiminio vya maji mashuleni), bei (mfano, kushawishi serikali kupunguza kodi ya mauzo ya sabuni), na mahali (mfano, kushawishi kuunganisha mabomba ya maji na vimiminio vya sabuni mashuleni).

Kutayarisha Uhamasishaji

Walengwa na Ugawaji katika Vikundi

Ugawaji humaanisha mchakato wa kugawa walengwa katika vikundi vyenye tabia na mahitaji yanayofanana. Ugawaji hufanyika ili wahamasishaji waweze kushughulikia mahitaji ya kila kikundi cha walengwa. Kila kikundi kitahitaji mikakati tofauti ya masoko. Vikundi vya msingi vya walengwa katika programu za unawaji mikono hujumuisha (a) mama wa watoto wenye umri chini ya miaka mitano; (b) waangalizi wengine wa watoto wenye umri chini ya miaka mitano; na

(c) watoto wenye umri wa kwenda shule walioko mashuleni na sehemu nyinginezo.

Ugawaji zaidi huweza kugawa wale wasionawa mikono yao kabisa (huenda wakawa wale waliochelewa kutekeleza tabia hii, au wasioelekea kutekeleza tabia ya unawaji mikono kwa sabuni) kutoka kwa wale ambao tayari huonawa mikono yao, lakini kwa maji tu (wale waliojiunga na mwenendo huu, walio tayari kukubaliana na ujumbe wa unawaji mikono). Katika hali fulani italazimu kugawa walengwa katika makundi ya kikabila au kidini. Vikundi vingine huweza kujumuisha walengwa wa vijijini na mjini. Bila kujali jinsi walengwa walivyogawanywa, ni muhimu kuhakikisha kuwa ujumbe ni sahihi kwa makundi yote.

Pia, kuna ugawaji wa *pili* wa walengwa, walengwa wanaotarajiwa kusaidia na kushawishi mabadiliko ya tabia miongoni mwa makundi ya mwanzo. Makundi haya ya pili huweza kujumuisha (a) baba wa watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano; (b) mama wa kambo; (c) walimu; na (d) wafanyakazi wa idara ya afya.

Ugawaji wa tatu huweza kuwa ni walengwa wa kampeni za uhamasishaji/uhusiano wa umma za kusaidia programu. Hawa hujumuisha wadau muhimu wanaoweza kusaidia kuvuta dhamiri za wanasiasa. Wanaweza pia kusaidia katika maeneo kama vile uwekaji wa vifaa vya kunawia mikono mashuleni au katika vyoo vya umma na kuingiza unawaji mikono katika programu zao. Wadau hawa huweza kujumuisha (a) viwanda; (b) serikali; (c) vyombo vya habari; na (d) mashirika ya maendeleo (mashirika ya kimataifa, mashirika makubwa, asasi zisizo za serikali, na jumuiya za kiraia).

Mifano mingine ya malengo madhubuti hujumisha kushawishi serikali kupunguza ushuru katika malighafi za sabuni. Pia, kushirikiana na mashirika ya maendeleo ili kupanga miradi ya miundombinu sambamba na uhamasishaji wa usafi kunaweza kuhakikisha uwekaji wa bidhaa zinazohusiana na unawaji mikono, kama vile vituo vya maji.

Mashirika, Dhana, na Majaribio

Mipango madhubuti iliyoandaliwa vizuri ni msingi wa kuwa na kampeni yenye mafanikio, na utumiaji wa mashirika yenye utaalumu wa mawasiliano ni muhimu. Mashirika mazuri yana stadi za kubadilisha maono ya walengwa na kuwa programu madhubuti za mabadiliko ya tabia. Hata hivyo, matokeo ni kama inavyoelezwa kwa ufupi hapa chini. Mashirika ya mawasiliano yana wajibu wa kubadilisha malengo na ufahamu wa walengwa kuwa kampeni madhubuti za mawasiliano. Mashirika haya huanza na mchakato huu kupitia ‘taarifa ya ubunifu’, andiko linalobuniwa kubainisha mawanda ya kazi wanayotarajia kuifanya. Taarifa inapaswa kuwasilishwa

kwenye timu ya mawasiliano pamoja na muda wa majadiliano na uibuaji wa mawazo. Taarifa inapaswa kuwa wazi kadiri iwezekanavyo na ijumuishie mambo muhimu manne yafuatayo:

1. Jukumu la kazi.
2. Jukumu la mawasiliano: (a) walengwa ni nani?; (b) Wanafanya nini/wanafikiria nini sasa?; na (c) Tunataka wafanye nini/wafikirie nini?
3. Yapi ni *maoni finyu*, kituo chetu cha kipekee cha mauzo? Yaani, lipi ni lengo letu moja, faida moja tunayotaka kuwasilisha kwa walengwa? (Faida hii lazima iwe *inaloaminika*).
4. Jukumu la utekelezaji, hujumuisha hisia ambazo mawasiliano yatakuwa nazo.

Utafiti wa walengwa umetoa vipengee muhimu vya taarifa, ambavyo ni (a) sifa za walengwa; (b) tabia zilizopo; (c) vichocho, vikwazo, na mazingira; na (d) ramani ya njia za mawasiliano.

Taarifa ya mwisho hujadiliwa, kwa pamoja, na shirika na mteja. Shirika la Lintas Ghana limetoa mwongozo juu ya “Taarifa Kamilifu” (tazama Kisanduku na. 9). Pamoja na taarifa, mteja anapaswa kutoa ripoti kamili ya utafiti wa walengwa, ikijumuisha maandishi ya mahojiano na vikundi lengwa na vidokezo vya maono vilivyopatikana kutoka katika utafiti. Taarifa hii itachangia katika uelewa wa shirika wa tabia zinazopendwa, walengwa, na njia za mawasiliano.

Kufuatia vikao vya taarifa ya mwanzo, meneja wa mahesabu wa shirika atoa taarifa ya ndani kwa ajili ya timu ya ubunifu. Kasha, mchakato wa ubunifu hujirudiarudia pamoja na vikao vya mara kwa mara vya mashirika na wateja. Ni muhimu kuwa wazi katika mchakato wote huu. Uzoefu wa viwanda ni muhimu, hivyo ni muhimu kwa utaalamu wa sekta binafsi kutumika wakati wote wa kuunda mkakati wa mawasiliano. Timu kuu yenye uzoefu na masuala yote ya utafiti na mkabala unapaswa kudumishwa katika mchakato wote, jambo ambalo mara nyingi hufanyika kwa miezi kadhaa.

Mkakati wa Kibunifu wa Senegali

WATU WAZIMA

Malengo:

- Kufuata tabia ya kunawa mikono kwa sabuni baada ya kutumia choo, baada ya kumbadilishia nguo mtoto, kabla ya kula, kabla ya kumlisha mtoto na kabla ya kupika
- Kurithisha tabia hii kwa watoto na watu wengine wa karibu

Walengwa: mama na walezi wa watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano

Manufaa:

- *mvuto*, usafi, kunukia vizuri, na kuwa na afya njema
- kujikinga dhidi ya magonjwa, uchafu, harufu mbaya, na aibu

Hali: chanya na yenye bashasha

Mwitikio unaotarajiwa:

Kwa afya yangu na ya familia yangu, mimi hunawa mikono kwa sabuni

Vyanzo:

- Utafiti wa mlengwa uliofanyika nchini Senegali mwishoni mwa mwaka 2003
- Uzoefu wa programu za unawaji mikono katika nchi zingine

WATOTO

Malengo:

- Kufuata tabia ya kunawa mikono kwa sabuni kabla ya kula na baada ya kutumia choo
- Kuonesha mfano huu kwa watu wengine

Walengwa: watoto wenye umri wa miaka 6-12

Manufaa:

- utuvu na kukubalika kwa watu wengine
- kujisikia vizuri (kimwili na kiakili)

Hali: tuvu, “ya ndani kwa ndani”, na yenye kutia hamasa

Mwitikio unaotarajiwa:

Ninanawa mikono kwa sabuni, na ninajisikia vizuri na safi sana
Nisiponawa mikono kwa sabuni, nitaonekana sifai kwa vijana wenzangu

Vyanzo:

- Uchunguzi katika shule za msingi za Dakar
- Uzoefu wa programu za unawaji mikono katika nchi zingine
- Msimamo wa mkakati wa watu wazima

Kisanduku na. 9: Taarifa Kamilifu

Wakati wa maandalizi ya harakati za Unawaji Mikono za nchini Ghana, shirika la utangazaji la Lintas lilitolewa kuandaa vifaa vya kampeni. Haikumchukua muda mteja, Kamati ya uendeshaji wa harakati za unawaji mikono nchini Ghana, kubaini kwamba mafanikio ya uandaaji wa vifaa vya kampeni yalitokana na taarifa ya kibunifu iliyobuniwa na kuandaliwa vyema. Kampuni ya Lintas-Ghana iliwasilisha miongozo yake ya uandaaji wa *Taarifa Kamilifu* wakati wa warsha ya kiufundi kuhusu unawaji mikono duniani iliyofanyika mwaka 2003.

Madhumuni ya Taarifa

- Kuandaa matangazo mazuri
- Kujenga au kuwasilisha uelewa wa kawaida wa kazi
- Kuhamasisha
- Kutayarisha chombo cha kupimia matokeo

Uhusiano baina ya Shirika na Mteja

Uandaaji wa taarifa ni mchakato wa timu unaojumuisha:

- Kushirikiana na shirika
- Kupokea andiko la rasimu mapema, kisha kulishughulikia upya
- Kupata ridhaa kutoka kwa wadau wote
- Timu madhubuti (ndogo, yenye msimamo)
- Kubainisha majukumu na kumwezesha kiongozi
- Kuandaa dira ya pamoja
- Mikutano ya kufurahisha, yenye ufanisi na malengo bayana yanayoeleweka kwa wote

Hatari dhidi ya Usalama

- “Kama huwezi kuonwa, huwezi kupata chochote”: Bill Bernbach, mwandishi maarufu wa matangazo ya biashara na mwanzilishi wa *DDB Worldwide*
- Utangazaji wa Anodini ambao hauna uasili na usiofurahisha hauwezi kuwa na ufanisi
- Utangazaji unaojitokeza sana hubeba hatari
- Timu ndogo, yenye uongozi mzuri ina ujasiri wa kukabili/kupambana na hatari hii na kuandaa mawasiliano yanayoshangaza, yenye mvuto na ya kukumbukwa

Mipango na Utafiti

Kijue kile unachotaka ukifikie

- Mabadiliko ya kifikra
- Mabadiliko ya kitabia
- Kiasi (ngapi, kufikia lini)
- Dokeza, kisha wajue walengwa—kiidadi na kisaikolojia—maono maujudi, vibamba vya dhahabu, vichocheo, na vikwazo. Namna wanavyopata taarifa au habari wanazoziamini
- Mkakati wa mawasiliano

Kiongozi wa timu

- Mtu mwenye uzoefu zaidi na masoko
- Kiongozi mwenye uwezo wa kuhamasisha
- Aliyewezeshwa kufanya maamuzi kwa niaba ya timu nzima
- Mwenye utayari kila wakati na kila msingi kufanya maamuzi ya mwisho
- Asiwe mtu wa kukwaza au kukwamisha wengine bali mwezesaji

Maudhui

- Rahisi: ukurasa mmoja, hakuna istilahi
- Hakikifu (yaepuke hisia binafsi)
- Tunazunguma na akina nani?
- Wanafikiria nini sasa? Mahitaji yao ni nini?
- Tunataka wafikirie nini? Kauli zenye fikra moja ambayo ni muhimu kwa maisha ya walengwa
- Kwa nini watuamini?
- Mahitaji/miongozo ya kiutekelezaji

Kipindi cha kuwasilisha Taarifa

- Wasilisha taarifa ukiwa ana kwa ana na timu ya ubunifu
- Kuwa mbunifu, ifanye taarifa yako ionekane ya kuvutia na iwe uzoefu wa kukumbukwa maishani
- Kubali kubadilika kwa kuzingatia hoja zinazoibuliwa na timu
- Kuwa mcheshi na uifanye taarifa yako iwe ya kuburudisha

Kutathmini utangazaji

- Utangazaji upimwe kulingana na taarifa: Je, tangazo linatoa taarifa? Je, linaweza kuiwasilisha?
- Je, kuna wazo moja linaloyanganisha matangazo yote yanayotolewa katika vyombo mbalimbali vya habari?
- Je, tangazo linashangaza?
- Je, tangazo linafurahisha?
- Je, tangazo ni la kukumbukwa?

Taarifa isiyo kamilifu

- Taarifa ya mdomo (haina uzito sawa na ile ya maandishi)
- Taarifa iliyosheheni maneno magumu, finyazo, vifupisho na machaguo mbalimbali
- Taarifa isiyoeleweka kuhusiana na bajeti au upangaji muda wa utekelezaji
- Taarifa iliyokuwa na mjadala
- Taarifa inayoomba itokee miujiza, yaani, yenye malengo magumu kutekelezeka, yasiyojali wala kuzingatia vikwazo vilivyopo vya kiutendaji
- Taarifa ina kauli ya fikra moja yenye pande mbili

Chanzo: Colin Charles, *Lintas Ghana* (Agosti, 2003)

Kwanza, matokeo ya utafiti hutumika kuandaa dhana au misingi kadhaa. Misingi hii huandaliwa na kujaribiwa na shirika la utafiti linalojitegemea ili kujua mwelekeo upi wa ujumbe unaweza kusababisha mabadiliko ya tabia. Dhana zinazofaa zaidi hatimaye huendelezwa zaidi hadi kuwa habari fupifupi kwa ajili ya matangazo ya luninga na redio na kuwa mwongozo wa

kuandaa wa mabango ya matangazo. Habari za matangazo huoneshwa katika mabango ambayo pia hujaribiwa tena kwa walengwa kwa ajili ya kutathmini uaminikaji, mvuto, na nguvu yao ya kubadilisha tabia. Kzi hii hufanywa na shirika la utafiti la kujitegemea. Michakato ya kujaribu dhana na mabango ya matangazo hufanana; kama inavyooneshwa katika kisanduku na. 7.

Jedwali na. 7: Faida na Hasara za Mikabala Tofauti ya Mawasiliano

Mkabala	Maelekezo	Faida	Hasara
Vyombo vya habari	Ujumbe unaotolewa usambazwe kupitia mchanganyiko wa redio, televisheni, mabango, na njia nyinginezo	Gharama nafuu, ujumbe unakuwa wa kukumbukwa kwa kiasi kikubwa, njia inaweza kuinua mtazamo wa kisiasa wa harakati za unawaji mikono, ni rahisi kufuatilia	Njia hii inahitaji safari nyingi sana za utoaji wa tangazo (mara 6+) ili kuathiri mabadiliko ya tabia. Walengwa hawawezi kuchangamana, Ni vigumu kugharimia
Mawasiliano ya moja kwa moja na mlengwa	Matukio yaandaliwe na uongozi wa mashirika yenye utaalamu katika jambo hili, na yaendeshwe mashuleni, sehemu za umma, vikundi vya kijumuiya	Walengwa wanaweza ikuchangamana vizuri, athari zake ni kubwa, yanaweza kuwa ya kukumbukwa	Gharama ni kubwa Mashaka kuhusiana na athari na ukomo wa idadi ya walengwa
Njia za Umma	Kutumia uwezo wa mashirika ya kiserikali kutoa ujumbe wa unawaji mikono kupitia shule na vituo vya afya	Uwezekano mkubwa wa kuendelezwa, iwapo uhamasishaji wa unawaji mikono utakuwa sehemu ya mtaala, na iwapo maelekezo yatatolewa kwa kinamama wanaojifungua	Ni vigumu kudhibiti Kushusha motisha ya wafanyakazi, Kukutana na walengwa kunaweza kusiwe kwa mara kwa mara na hii inaweza kusababisha kufikiwa kwa watu wachache tu, na uwezo mdogo wa kufuatilia shughuli

Ni muhimu kujipa muda katika mchakato wa ubunifu kwa ajili ya kujaribu na kujaribu tena dhana; mabango ya matangazo; na rasimu za matangazo, kwa kuwa uchujaji ndio utakaoongeza mafanikio ya kampeni.

Mikakati Anuwai ya Kubadili Tabia

Programu za unawaji mikono hutegemea njia mbalimbali za mawasiliano kama vile vyombo vya habari na mawasiliano ya moja kwa moja na wateja. Kama inavyoelezwa katika jedwali namba 7, vyombo vya habari huweza kujumuisha luninga, redio, na mabango. Mawasiliano ya moja kwa moja na wateja hujumuisha shughuli zinazofanywa na asasi za udhibiti wa matukio na asasi ziliyopo, kama vile serikali za mitaa, mashule, mamlaka za afya, asasi zisizo za serikali, maeneo ya biashara za rejareja, makanisa, misikiti, n.k. Kadiri mchanganyiko wa njia za mawasiliano katika eneo husika unavyokuwa madhubuti, ndiyo kampeni itakavyokuwa madhubuti pia.

Vyombo vya habari (luninga, redio, mabango): Njia za mawasiliano kama vile luninga, radio, intaneti, vipeperushi na mabango zikitumiwa zinaweza kuwafikia walengwa wengi zaidi kwa gharama nafuu zaidi kwa kila mtu. Kwa hiyo, njia hizi huweza kuwa za gharama nafuu zaidi. Hata hivyo, kwa upande wa mapungufu ni kwamba mawasiliano kupitia vyombo vya habari yanachukuliwa kuwa dhafu katika kuleta mabadiliko ya tabia ikilinganishwa na mawasiliano moja kwa moja na makundi au

na mtu mmoja mmoja kutokana na ukosefu wa fursa ya makusano baina ya walengwa.

Mawasiliano ya moja kwa moja na walengwa: Mikutano ya hadhara, maigizo ya mitaani, senema za hapa na pale na matukio mengine maalumu yanayoendeshwa na mashirika ya kitaalamu ya mawasiliano ya moja kwa moja na walengwa, hali kadhalika vipindi vya elimu mashuleni na kwenye vituo vya afya, yanaweza kuwafikia watu wengi zaidi, iwapo matukio ya kutosha yataendeshwa. Umadhubuti wa mkabala huu haujachunguzwa sana, na elimu ya afya kimakundi imekuwa na matokeo yasiyoaminika kuhusu tabia. Hata hivyo, wahusika huamini kuwa wakati mawasiliano ya moja kwa moja na walengwa ni ghali zaidi kwa mtu anayefikiwa kuliko yale ya vyombo vya habari, nguvu yake ya kubadili tabia kwa kipindi kirefu ni kubwa zaidi kutokana na uimara zaidi wa mawasiliano na fursa ya makusano baina ya walengwa.

Mawasiliano ya serikali na mashirika wanayoshirikiana: Katika ulimwengu bora, wafanyakazi wote wa serikali wa afya, wafanyakazi wa usafi, waalimu wa shule, na wafanyakazi wengine wangeweza kuanzisha unawaji mikono katika kila fursa ya kukutana na walengwa. Hata hivyo, wafanyakazi hao wana vipaumbele vingine, na mbinu maalum zitahitajika iwapo unawaji mikono unatakiwa kuwa moja ya vipaumbele vyao. Msingi wa kufikia mafanikio ya mawasiliano haya ni kuundwa

kwa kundi la mawakala waliohamasika na waliopewa mafunzo ya hali ya juu. Si rahisi kufikia jambo hili katika juhudi za unawaji mikono kama ilivyo kwa programu nyingine yoyote ya afya. Hata hivyo, juhudi za kujumuisha uhamasishaji wa unawaji mikono katika ufafanuzi wa majukumu ya kazi za walimu na wafanyakazi wa afya zinaweza kuwa njia mojawapo ili kufikia suluhisho la kudumu. Kampeni ya vyombo vya habari pia inaweza kusaidia kuhamasisha wafanyakazi wa serikali katika kueneza ujumbe wa unawaji mikono. Matukio mahsusi katika vituo vya afya, kama ugawaji sabuni bure katika vifurushi vya zawadi kwa kinamama waliotoka kujifungua, vile vile kuinua hamasa ya wafanyakazi wa afya na kutoa vichocheo kwa kinamama waliojifungua kujifunza tabia mpya kwa ajili ya manufaa ya watoto wao wachanga.

Matumizi ya *dhamiri* yanaweza kuongeza uwezekano wa mabadiliko ya tabia. Kliniki zinaweza kuhimizwa ziwape kinamama waliojifungua “vyeti” vya kuheshimu dhamiri yao katika unawaji mikono yao kwa sabuni katika tukio muhimu. Vyeti hivi vinaweza kugawiwa kwa kinamama waliojifungua na watoto kwenye matukio ya kijamii (tazama “Mawasiliano ya moja kwa moja na walengwa” hapo juu) na kwa watoto mashuleni mwao. Kuzawadia watu kadiri wanavyoendelea kudumisha tabia mpya, hata kwa zawadi ndogondogo mfano beji au vibandiko au sifa za kawaida kunaweza kuwa muhimu katika kuwatoa watu kutoka katika jaribio moja au unawaji mikono kwa sabuni hadi kwenye uendelezaji wa tabia hiyo.

Wanafunzi wanaweza kuwa na zawadi za afya za kila mwezi, wakati kliniki zinaweza kuwazawadia kinamama waliojifungua kwa kuendelea kunawa mikono yao kadiri watoto wanavyokua.

Kuweka nembo katika bidhaa: Kuhakikisha kwamba ujumbe wa unawaji mikono unabebwa kwenye bidhaa zinazohusiana na unawaji mikono kwa sababu inaweza kudokezea haraka kuhusu unawaji mikono kwa sabuni katika tukio muhimu. Makampuni ya vyakula yanaweza kuhimizwa kuandika ujumbe au nembo kwenye bidhaa za vyakula ili kuwakumbusha watu wanawe mikono kabla ya kula au kutayarisha chakula, wakati makampuni ya kutengeneza sabuni yanaweza yaweka ujumbe huu kwenye makasha ya sabuni. Kwa mfano, kampuni moja ya sabuni huko Ghana inakusudia kuanzisha ufungaji mpya wa sabuni wenye rangi sawa na picha za kwenye kampeni ya unawaji mikono. Jambo hili halihitaji kuongeza gharama za ziada lakini linaweza kuhitaji ushawishi na uhusiano wa umma. (tazama hapo chini).

Uhusiano wa Umma na Ushawishi

Wakati ambapo shughuli za vyombo vya habari na mawasiliano ya moja kwa moja na walengwa zinalenga kubadili tabia ya unawaji mikono kwa kinamama na watoto, uhusiano wa umma na shawishi unalenga kujenga na

kudumisha usaidizi wa juhudi hizi kutoka makundi mapana zaidi ya wadau—walengwa wa tatu waliotajwa hapo juu kwenye “walengwa na ugawaji katika vikundi”. Ikiwa utatumiwa kikamilifu, uhusiano wa Umma unaweza kuwa zana madhubuti inayochochea na kuendeleza shauku, inayotaraji na kushughulikia uenezi hasi na inayoongeza nguvu ya athari ya kampeni.

Programu za unawaji mikono zinahitaji ushawishi wa mwanzo wa pamoja ili kuwaleta pamoja wadau wote muhimu, lakini ushawishi siyo shughuli ya mara moja tu. Wakati wa hatua za mwanzo za programu, itasaidia kama kutakuwepo na ziara ya wataalamu wa kimataifa ili kuhamasisha unawaji mikono na kuongeza umadhubuti wa programu: si kila mtu anaweza kuona jinsi unawaji mikono ulivyo suala muhimu sana. Ushawishi vilevile unahitajika wakati wa uhai wa programu ili kuwaweka pamoja wadau wakati wote na kuwadokeza washiriki wapya ambao wanapata wafanyakazi. Lengo kuu la ushawishi ni wafanyaji maamuzi kama walibainishwa katika uchanganuzi wa wadau. Daima inakuwa ni busara kuwalenga watu ngazi za juu kadiri inavyowezekana: Mawaziri Wakuu na Mawaziri, pia watendaji wakuu na wawakilishi wa nchi. Itakuwa ni muhimu sana vilevile kuwatambua wapinzani wanaoweza kujitokeza na kuwapa taarifa kamili na hatimaye kuwaweka katika kambi yetu. Migogoro kuhusu hali ya programu inaweza kusababisha habari mbaya zinazoweza kuharibu sana au hata kudidimiza kabisa programu za unawaji mikono (tazama kisanduku na. 10).

Uhusiano wa umma unalenga makundi ya wadau wanaoweza kushawishi umma, fedha, na utaalamu. Makundi hayo hujumuisha:

- Vyombo vya habari vinavyoendeleza habari na matukio yanayobainisha matokeo ya utafiti, matukio ya kampeni, na mafanikio, na kuchochea ujumbe wa unawaji mikono;
- Mawakala wa serikali wanaoshawishi maofisa ili kuunga mkono na kuhamasisha programu katika taasisi na bajeti zao na kuinua mazingira ya uendeshaji;
- Sekta binafsi inayovishirikisha viwanda vya sabuni na wadau wengine wa sekta binafsi katika kutoa utaalamu na msaada wa kifedha kwa ajili ya kubuni na kutekeleza kampeni ya unawaji mikono au kubeba ujumbe wa unawaji mikono na nembo katika bidhaa zao ili kuwakumbusha watu kunawa mikono katika tukio muhimu; na
- Kusaidia mashirika yanayojenga utayari na mapenzi katika maendeleo ya jamii ili kupata msaada wa kifedha, kuunganisha msaada wa kiufundi, na kuhitimishwa kwa ujumbe wa unawaji mikono katika programu na miradi.

Mpango wa Uhusiano wa Umma

Madhumuni ya Mpango wa Uhusiano wa Umma ni kujenga mwamko na kuwezesha. Haya hufikiwa kupitia njia mbalimbali, kama vile taarifa kwa vyombo vya habari, hotuba

na mihadhara, na matukio. Mambo muhimu wakati wa kuandaa Uhusiano wa Umma ni:

Fahamu walengwa: Aina zipi za taarifa ambazo vyombo vya habari hupenda kuziandika? Ni vyombo gani vya habari ambavyo hupendwa sana na wadau husika? Ni mambo yapi yamekuwa gumzo kwa wadau yanayoweza kuhimiza au kukwaza unawaji mikono? Nani wanaweza kushughulikia vikwazo vya unawaji mikono vilivyoibuliwa katika utafiti, kama vile kodi kubwa ya uagizaji malighafi ambayo husababisha kupanda kwa bei za sabuni au uhaba wa vifaa vya kunawia mikono shuleni? Kama ilivyo kwa maeneo yote ya jitihada za unawaji mikono, maarifa ya ndani ya kila kundi la wadau ni muhimu wakati wa kuandaa ujumbe mzuri.

Himiza mawasiliano na ushirikiano baina ya walengwa: Hakikisha kuwa mashirika tofauti yanawasiliana na kushirikiana. Msaada binafsi utahimiza ujumbe wa unawaji mikono, kuupa hadhi na kuchochea utatuzi wa matatizo.

Anza mapema: Uhusiano wa Umma ni hatua ya mwanzo ya juhudi za unawaji mikono. Hatua nyingi zisizo rasmi za uundaji ushirikiano zitaweka msingi wa Uhusiano wa Umma.

Mwanzoni, Uhusiano wa Umma utaweza kuelezea umuhimu wa kunawa mikono kwa sabuni. Kisha, baada ya kupata matokeo ya utafiti, Uhusiano wa Umma utaweza kudokezea mahitaji mahususi ya nchi ya kunawa mikono.

Kisanduku na. 10: Somo la Uhusiano wa Umma: Unawaji mikono huko Kerala, India

Ikiwa sehemu ya Ushirika wa Kidunia wa Unawaji Mikono, programu ya unawaji mikono ilianzishwa huko Kerala, India mapema mwaka 2001. Chini ya uwezesaji wa Benki ya Dunia na Mpango wa Maji na Usafi, serikali ya Kerala ilishirikiana na Chama cha Watengenezaji wa Sabuni na Karatasi za msalani cha India katika kuanzisha mpango wa kuhimiza mwamko wa unawaji mikono nchini kote. Kiwanda kikubwa kabisa cha binafsi cha sabuni nchini India cha Hindustan Lever, na mjumbe muhimu wa Chama cha Watengenezaji wa Sabuni nchini India, kilitekeleza jukumu muhimu la kuunda ushirikiano baina ya sekta binafsi na ya umma. UNICEF, Taasisi ya Usafi na Dawa za Kitropiki ya London na Mashirika kadhaa yasiyo ya Kiserikali yalishirikishwa pia.

Wakati mchakato wa kubuni programu ya unawaji mikono na mpango wa utekelezaji, upinzani ulianza kutoka kwa jamii, wanaharakati wa mazingira na wapinga utandawazi walianza kuikosoa programu hiyo kupitia magazetini na kwenye majarida. Wanaharakati hao waliungwa mkono mara moja na makundi yenye ushawishi mkubwa kama vile madaktari, magazeti ya ndani ya nchi, na wanasiasa wa upinzani. Hoja za msingi katika ukosoaji wao zilikuwa ni: (a) uteuzi wa Kerala kwa ajili ya programu hiyo kwa kuzingatia viashiria vya maendeleo ya hali ya juu ya watu wake (b) uhusiano usio bayana kati ya unawaji mikono na kuimarika kwa afya (c) athari mbaya zinazotokana na kuongezeka kwa hisa za soko za makampuni ya kimataifa ya sabuni dhidi ya viwanda vya sabuni vya wenyeji na vya ndani ya nchi (d) madai kwamba Serikali kuu ilikuwa inatekeleza tu matakwa ya Benki ya Dunia. Kutokana na kupigwa vita na vyombo vya habari pamoja na muda mrefu wa kutotekelezwa kwa mpango, baraza la mawaziri liliamua kuutelekeza mpango huo mnamo Agosti 2003.

Je, matatizo katika Kerala yangeweza kuepukwa au kutatuliwa ipasavyo? Ushirikiano mzuri uliobuniwa baina ya mhisani aliyejitolea, kiwanda cha sabuni, na wazo la awali la Serikali la kuwa na programu ya unawaji mikono uliyeyuka kutokana na ukosoaji wa vyombo vya

habari. Mpango wa Uhusiano wa Umma ungeweza kuchangia katika:

Usimamiaji mzuri wa vyombo vya habari: Majibu pekee dhidi ya ukosoaji uliofanywa na vyombo vya habari yalikuwa ni taarifa ya serikali ya kutounga mkono ambayo iliyotolewa miezi sita baadaye. Ufafanuzi na taarifa za mara kwa mara zingesaaidia sana katika kuifanya programu iungwe mkono na vyombo vya habari.

Wadau walioeleweshwa vizuri: Sio wadau wote muhimu ambao walijisikia kwamba walishirikishwa wakati wa kubuni Programu na kuandaa mpango wa utekelezaji.

Ushirikishwaji wa biashara ndogondogo: Japokuwa viwanda vya ndani na vidogo vidogo vya sabuni vilishirikishwa, programu hii haukueleweka vyema kwa wote hali iliyozua hisia kuwa viwanda vikubwa vya kimataifa vingekuwa na ukiritimba wa soko.

Wadau walioeleweshwa vizuri: Kulizuka hisia kwamba kumeundwa kampeni ya kuuza sabuni za kampuni moja tu na kwamba harakati zote hizo zilikuwa zikisukumwa na mhisani mmoja tu. Hakika, kampeni haikuwa ikitangaza kiwanda au bidhaa yoyote mahususi, na shirika zaidi ya moja linalotambulika kimataifa lilishirikishwa vizuri.

Wakati huohuo mwanasiasa alidai kuwa ingekuwa vyema kwa Serikali kutumia fedha katika kuwapatia wananchi huduma ya maji salama na miundombinu ya usafi kuliko kunawa mikono. Hoja hii ilishadidiwa kwa dai kuwa maji salama na juhudi za usafi ni halisi na zinaonekana, wakati juhudi za kimawasiliano kama vile ya kunawa mikono ni mambo ya kupita tu, si halisi hivyo kuna uwezekano mkubwa wa upotevu na matumizi mabaya ya fedha za umma. Hata madaktari walitilia shaka faida za kiafya za kunawa mikono kwa sabuni. Taarifa za faida za kunawa mikono pamoja na misingi ya ufuatiliaji na tathmini vingeweza kusambazwa kwa watunga sera, majimboni, na kwa mabingwa wa afya wenye majukwaa ya kubadilishana mitazamo.

Fungamanisha Uhusiano wa Umma na juhudi pana za mawasiliano: Mkakati wa mawasiliano unapokuwa ukiandaliwa, shughuli za Uhusiano wa Umma itabidi zifungamanishwe na vyombo vya habari na kampeni za moja kwa moja za watumiaji. Hatua hii italeta matokeo mazuri kupitia ufasaha wa ujumbe, mpangilio wa muda unaostahili, pamoja na utambulisho wa kampeni [nembo, rangi n.k.]. Kwa kifupi Uhusiano wa Umma hauna budi kushabihiana na upeanaji habari, iwe mtaalamu wa Mahusiano ya Umma ameshirikishwa au la.

Vyombo Mseto vya Habari

Hatua ya pili ni ukadiriaji wa athari za njia tofauti za mawasiliano kwa walengwa. Kwa kutumia rasilimali zinazofaa ni muhimu kutafuta ni mchanganyiko gani wa njia za mawasiliano utakuwa wa gharama nafuu. Hatua hii ni sayansi inayofahamika vyema kwa wahusika. Njia za matumizi ya vyombo vya habari na ruwaza za kukutana kwa walengwa huundwa na wataalamu. Uwezo wa luninga, redio, na vyombo vingine vya habari wa kuwafikia walengwa wote hutazamwa. Kisha makadirio hufanywa kuhusiana na gharama na umadhubuti wa njia tofauti, na mwisho mchanganyiko wa njia huteuliwa ili kuinua ufanisi wa gharama.

Wakati wa kupanga mkakati wa mawasiliano na kutenga bajeti kwa ajili ya njia mbalimbali za mawasiliano, ni muhimu kuhakikisha kuwa njia zote zinapeleka ujumbe wa uhamasishaji wa aina moja na vifaa kama vinavyotumika katika njia za vyombo vya habari kwa umma. Hivyo basi, kabla ya kuandaa mkutano wa moja kwa moja na watuamijaji pamoja na programu ya ngazi ya Wilaya, ni muhimu kuhakikisha kuwa ujumbe wa vyombo vya habari kwa umma unakamilishwa.

Hata hivyo, hii haimaanishi kuwa kampuni hiyohiyo lazima itumike katika kila mkabala wa mawasiliano. Mashirika yanayojishughulisha na matangazo na mikutano ya ana kwa ana na watumiaji itabidi yatumike.

Mwisho, kuna shughuli nyingi zinazoweza kuhamasisha unawaji wa mikono ndani ya nchi. Hata hivyo, kwa kuwa kuna uhaba wa rasilimali na muda, kila shughuli lazima ithibitishwe kwa kigezo cha muda na rasilimali ili mambo haya yasiathiri juhudi nyingine. Mathalani, mashirika mengi madogomadogo yanaweza kuhitaji kushirikishwa, lakini yanaweza kutumia muda mwingi zaidi katika masuala ya kukubaliana kimkakati kuliko faida itakayotokana na ushiriki wao. Mpango wa kimkakati ni muhimu: kwa kila shughuli, mameneja wanapaswa kuamua kiasi cha matarajio yao kwa kuzingatia matokeo ili wajikite zaidi kwenye mikakati ile yenye matarajio makubwa.

Ufuatiliaji na Tathmini

Madhumuni ya ufuatiliaji na tathmini ni kutaka kujua ukubwa na umakini wa programu. Ufuatiliaji husaidia kutambua na

kutatua matatizo wakati wa utekelezaji wa programu. Tathmini ni mchakato wa kupima matokeo wakati na baada ya utekelezaji ili kujua kiasi cha mafanikio kilichofikiwa na programu. Ufuatiliaji na tathmini hujumuisha hatua kubwa tatu: utafiti wa awali, ufuatiliaji endelevu wa shughuli za programu, na utafiti wa baada ya shughuli.

Katika kiwanda, ni jambo la kawaida kuendesha programu ya mawasiliano katika awamu za miezi sita sita, huku kukiwa na pengo la miezi mitatu mitatu kila baada ya awamu moja ili kupitia upya na kushughulikia maudhui. Jambo hili huwezesha tathmini ya mawanda ya ujumbe, yaliyomo kwenye ujumbe pamoja na jinsi walengwa wa ujumbe walivyopokea na kuutafakari. Vyombo mseto vya habari hupitiwa upya ili kuviwezesha kuwafikia walengwa wengi zaidi, kutafakari njia zinazowafikia watu, pamoja na kubaini njia zinazoaminiwa zaidi na walengwa. Tathmini ya muda inaweza kupima kiasi cha ujumbe unaopokelewa na kutoa taarifa kwa ajili ya marekebisho madogo au makubwa iwapo yatahitajika. Hata hivyo, katika hatua za mwanzo, isitarajiwe kwamba kutakuwa na mabadiliko makubwa ya tabia na ni lazima kutegemea upimaji wa namna watu wanavyoelewa na kukubali ujumbe mbalimbali pamoja na viashiria vya dalili za mabadiliko ya tabia.

Utafiti wa Msingi

Awali kabisa, timu inahitaji kufahamu desturi za wenyeji kuhusu unawaji mikono pamoja na sababu zinazowafanya wanawe kwa sabuni. Utafiti mmoja wa msingi, ambao unaweza kufanywa pamoja na utafiti wa walengwa, unaweza kusaidia timu anzishi katika kuandaa mipango. Makampuni ya kuuza bidhaa yana tabia ya kuchagua jamii inayofaa kwa ajili ya kuifanyia uchunguzi wa mitazamo na vichocheo vya kutumia bidhaa. Hata hivyo, utafiti wa msingi kwa ajili ya kutathmini matokeo ya programu, huhitaji sampuli ya walengwa iliyochoaguliwa kwa makini. Kuwa na timu ya pamoja au iliyo na ushirikiano wa karibu sana ya watu wanaofanya tathmini ya msingi na wale wanaotafiti sababu za unawaji mikono hupunguza gharama, kwa kuwa wataweza kuteua na kufanya kazi na sampuli ileile ya walengwa. Zaidi ya hayo, matokeo yao yatakuwa na nguvu zaidi kimaielezo, kwa sababu uelewa mzuri wa misukumo ya watu unaweza kuhusishwa moja kwa moja na tabia zao za unawaji mikono.

Utafiti wa msingi kuhusu unawaji mikono unapaswa kufanywa miongoni mwa sampuli mchanganyiko ya watu ambao ni walengwa wa programu ya kuhamasisha unawaji mikono. Hivyo basi, pale ambapo utafiti wa msingi unapoanzishwa, timu ya kuhamasisha unawaji mikono inapaswa ifahamu vyema kuhusu walengwa wa kampeni. Mathalani, je, kampeni ni ya kitaifa inayolenga kujumuisha kaya zote au inalenga tu mijini, vijijini, au kaya za kipato cha chini? Baada ya kubainisha walengwa wa kampeni, mkakati unaandaliwa ili kuteua sampuli mchanganyiko ya watu miongoni mwa walengwa. Sampuli ya makundi mchanganyiko sawa na ile inayotumika katika majaribio ya utafiti wa chanjo, ambapo jumuiya huchaguliwa

kimchanganyiko kwa makisio ya kupata sampuli zinazowakilisha walengwa wote, kwa ujumla ni mkabala madhubuti na unaotekelezeka. Timu ya utafiti hutembelea jamii thelathini zinazochaguliwa kimchanganyiko na hutathmini kaya kumi hadi thelathini katika kila jamii moja.

Viashiria vya awali vya utafiti wa msingi hujumuisha:

- **Kuwepo kwa sabuni** katika nyumba husika, kuwepo kwa sabuni ya kunawia mikono katika nyumba husika;
- **Kuwepo kwa sehemu ya kunawia mikono** (yaani mahali ambapo maji na sabuni huwepo kila wakati kwa ajili ya kunawia mikono);
- Orodha ya kumbukumbu ya matukio yaliyoshuhudiwa ya **unawaji mikono katika nyakati muhimu**, hususani taarifa za wanafamilia wanaonawa mikono yao kwa sabuni kabla ya kuandaa, kula, au kugawa chakula; baada ya kwenda haja kubwa; na baada ya kutawadha mtoto aliyepata haja kubwa; na
- **Utokeaji wa ugonjwa wa kuhara** miongoni mwa kila mwanafamilia katika saa 24 zilizopita, ambayo itabidi yapimwe katika nchi ambapo wadau muhimu hawashawishiki kuwa kuna uhusiano baina ya afya na unawaji mikono au wanaotaka upimaji wa moja kwa moja wa athari za kiafya.

Ufuatiliaji

Kitu cha pili kinachohitajika katika kutathmini programu ya kuhamasisha unawaji mikono ni mchakato endelevu wa

kufuatilia utekelezaji wa shughuli zilizopangiliwa na kuhakikisha kuwa ujumbe unawafikia walengwa.

Taarifa zilizotokana na mfumo mzuri wa ufuatiliaji zinaweza kusaidia katika kuelekeza upya programu na kuzifanya ziwe madhubuti. Kama ilivyo kwa programu kubwa yoyote, mameneja wanahitaji kuweka mifumo ya kufuatilia maendeleo ya shughuli za programu na kukusanya data za matokeo. Taarifa hizo zinaweza kujaziwa na utafiti wa muda maalum ili kutambua upeo wa programu kupitia njia mbalimbali za mawasiliano. Kimsingi, utafiti mdogo, unaowakilisha walengwa huonesha jinsi kila mhusika alivyoshiriki katika programu. Walengwa hutoa taarifa ya kumbukumbu zao za mawasiliano na yaliyomo kwenye mawasiliano hayo na huonesha iwapo hali hiyo imesababisha mabadiliko yoyote ya mitazamo au tabia. (Kama ilivyoelezwa, hii haithibitishi mabadiliko ya tabia, lakini ni kiashiria cha jumla cha maendeleo katika mwelekeo sahihi.) Kazi ya kubaini ubora kuhusu namna walengwa wanavyopokea habari kutoka kwenye chombo cha habari inaweza kutoa mwongozo mzuri wa namna ya kupanga upya programu.

Tathmini

Tathmini ya mwisho hulinganisha tabia za kunawa mikono na utafiti msingi ili kujua matokeo na athari za programu. Wakati wa tathmini, sampuli mchanganyiko mpya huteuliwa kutokana na walengwa husika. Jamii mpya thelathini hubainishwa, na kaya kumi hadi thelathini hufikiwa katika kila jamii iliyobainishwa. Zana ileile iliyotumika katika kukusanya data

Jedwali na. 8: Harakati za Kitaifa za Unawaji Mikono Ghana: Matokeo ya Tathmini ya Awamu ya I (Katika asilimia)


Wanawake

Kunawa mikono sabuni	Kuripoti Kunawa Mikono kabla ya Kampeni	Kuripoti Kunawa Mikono tangu kuanza Kampeni	Madadiliko kwa katika Kuripoti
Baada ya haja kubwa	76	89	+13
Kabla ya kula	14	55	+41
Kabla ya kulisha mtoto	6	25	+19
Kabla ya kuandaa chakula	11	26	+15
Baada ya kula	53	31	-22

Watoto

Baada ya haja kubwa	76	89	+13
Kabla kula	14	76	+62
Baada ya kula	61	41	-20

Kielelezo na. 6: Ufuatiliaji na Tathmini: Kazi na Matokeo ya Programu




kwenye utafiti wa msingi hutumika kukusanya data baada ya utekelezaji wa programu. Uchunguzi wa kina wa sababu za tabia ya kunawa mikono haupaswi kurudiwa. Data kutoka katika utafiti wa mwisho huchambuliwa na kulinganishwa na zile za utafiti wa kwanza ili kupima mabadiliko ya tabia (tazama jedwali na. 8).

Tathmini ya kina ya programu, ikijumuisha matokeo ya mwisho, athari za kiafya, ni ghali kuitekeleza vizuri na huhitaji utaalamu maalumu wa magonjwa ya mlipuko. Kuenea kwa ugonjwa wa kuhara hutofautiana sana, hivyo vipimo viwili kwa siku moja katika miaka miwili tofauti kwa walengwa wa

aina mbili wenye kaya 300-900 hakitoshi kuonesha athari za moja kwa moja zinazoweza kuhusishwa na programu za uhamasishaji wa unawaji mikono. Hata hivyo, data hizi zinaweza kutumika katika kupata picha ya ueneaji wa ugonjwa wa kuhara na uhusiano wake na tabia za kunawa mikono zilizoshuhudiwa. Hali hii huweza kutumika kupata picha ya athari za uimarikaji wa unawaji mikono katika ugonjwa wa kuhara. Hata hivyo, kwakuwa athari inayotokana na uimarikaji wa tabia za kunawa mikono kwa magonjwa inajulikana, kwa kawaida inatosha kuchunguza athari za kitabia kama ushahidi kuwa programu inafanikisha malengo yake. Hatimaye, athari za kiafya zitaweza kutabiriwa.





SEHEMU YA 4
Muundo wa Programu

SEHEMU YA 4

Muundo wa Programu

Ushirika Mseto

Kuweka pamoja timu ya taifa yenye nia thabiti, rasilimali, na stadi za kubuni na kuendesha programu ya unawaji mikono huhitaji muda na juhudi. Washirika wenye historia tofauti wasipozoeshwa kufanya kazi pamoja, huchukua muda kuweka malenga ya pamoja na kujenga hali ya kuaminiana.

Ushirikiano baina ya sekta binafsi na sekta ya umma huweka mfano madhubuti kwa ajili ya programu za unawaji mikono kwa sababu huunganisha pamoja malengo ya kiafya ya sekta ya umma na utaalamu wa masoko wa sekta binafsi. Kama ilivyodokezwa, sekta binafsi hutarajia kunufaika kutokana na kujiunga na ushirika huo hasa kupitia upanuzi wa masoko, kwa kuonekana kama ni mchango kwa malengo ya kijamii, na kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo na wataalamu wa kimataifa. Sekta ya umma hufaidika kutokana na utaalamu wa masoko na rasilimali za viwanda. Hivyo, huweza kuanzisha kampeni za afya ya jamii ambazo ni shindani, au bora zaidi kuliko juhudi za utafutaji masoko iviwandani.



Mfano wa Ushirika wa Jumla

Uzoefu uliopatikana katika kampeni zilizopita za kunawa mikono huko Amerika ya Kati, Ghana, Nepali, na Senegali unaonesha kuwa mfano wa kamati-ratibu kwa ajili ya Ushirikiano baina ya sekta binafsi na sekta ya umma ni njia madhubuti ya kusimamia programu yenye makundi tofautitofauti ya washirika.

Mratibu: Mratibu husimamia shughuli za kila siku, huwashirikisha na kuwataarifu wadau na huhakikisha kuwa juhudi zote zinafanyika kwa shabaha ya kufikia malengo. Mratibu anawajibika na kuandaa na kukamilisha mpango wa kazi wa mradi kwa njia ya kuwashirikisha washirika na rasilimali. Mfano wa Hadidu za Rejea (HaRe), uliopo katika kiambatisho, unabainisha kazi, sifa na stadi za mratibu.

Kamati elekezi: Wadau muhimu wanaotoa rasilimali—msaada wa kiufundi, fedha, na uongozi—huunda kamati elekezi. Wajumbe wa kamati hii, kila mara, huwasiliana miongoni mwao pamoja na mratibu na kuongoza vipengele maalumu vya mpango wa kazi. Faida ya kuwa na wajumbe wengi lazima ipimwe ikilinganishwa na gharama za uendeshaji, ambazo hupanda sana kulingana na kila ongezeko la mjumbe.

Kamati ya ushauri: Kamati ya ushauri huundwa na wadau wenye maslahi mahususi katika mradi lakini ambao hawatarajii kushirikishwa katika kazi za kila siku za programu. Wajumbe wake wanaweza kuombwa kutoa tathmini ya muda fulani na kuridhia baadhi ya mambo. Kamati hii huweza kujumuisha watumishi wa serikali, wanahabari, jumuiya za kijamii, jamii pana ya wanasayansi, na mameneja waandamizi wa asasi. Wanaweza pia kuwa wawakilishi wa mashirika, mathalani, mashirika ya kikanda au asasi zisizo za serikali ambazo zitaeneza kampeni katika maeneo mahususi ya kijiografia.

Ikikutana katika vikao rasmi au visivyo rasmi, kamati ya ushauri humsaidia mratibu kupanga wadau katika kiwango kinachofaa cha ushirikiano na kusaidia kuwaweka pamoja na kuwaongezea shauku. Makundi madogomadogo katika mawasiliano, utafiti wa walengwa, na vyombo vya habari huweza kufaa.

Mpango wa Kazi

Kuandaa ushirika wa unawaji mikono ni mchakato unaojirudiarudia na, kwa kiasi kikubwa, ni wa kiujasiriamali. Wakati ambapo mwelekeo wa jumla unaweza kubainishwa mapema, malengo huwa na maelezo ya kina zaidi na kazi za utekelezaji huimarika kadiri mradi unavyopiga hatua. Kuuweka mchakato huu pamoja ndio mpango wa kazi (sanduku na 13),

Kisanduku na. I I: Utekelezaji wa Unawaji Mikono: Ushirika wa Unawaji Mikono Huko Peru

Kubainisha washirika sahihi, kujenga uhusiano wa kuaminiana, kisha kudumisha ushiriki na ridhaa ya kukubaliana kwa kiwango cha juu, bila shaka ni mambo magumu na yanayokatisha tamaa, na wakati huohuo ni majukumu muhimu ambayo mratibu lazima ayatimize na kuyadumisha wakati wa juhudi husika. Ushirika wa sekta ya umma na ya binafsi unapoaminika kuwa imara, mratibu asibweteke kwa mafanikio hayo, kwa sababu wakati wote kuna hatari ya kuweza kuzuka matatizo, yakaathiri au kuharibu maelewano imara yaliyopo miongoni mwa wadau.

Juhudi za Peru zilianzia mahali pazuri. Dira ilipanda mbegu, na miezi michache baadaye, Wizara ya Afya, Shirika la Maendeleo la Uswisi, Programu ya Maji na Usafi ya Benki ya Dunia, na Shirika la Misaada la Marekani ziliunganisha kamati ya uwezesaji ya unawaji mikono pamoja na ajenda zilizofafanuliwa vyema kwa ajili ya mwaka mmoja wa utekelezaji.

Vikao vya kamati ya uwezesaji vilifanyika mara kwa mara, na ujenzi wa ushirika madhubuti ulikuwa ni kipaumbele cha kwanza. Karibu mashirika 20 yalibainishwa na kutembelewa kukiwa na malengo mawili: kutoa habari kuhusu unawaji mikono kwa njia ya hotuba za ushawishi na uhamasishaji na kukusanya taarifa za tabia ya ushirika tarajali: wasifu wake; malengo yake ya kitaasisi; manufaa atakayoleta katika ushirika; na umuhimu wake katika utoaji wa ushauri wa kitaalamu na uwezo wake wa kushawishi, kwa ajili ya kuvutia washiriki wapya, na kwa ajili ya kuwa mshiriki wa kifedha katika nyakati fulani.

Wajumbe wa kamati ya uwezesaji nchini Peru hushiriki katika warsha za kimataifa za kiufundi

Mwaka wa kwanza: Kamati ya uwezesaji ilijigeuza kuwa kamati madhubuti ya utendaji, huku wajumbe wapya wakijiunga kutoka katika sekta binafsi: Vipindi vya Redio Peru, shirika la utangazaji la taifa linalojihusisha na majukumu ya kijamii, na shirika la

kimataifa lisilo la kiserikali la CARE lenye uzoefu katika uhamasishaji wa unawaji mikono katika maeneo ya vijijini. Wataalamu wake walishiriki na walifuatilia kwa karibu mchakato wa upangaji wa shughuli zilizoishia katika mpango wa kazi mwishoni mwa mwaka wa kwanza.

Washirika wengine binafsi kama vile *Colgate Palmolive* na *Alicorp* (kampuni ya taifa inayoongoza katika uzalishaji wa sabuni za kufulia), wajumbe wa jumuiya kubwa, na kamati ya ushauri walikuwa muhimu katika kikosikazi cha mawasiliano, kilichoandaa muundo wa programu ya mawasiliano ya mpango wa kazi.

Kupunguza kasi: Kuanza kwa awamu ya utekelezaji kuligubikwa na hali ya wasiwasi. Vyanzo vya mapato vilivyokuwa vimebainishwa kuwa ni madhubuti vilitetereka, jambo lililosababisha juhudi kwenda polepole na kasi ikapotea.

Mabadiliko yalitokea karibu katika kila taasisi mwanachama wa kamati ya utendaji. Kazi za washirika hazikueleweka vema kwa wanachama wapya: Je, juhudi zifanywe kuwa za umma? Je, ni majukumu yapi wajumbe wa kamati ya utendaji wanapaswa kuwa nayo mara baada ya fedha kupokelewa?

Dirisha la fursa lilifunguliwa pale Shirika la Misaada la Marekani lilipoamua kugharimia shughuli ya kwanza ya awamu ya utekelezaji: mchakato wa ubunifu, ulioleta fursa ya uundaji mpya wa kamati ya utendaji kwa kuzingatia mpango wa kazi bayana. Ilibidi mchakato uanze tena.

Uwezo wa kuwasiliana, na ujenzi wa imani miongoni mwa asasi tofauti; uwezo wa kuhamasisha ushiriki na utashi wa washiriki; uimarishaji wa haki zao za umiliki wa shughuli zao; kujua wakati wa kuchachamaa na wakati wa kusimama; kutabiri mabadiliko na uwezo wa kugundua fursa na kudhibiti hatari wakati zinapojitokeza; yote haya ni nyenzo muhimu kwa mratibu.

Kisanduku na 12: Shughuli za Sekta Binafsi za Unawaji Mikono

Sekta binafsi duniani kote huhusisha na uhamasishaji wa unawaji mikono na shughuli za utoaji wa elimu ambazo zinaweza kuhusisha na kuratibu miradi ya unawaji mikono katika nchi husika ili kupanua mawanda ya programu na kusaidia kuhakikisha uendeleu wa programu kwa kuweka ujumbe wa unawaji mikono katika aina mpya za sabuni zinazongezeka. Dondoo zifuatazo kutoka katika nyenzo za uhamasishaji za kampuni kubwa tatu za uzalishaji wa sabuni zinabainisha mikabala ya sekta binafsi kuhusiana na suala zima la shughuli za unawaji mikono.

Colgate-Palmolive: Mikono Safi, Afya Njema

Dondoo za afya zilielezea unawaji mikono kuwa ni zana muhimu sana katika kulinda afya ya jamii. Ni tegemeo kubwa katika udhibiti wa maambukizi. Cha kushangaza, uhamasishaji wa unawaji mikono kwa umma kwa kawaida umekuwa hauonekani. Utafiti wa tabia za umma unaonesha pengo kati ya utendaji na inavyochukuliwa kuwa. Huu ni ukweli bayana katika nchi zilizoendelea na zinazoendelea pia. Ili kushughulikia mahitaji ya uhamasishaji wa elimu ya unawaji mikono, kampuni ya *Colgate-Palmolive* ilianzisha mradi wa elimu kwa dunia nzima uliojulikana kama Mikono Safi, Afya Njema. Mradi ulianza mnamo mwaka 1998 kwa kampeni ya mabango yaliyoandikwa Boresha ngozi kwa Afya Njema, iliyoandaliwa maalum kuhamasisha na kuinua mwamko wa watu kuhusu unawaji mikono kupitia njia ya kuwafikia wataalamu wa afya ya jamii wa Marekani na jamii kwa ujumla.

Mnamo mwaka 2000 programu hii ilipanuliwa kwa kuanzishwa programu ya elimu mashuleni iliyoandaliwa maalumu kuwasaidia waelimishaji katika kuwafundisha watoto wenye umri wa kwenda shule kwa njia ya kuwashirikisha zaidi. Tangu programu hii izinduliwe Marekani, imeweza kuwafikia mamilioni ya watoto nchini Marekani, barani Asia, Amerika ya Kusini na Afrika.

Programu hii inajumuisha mtalaa wa shule na programu za jumuiya. Watoto, wazazi, waelimishaji, na wataalamu wa afya wanafanya kazi pamoja ili kufanya unawaji mikono kuwa kipengele muhimu cha elimu ya usafi na desturi za watu. Tafiti zinaonesha kuwa, watoto wadogo waliozoeshwa kwenye mtalaa huu wanaweza kuelewa kwa urahisi jinsi ya kunawa na sababu za kunawa, na kuufanya mtalaa huu kuwa rafiki mkuu katika ufundishaji wa ulinzi binafsi.

Procter & Gamble: Program ya Unawaji Mikono nchini Meksiko

Kampuni ya sabuni ya mche ya *Safeguard* ya nchini Meksiko imekuwa ikiendesha kampeni ya vipengele vingi kuhamasisha unawaji mikono miongoni mwa watoto. Unawaji mikono umeonekana kuwa na matokeo madhubuti katika kupunguza magonjwa ya kuhara na yale ya kuambukiza. Programu inafanya kazi kama ushirika, *Safeguard* ikitoa utaalumu na vifaa, wakati ikiacha jukumu la kuwafikishia watu habari kwa washirika wake wa vyombo vya habari, asasi za kiserikali, na elimu. Mtangazaji maarufu kitaifa Lolita Ayala, ambaye ana shirika la watoto waishio katika mazingira magumu, anaunga mkono kampeni nzima.

Safeguard huchangia sehemu ya mauzo yake kwenye Mfuko wa *Solo por Ayudar*.

Kampeni huwatumia washirika wafuatao:

- Shirika la Hifadhi ya Jamii la Meksiko, ambalo hutumia miundombinu yake kusambaza vifaa vinavyohusu unawaji mikono. Lengo la sehemu hii ni kuwafikia wakazi wa vijijini zaidi ya milioni mbili katika kipindi cha miezi 12 ya mwanzo. *Safeguard* ikifikia malengo haya ikiwa na matokeo mazuri, inapanga kupanua programu hadi kufikia watu milioni 11.
- Zaidi ya vituo vya redio 2000 vya Meksiko, ambavyo vimekuwa vikisambaza habari kuhusu unawaji mikono.
- Makumbusho ya Watoto ya Jiji la Meksiko yamekuwa yakionesha mchezo wa kompyuta kuhusu bakteria, mchezo ambao watoto huweza kuutumia katika kituo chake kikuu au katika maonesho ya kutembeza.
- Maonesho ya vikaragosi yanayohamasisha usafi kwa watu zaidi ya asilimia 80 ya darasa la kwanza katika majiji matatu, hali kadhalika katika eneo maarufu la maduka ya Merida.

Unilever: Lifebuoy Swasthya Chetna (Kuamsha watu kuhusu Afya Zao)

Programu hii ilibuniwa kutokana na mienendo binafsi ya usafi kama vile kutumia sabuni kila siku kunawia mikono, hali kadhalika kuogea huko India. Ilikuwa ni kampeni ya awamu nyingi na iligusa kila mwanajumuiya—watoto, wazazi, wahamasishaji, na kinamama wazazi waliotoka

Ushirika wa Lifebuoy



kujifungua—katika kila maeneo yote ya makutano, yenye vyombo vyovyote vya habari.

Programu hutumia zana ya kibunifu, 'Glow Germ demo' kuondoa imani potofu, 'Usafi unaoonekana ni usafi salama' na kuonesha kuwa 'Maji hayatoshi'. Mbali na hayo, hadithi, maigizo mafupi ya kuchekesha, chemshabongo, mikutano ya hadhara, makambi ya

kupimia afya, mabango, na majarida yalitumika kutolea ujumbe. Sasa kampeni hii iko katika mwaka wake wa tatu, na mwitikio wake umekuwa wa kutia moyo. Wanakijiji huizungumzia sana na huichukulia kama kampeni yao. *Lifebuoy Swasthya Chetna* kwa sasa inavifikia vijiji karibu 18,000 katika majimbo manane, ikilenga kuwafikia watu milioni 100 kufikia mwishoni mwa mwaka 2005.

ambao huwapatia wadau uhalali wa kuchangia na huwajulisha mahali ambako ugharamiaji unahitajika.

Mpango wa kazi hubadilika kulingana na juhudi. Kadiri ushirika unavyozidi kukua, mpango wa kazi utawasaidia washiriki kuimarisha mawazo na kufikia mwafaka. Rasimu ya kwanza huonyesha dira ya ushirika. Matoleo yanayofuata yataakisi ushiriki wa washirika wapa na ukamilishaji wa vipengele,

kama vile utafiti wa walengwa na mbinu za mawasiliano. Kwa kawaida mipango ya kazi huwa haizidi kurasa 15, ikijumlisha ukurasa au kurasa mbili za muhtasari maalum kwa waandamizi. Washirika wanaopenda huweza kualikwa kupitia upya nyaraka zenye maelezo ya kina zaidi, kama vile matokeo ya utafiti wa walengwa au mkakati wa mawasiliano. Mpango wa kazi lazima usawidiwe katika muundo rahisi, unaovutia na unaoweza kusambazwa kirahisi.

Kisanduku na. 13: Vipengele vya Mpango wa Kazi

Muhtasari huu unatoa hatua ya kuanzia kwa ajili ya mpango wa kazi unaodhihirisha na kuhamasisha programu ya unawaji mikono.

Muhtasari maalum kwa waandamizi: Muhtasari wa ukurasa hadi kurasa mbili wa mpango wa kazi, kwa kawaida huandikwa mwishoni.

Dira, dhamiri, na muhtasari wa yatakayofanyika: Maandiko haya mafupi hujibu maswali kama vile: Nini yatakuwa matokeo ya mradi? Mradi utatimiza malengo gani? Washirika wa mradi ni nani?

Muhtasari wa Sekta: Andiko hili linatoa muhtasari wa mlolongo wa mwenendo uliopo na wa baadaye katika nchi, ambao unaweza kutumiwa katika kampeni ya unawaji mikono: Malengo ya Maendeleo ya Milenia na Mikakati ya Kupunguza Umaskini—afya na vifo vya watoto, n.k.—huonesha idadi na mielelekeo. Je, hili ni eneo linalopanuka? Pia huelezea kuhusu soko la sabuni la nchi: Wahusika ni nani kimapato na kimauzo? Mielelekeo ni ipi?

Uchambuzi wa mzigo wa afya na gharama za ugonjwa.

Unawaji mikono kwa sabuni utaleta manufaa gani: Andiko hili ni muhtasari wa uthibitisho wa kisayansi kuhusu umuhimu wa unawaji mikono kwa sabuni, uwezekano wake, na umadhubuti wake. Linaashiria matokeo ya kiafya na kiuchumi yanayoweza kupatikana kutokana na ushirikiano.

Unawaji mikono katika nchi X hutoa matokeo ya utafiti wa walengwa na muhtasari wa mabadiliko ya tabia yanayotakiwa.

Mkakati wa mawasiliano hutoa muhtasari wa mkakati wa mawasiliano, ukiweka malengo sahihi yanayopimika, mathalani: “Kuinua maradufu kiwango cha unawaji mikono kwa sabuni miongoni mwa kinamama wenye watoto wa umri wa chini ya miaka mitano baada ya kutoka chooni au kutawadha watoto” au “Asilimia hamsini ya kinamama waliojifungua nchini watapokea mche mmoja wa sabuni na maelekezo juu ya umuhimu wa unawaji mikono.” Hubainisha mikakati, mikabala, na misingi mikuu ya mpango wa mawasiliano.

Kampeni ya mawasiliano hupambanua vyombo vya habari, mawasiliano ya moja kwa moja na walengwa, programu za serikali, uhusiano wa umma, na vipengele vingine vyovyote.

Ufuatiliaji na tathmini huelezea Mikakati ya Ufuatiliaji na Tathmini: aina gani za data zitakusanywa, kivipi, na lini?

Muundo wa uongozi wa Ushirika baina ya Sekta ya Umma na ya Binafsi: Ni kumbukumbu ya kamati zilizopo na zinazohitajika na majukumu yake, nani ataratibu na zipi zitakuwa ni kazi za uratibu, na uthibitishaji wa uteuzi wa washiriki.

Muda na mambo makuu huonesha kiasi cha fedha kitakachohitajika kugharamia mambo yatakayokamilishwa katika tarehe zilizopangwa. Hali ya kifedha na mahitaji ya gharama huonesha gharama za uendeshaji kwa kila sehemu na kazi, na hujumuisha vyanzo vya fedha. Aidha, huonesha msaada uliopatikana na unaohitajika.

Kipengele	Maelezo	Muda	Gharama Zilizokadiriwa au 'Kwa namna Nyingine' kama Msaada umepatikana na Kiasi	Chanzo cha Fedha (Kama kimepatikana)
1. Tathmini ya hali na makubaliano ya awali				
2. Uanzishwaji wa Programu				
3. Utafiti wa Walengwa				
4. Uandaaji wa Mkakati				
5. Uandaaji wa vifaa na ujaribizi				
6. Utekelzaji wa kampeni				
7. Ufuatiliaji na tathmini				



Hitimisho

Hitimisho

Kijitabu hiki kinatoa muhtasari wa mkabala wa uhamasishaji wa unawaji mikono kwa kutumia sabuni, mkabala ambao utaendelea kukua.

Masuala mengi bado yanahitaji kufanyiwa kazi. Matalani, juhudi zaidi zinahitajika kuonesha unafuu wake kigharama. Aidha, ujenzi wa ushirika baina ya sekta ya umma na ya binafsi unaweza kuwa wa polepole na hata matokeo yake yakapatikana polepole zaidi. Hali hii haishangazi, kwa kuwa mawasiliano huwa magumu hasa yanapohusisha makundi yenye tamaduni, njia za kufanya mambo na madhumuni tofauti. Hali kadhalika, ubadilishaji wa watumishi mara nyingi huhitaji kurudiwarudiwa kwa ujenzi wa uhusiano, kama mfano wa Peru unavyoonesha. Hata hivyo, kadiri programu za unawaji mikono kwa sabuni zinavyodhihirisha ufanisi wake, na kumbukumbu za uzoefu zinavyotumiwa, kasi na ufanisi vitaongezeka na kuhamasisha ushirika hakutakuwa kazi ngumu.

Jambo lingine muhimu ambalo ushirika baina ya sekta ya umma na ya binafsi unakabiliana nalo ni ukweli kwamba usafi si swala la kushughulikiwa na asasi moja. Katika programu nyingi, kama

vile Ghana, fedha hutoka katika sekta ya maji na usafi. Hata hivyo, ili unawaji mikono ukubalike na udumishwe kwa mapana, programu hizo zinahitaji pia kuwa sehemu ya shughuli za Wizara za Afya na Elimu.

Ushahidi wa kutosha kuhusiana na umuhimu wa unawaji mikono kwa afya ya jamii pia utasaidia kuinua ridhaa ya jamii. Hasahasa, majaribio ya uhakika kuhusu athari za unawaji mikono katika magonjwa ya kuambukiza hayana budi kufanyika. Bado kuna ushahidi dhaifu kuhusu athari zake katika maambukizi makali ya mfumo wa upumuaji, hivyo panahitajika utafiti zaidi. Aidha utafiti zaidi katika ulinganishaji wa umadhubuti wa mikabala mbalimbali katika kuwezesha mabadiliko ya tabia utasaidia kurahisisha utekelezaji.

Ushahidi uliopo unatosha kuwezesha sekta ya afya ya jamii kushughulikia masuala ambayo, kwa kutazama uwezekano wake, yanaonesha matumaini makubwa. Kwa mtazamo huu, kueneza unawaji mikono kwa sabuni kila mahali ni changamoto kubwa kwa sekta ya afya ya jamii katika karne hii ya 21. Serikali, viwanda, mashirika ya misaada, na asasi za kitaalamu zote kwa pamoja zina jukumu la kutekeleza.





**Marejeo
na Vyanzo**

Marejeo na Vyanzo

- Burros A., D. Ross, W. Fonscea, L. Williams, na D. Moreira-Filho. 1999.** Preventing acute respiratory infections and diarrhoea in child day care centres. *Acta Paediatrica* 88 (10): 1113-18.
- Bateman, M., Bendehmane, D., na Saade, C. 2001.** *The Story of a Successful Public-Private Partnership in Central America, Handwashing for Diarrheal Disease Prevention.* Arlington, VA.: BASICS II, UNICEF, Benki ya Dunia na EHP OHIDN/BGH/USAID. www.ehproject.org.
- Bateman M., Jahan R., Brahman S., Zeitlyn S., na Laston S. Joint Publication 4: Prevention of Diarrhea through Improving Hygiene Behaviors: The Sanitation and Family Education (SAFE) Pilot Project Experience.** CARE, ICDDR, B na EHP (OHIDN/BGH/USAID). Kilichapwa tena mwaka 2002. www.ehproject.org.
- Biran, A. 1999.** What form could a DFID-funded Hygiene Promotion Programme Take in Order to Support and Help Ensure Maximum Health Benefits from Proposed Improvements to Water Supply Systems in Northern Kyrgyzstan? Tasnifu ya Uzamili (Sayansi) kwa ajili ya LSHTM.
- Buchholz na Wordemann. 2001.** *What Makes Winning Brands Different: The Hidden Method behind the World's Most Successful Brands.* Wiley & Sons, Chichester.
- Cairncross, S. na Shordt, K.** "It Does Last! Some Findings from the Multi-City Study of Hygiene Sustainability." *Waterlines* 22 (3): 4-7.
- Cercone, James A. na wenzake. 2004.** Handwashing as a cost-effective approach to improving health: A framework for the economic analysis of handwashing projects: Case study of Central America and Peru.
- Curtis V., B. Kanki, S. Cousens na wenzake. 2001.** Evidence for behaviour change following a hygiene promotion programme in West Africa. *Jarida la Shirika la Afya Duniani* 79 (6): 518-26.
- Curtis V., A. Biran, Deverell K., C. Hughes, K. Bellamy, na B. Drasar. 2003.** Hygiene in the home: Relating bugs and behaviour. *Sayansi ya Jamii na Dawa* 57 (4): 657-72.
- Curtis V. na Cairncross. 2003.** Water, Sanitation & Hygiene at Kyoto. *Jarida la Uingereza la Utabibu* 327: 3-4.
- Curtis V. na Cairncross. 2003.** Effect of washing hands with soap on diarrhoea risk in the community: a systematic review. *The Lancet Infectious Diseases* 2003; 3: 275-81.
- Delafield, S. 2004.** Activity Report 128: *Planning Tools for the Nepal Public-Private Partnership for Handwashing Initiative.* Mradi wa Afya ya Mazingira OHIDN/BGH/USAID. www.ehproject.org.
- EHP. 2004.** Strategic Report 8: *Assessing Hygiene Improvement: Guidelines for Household and Community Levels.* Mradi wa Afya ya Mazingira OHIDN/BGH/USAID, 2004. www.ehproject.org.
- EHP, UNICEF, WB/WSP, WSSCC, na USAID. 2004.** Joint Publication 8: *The Hygiene Improvement Framework: A Comprehensive Approach to Preventing Childhood Diarrhea.* Washington, D.C.: UNICEF, WB/WSP, WSSCC, na EHP OHIDN/BGH/USAID. www.ehproject.org.
- EHP, UNICEF, WSSCC na USAID. 2004.** Joint Publication 13 (Adapted from EHP Joint Publication 8): *Preventing Childhood Diarrhea Through Hygiene Improvement.* Washington, D.C.: EHP OHIDN/BGH/ USAID. www.ehproject.org.
- EHP. Behavior Change Lessons Learned.** Washington, D.C.: EHP Office of Health, Infectious Diseases and Nutrition, Bureau for Global Health, U.S. Wakala wa Maendeleo ya Kimataifa (OHIDN/BGH/USAID), 1999. www.ehproject.org.
- Esrey S.A., J.B. Potash, L. Roberts, na C. Shiff. 1991.** Effects of improved water supply and sanitation on ascariasis, diarrhoea, dracunculiasis, hookworm infection, schistosomiasis, and trachoma. *Jarida la Shirika la Afya Duniani* 69 (5): 609-21.
- Favin, M. 2004.** Activity Report 143: *Promoting Hygiene Behavior Change within C-IMCI: The Peru and Nicaragua Experience.* Washington, D.C.: Mradi wa Afya ya Mazingira OHIDN/BGH/USAID. www.ehproject.org.
- Favin M., Naimoli G., na Sherburne L. 2004.** Joint Publication 7: *Improving Health Through Behavior Change: A Process Guide on Hygiene Promotion.* Washington, D.C.: PAHO, PLAN na EHP OHIDN/BGH/USAID. www.ehproject.org.
- Gilman R.H., G.S. Marquis, G. Ventura na wenzake. 1993.** Water cost and availability: Key determinants of family hygiene in a Peruvian shantytown. *Jarida la Marekani la Afya ya Jamii* 83 (1): 1554-58.
- Hoque, B.A. 2003.** Handwashing Practices and Challenges in Bangladesh. *Jarida la Kimataifa la Utafiti wa Afya ya Jamii*, 13 Mswada 1: 81-87.
- Jones, G., Steketee, R.W., Black, R.E., Bhutta, Z.A., Morris, S.S. na the ellagio Child Survival Study Group. 2003.** "How Many Child Deaths Can We Prevent This Year?" *Lancet*, 362: 65-71.
- Kolesor, R., Kleinau, E., Torres, M.P., Gil, C., de la Cruz, V. na Post, M. Combining Hygiene Behavior Change with Water and Sanitation: Monitoring Progress in Hato Mayor, Dominican Republic.** Washington, D.C.: Mradi wa Afya ya Mazingira OHIDN/BGH/USAID, 2003. www.ehproject.org.
- Luby, S.P., M. Agboatwalla, J. Painter, A. Altaf, W.L. Billhimer, na R.M. Hoekstra. 2004.** Effect of intensive handwashing promotion on childhood diarrhea in high-risk communities in Pakistan: A randomized controlled trial. *Journal of the American Medical Association* 291: 2547-54.
- McGahey, C. na Rosensweig, F. 2002.** *Hygiene Improvement Framework.* Washington, D.C.: Water Supply and Sanitation Collaborative Council (WSSCC) and EHP OHIDN/BGH/USAID. www.ehproject.org.
- Omotade, O.O., C.M. Kayode, A.A. Adeyemo, na O. Oladepo. 1995.** Observations on handwashing practices of mothers and environmental conditions in Ona-Ara Local Government Area of Oyo State, Nigeria. *Journal of Diarrhoeal Disease Research* 13 (4): 224-28.
- PRISM na EHP. 2004.** *Joint Publication 11E: Behavioral Study of Handwashing with Soap in Peri-urban and Rural Areas of Peru.* Washington, D.C.: EHP OHIDN/BGH/USAID. www.ehproject.org.
- Rai, R., Khanal, S., na Wicken, P. 2004.** *Hygiene Behavior Can Be Sustained, A Report on the Nepal Country Findings of a Multi-Country Study on Sustaining Changes in Hygiene Behavior.* NEWAH.
- Simpson, Mayling, Sawyer, Ron, na Clarke, Lucy. 1997.** *Participatory Hygiene and Sanitation Transformation (PHAST): A New Approach to Working with Communities.* WHO, EOS/96.11; Kilichapishwa tena mwaka 2002. www.who.org.
- Sircar B.K., P.G. Sengupta, S.K. Mondal na wenzake. 1996.** Effect of handwashing on the incidence of diarrhoea in a Calcutta slum. *Katika Journal of Diarrhoeal Diseases Research* 5 (20): 114.
- UNICEF/WES, USAID, World Bank/WSP, WSSCC. 2004.** Joint Publication 8, *The Hygiene Improvement Framework: A Comprehensive Approach for Preventing Childhood Diarrhea.*
- Wood S., Sawyer R., Simpson-Hebert M. 2002.** *PHAST step-by-step guide: a participatory approach for the control of diarrhoeal disease.* Geneva, World Health Organization (Haujachapishwa WHO/EOS/98.3). www.who.org.
- Zaltman, J. 2003.** *How Customers Think: Essential Insights into the Mind of the Market.* Harvard Business School Press.
- World Bank, EHP, WSP: Handwashing Consumer Research Reports:** Ghana, Peru, Senegal.



**Zana na
Hadidu za Rejea**

Zana na Hadidu za Rejea

Zana ya I: Majaribio ya Tabia na Mahojiano ya Kina

Taarifa na Maelekezo kwa Watafiti wa Uwandani

Majaribio ya Tabia ni Nini?

Jaribio la tabia hutambulisha tabia kwa watu na hupima uzoefu wao katika kujaribu kuizoea tabia hiyo kwa muda wa kati ya siku saba hadi 14. Jaribio hilo husaidia kuoneshaa picha kamili ya maendeleo ya uzoaji wa tabia mpya, mambo yanayochochea au kudhoofisha uzoaji wa tabia hiyo. Kwa hali hii, sabuni hutolewa kwa kila mshiriki ambaye huombwa kutumia sabuni hiyo kwa kunawia mikono TU, hasa baada ya kugusa kinyesi (baada ya haja kubwa, baada ya kutawadha mtoto, na baada ya kutupa kinyesi), na kabla ya kumlisha mtoto. Baada ya kipindi fulani mhoji humtembelea kila mwanamke na kufanya naye mahojiano ya kina ili kujifunza kuhusu uzoefu wake uliopatikana katika kipindi cha kati ya ziara zake mbili.

Mwenendo tunaolenga ni unawaji mikono kwa sabuni, tunataka kujua ni mambo gani yanayowachochea au kuwakwaza wanawake kuzingatia tabia hiyo. Mahususi kabisa, tunazingatia unawaji mikono KWA SABUNI baada ya haja kubwa, baada ya kutawadha mtoto, baada ya kutupa kinyesi cha mtoto, na kabla ya kumlisha mtoto. Wakati wa mahojiano unapaswa kudadisi sababu, mambo yanayopendelewa na

yasiyopendelewa kwa kila tukio tofauti la unawaji mikono, ili kuona iwapo sabuni hutumika na kwa nini. Ni muhimu pia kujifunza kutoka kwa wanawake ambao hawakutumia sabuni walizopewa kama ilivyo kwa wale waliotumia. Mara nyingi watoa taarifa watarejea kwenye maneno yenye vionjo binafsi kama vile usafi na uchafu. Ni muhimu kudadisi watu humaanisha nini kwa maneno hayo na jinsi yanavyooneshwa, hususani kwa kuhakikisha kuwa vidokezo vya fahamu (kugusa, kuona, kunusa, n.k.) vinahusishwa.

Mahojiano baada ya Uzoefu Uliopatikana

- Juma lililopita nilikuachia sabuni na nilikuomba uitumie mahususi kwa kunawia mikono, je, ulitumia?
- OMBA UONESHWE SABUNI, ANGALIA INAONEKANA IMETUMIKA KWA KIASI GANI NA ILIWEKWA WAPI: WEKA KUMBUKUMBU YA HALI YAKE:

SABUNI ILIWEKWA WAPI: _____

- Kabla hatujaanza, naweza kupata taarifa zenu za kijamii

Una umri gani? Chini ya miaka 24 = 1 25-30 = 2 31-35 = 3 36-40 = 4 41 na kuendelea = 5	
Unaishi wapi? Jina la Mahali: _____ Aina ya Mahali: Mjini = 1 Mji Mdogo = 2 Kijijini = 3	
Taja kiwango chako cha juu cha elimu ulichofikia	
Taja kazi yako	
Taja kazi ya mume wako	
Je, mume wako anafanya kazi karibu au mbali na nyumbani? Karibu na nyumbani = 1 Mbali = 2	
Una watoto wangapi? Mmoja = 1 Wawili = 2 Watatu = 3 n.k.	
Wangapi kati yao wana umri chini ya miaka mitano? Mmoja = 1 Wawili = 2 Watatu = 3 n.k. KAMA HAKUNA WATOTO WENYE UMRI CHINI YA MIAKA MITANO SITISHA MAHOJIANO.	

	Mtoto wako mdogo kabisa ana umri gani? 0-6 Miezi = 1 7-12 Miezi = 2 1-2 Mwaka = 3 3-5 Miaka = 4	
	Ulishawahi kuhamia mji mwingine kwenda kufanya kazi katika kipindi cha miezi 12 iliyopita? Ndiyo = 1 Hapana = 2 Mahali: _____	
	Unajisaidia haja kubwa wapi? Choo cha maji = 1 Choo cha tundu = 2 Choo binafsi cha watu maalumu = 3 Choo binafsi cha maji = 4 Choo cha umma = 5 Kichakani = 6 Sehemu Nyingine = 7 _____	
	Watoto wako wanajisaidia haja kubwa wapi? Kwenye chombo cha haja kubwa = 1 Nguoni = 2 Sakafuni = 3 Kama hapo juu = 4	

Sasa fanya mahojiano ukizingatia mada zifuatazo:

Uzoefu wa Jumla wa Sabuni (Kila wakati unawaji mikono unapotajwa, fafania iwapo sabuni ilitumika au la na kwa nini unawaji mikono hufanywa kwa/au bila sabuni)	Kabla ya kupewa sabuni hii, ulitumia sabuni kwa sababu gani na kwa nini? Matukio na sababu za kawaida za unawaji mikono. KAMA WATATAJA UCHAFU AU USAFI, WAULIZE HUMAANISHA NINI NA WANAJUAJE KUWA KITU NI SAFI AU KICHAFU (YAANI UNaweza KUWA MCHAFU HATA KAMA HUWEZI KUUONA, KUUNUSA AU KUUGUSA HUO UCHAFU?). Chanzo cha maji ya kunawia mikono. Kuna uhaba wowote wa maji? Je, uhaba huo wa maji unaathiri mwenendo wa unawaji mikono? Je, sabuni imewahi kutumika kunawia mikono? Kama ndiyo, ni lini na kwa nini? Ni mambo gani huchochea matumizi ya sabuni? Kama haitumiki, kwa nini? Aina ya sabuni: Ya kuogea au ya matumizi mchanganyiko. SABABU. Chanzo cha sabuni na utunzaji. Upatikanaji wa sabuni. Hutokea nini sabuni isipopatikana? Wanawake hujisikiaje sabuni isipopatikana, hukabiliana je na hali hiyo? Faida kuu za matumizi ya sabuni kunawia mikono KWA KILA HATUA. Kutopenda/matatizo makuu yanayohusishwa na unawaji mikono kwa sabuni. Nyakati muhimu sana za kunawia mikono kwa AU bila sabuni. Sababu. Matumizi mengine ya sabuni na sababu zake.
Matumizi ya sabuni	Je, sabuni aliyopewa mwanamke ilitumika? Ilitumikaje na ilitunzwa wapi? (Muombe mwanamke akuoneshe, kama bado hajakuonesha. (Chunguza hali ya sabuni na mahali ilipotunzwa.)
Wasiotumia sabuni/ matumizi madogo	Kwa nini sabuni haikutumiwa? Sababu hizi ni za jumla au mahususi kuhusiana na aina ya sabuni iliyotolewa? Jambo gani lingesaidia/kuchochea matumizi ya sabuni? Je, kulitumika aina tofauti tofauti za sabuni kunawia mikono? KAMA MAJIBU NI NDIYO, ENDELEA NA MAHOJIANO, KAMA JIBU NI HAPANA, SITISHA MAHOJIANO.

Watumiaji wa sabuni	<p>Kama bado haijajibiwa uliza, sabuni ilitumika kwa madhumuni gani na kwa nini? ZINGATIA HUSUSANI UNAWAJI MIKONO KWA SABUNI. HAKIKISHA KUWA UNACHUNGUZA SABABU ZA KILA TUKIO TOFAUTI LA UNAWAJI MIKONO KWA SABUNI (KUNA UWEZEKANO MKUBWA WA SABABU KUWA TOFAUTI).</p> <p>Je, watu wengine ndani ya nyumba walitumia sabuni, kama ndiyo ni nani hao, kwa madhumuni gani na kwa nini?</p>
Uzoefu wa matumizi ya sabuni	<p>Mambo yanayopendwa na yasiyopendwa kuhusiana na sabuni. Hisia baada ya kunawa mikono kwa sabuni—katika kila hatua. Tofauti kati ya kutumia na kutotumia sabuni—katika kila hatua. Matatizo/ugumu unaohusishwa na unawaji mikono kwa sabuni. Matatizo/ugumu ulishughulikiwaje? Je, unawaji mikono uliwahi kusahauliwa, kama ndiyo ni kwa nini na ni jambo gani lilifanywa ili kukumbuka? Mambo mazuri kuhusiana na unawaji mikono kwa sabuni. Mambo mabaya kuhusiana na unawaji mikono kwa sabuni. Faida za kunawa mikono kwa sabuni, ikilinganishwa na kunawa bila sabuni pia faida za kunawa mikono kwa sabuni bila kulinganisha na kunawa bila sabuni.</p>
Sifa za sabuni	<p>Kama mhusika hajaulizwa kuhusiana na mambo anayoyapenda na asiyoyapenda kuhusu sabuni kama yalivyoulizwa hapo juu basi muulize sasa. Je, sabuni iliyotolewa ilikuwa nzuri, au je, dukani kuna sabuni ambayo ni nzuri zaidi? Kama ndiyo, ni sabuni gani na kwa nini? Sifa muhimu zaidi za sabuni za kunawia mikono. (Dadisi: gharama, harufu, rangi, matumizi mbalimbali, utunzaji wa ngozi, ukubwa, povu, n.k). Sababu.</p>
MWISHO	<p>Baada ya mhusika kutumia sabuni kunawia mikono, je, anaona ni jambo zuri? Je, ataendelea kunawa mikono kwa sabuni baada ya mche aliopewa kwisha? Atatumia sabuni kwa kazi gani? Atamshawishije mtu mwingine kujenga tabia ya kunawa mikono kwa sabuni? Uliza “Kama nikirudi hapa baada ya mwezi au mwaka, nitakukuta ukinawa mikono kwa sabuni?” Na “Ni wakati gani utakuwa ukinawa mikono yako kwa sabuni?” ASANTE SANA KWA KUTUMIA MUDA WAKO KUZUNGUMZA NAMI, NIMEJIFUNZA MENGI KUTOKA KWAKO. MAZUNGUMZO YETU YAMEKUWA YA KUFURAHISHA. UNA MAONI YOYOTE YA MWISHO?</p>

Zana ya 2: Uchunguzi Pangilifu

Muundo Utakaotumika kwa ajili ya Utafiti wa Tabia na Ufuatiliaji na Tathmini ya Msingi

Malengo: Kuamua:

- Uwiano wa muda ambao kinamama hunawa mikono kwa sabuni baada ya kutoka chooni.
- Uwiano wa muda ambao kinamama hunawa mikono kwa sabuni baada ya kutawadha watoto wao.
- Uwiano wa muda ambao kinamama hunawa mikono kwa sabuni kabla ya kuwalisha watoto wao.
- Uwiano wa muda ambao watoto wenye umri wa kwenda shule hunawa mikono kwa sabuni baada ya kutoka chooni wawapo nyumbani.
- Uwiano wa muda ambao watoto wenye umri wa

kwenda shule hunawa mikono kwa sabuni baada ya kula wawapo nyumbani.

Maelekezo

Wasili dakika tano kabla ya muda wa kuanza kwa muda wa uchunguzi (Saa 11.55 alfajiri).

Amkia kiungwana na omba kuketi uwanjani. Weka kiti/kigoda mahali ambapo unaweza kuona shughuli za nyumbani.

Keti kimya na zungumza pale tu inapobidi.

Panapotokea tukio la muhimu, tazama kwa makini jambo linalotendeka, kisha jaza tukio hilo katika sehemu inayohusika kwenye fomu.

Baada ya kumalizika kipindi cha uchunguzi, chukua fomu ya utafiti (Hojaji).

Kabla hujaondoka, hakikisha kuwa kila swali kwenye fomu limejibiwa. Kufanya hivyo kutakusaidia kukwepa kurudi tena.

Wakati wote tumia kalamu ya bluu. Kalamu au nyenzo zingine za kuandikia za rangi nyingine hazitakubaliwa.

Zungushia jibu sahihi. Ukikosea, kata kwa msitari mmoja wa kukatiza kisha zungushia jibu sahihi.

Jibu moja tu huruhusiwa kwa kila swali.

Ni wasimamizi tu ndio huruhusiwa kujaza katika 9 au 99.

Zingatia

Muundo umebuniwa kwa ajili ya uchambuzi kwa kutumia EPIINFO: Msimbo wa herufi 5 ni vitambulisho vyake mahususi.



Uchunguzi Pangilifu wa Mienendo ya Matunzo ya Watoto

Sehemu ya I: Utambulisho

1.1	Namba ya utambulisho wa mama _ _ _ _ _ _ _			NAUMA	
1.2	Namba ya utambulisho wa mwangalizi _ _ _ _ _ _ _			NAUMW	
1.3	Jina			JINMA	
1.4	Anwani			ANWMA	
1.5	Jina la mtoto husika <5			JIMHU	
1.6	Jinsi ya mtoto kielezo	Me = 1	Ke = 2	9.	JIMKE
1.7	Tarehe ya ziara _ _ _ _ · _ _ _ _ · _ _ _ _				TARZI
1.8	Muda wa kuwasili _ _ _ _ · _ _ _ _				MUDKU
1.9	Muda wa kuanza uchunguzi _ _ _ _ · _ _ _ _				MDKUU
1.10	Muda wa kumaliza uchunguzi _ _ _ _ · _ _ _ _				MDKMU

Sehemu ya 2. Haja Kubwa kwa Mtoto Mchunguzwa

2.1	Mtoto alipata haja kubwa wakati ukiwepo? Ndiyo, nilimuona = 1 Ndiyo, nina uhakika alipata haja kubwa = 2 Hapana hakupata haja kubwa = 3	9	MHJKB
	JAZA SEHEMU YA 2 IWAPO TU MTOTO KIELEZO ALIPATA HAJA KUBWA		
2.2	Mtoto alipata haja kubwa wakati gani? _ _ · _ _		MMALK
2.3	Mtoto alikwenda haja kubwa wapi (Mara ya kwanza)? Kwenye nepi/chupi/pampa = 1 Sakafuni/uwanjani/ndani ya nyumba = 2 Kwenye kifaa cha kunyea = 3 Nje ya nyuma = 4 Kwenye karatasi = 5 Chooni = 6 Kwingineko (eleza) = 7.....	9	MAHKW
2.4	Je, kuna mtu alimtawadha mtoto? Hakuna = 1 Mama = 2 Dada = 3 Bibi/nyanya = 4 Mtu mwingine yoyote = 5	9	MTNMM
2.5	Je, kuna mtu aliondoa kinyesi cha mtoto? Hakuna = 1 Mama = 2 Dada = 3 Bibi/nyanya = 4 Mtu mwingine yoyote = 5	9	MKKIM
2.6	Mara baada ya kugusa kinyesi, je, mtu huyo . . Aliendelea na kazi zake = 1 Alisuuza mkono mmoja kwa maji = 2 Alisuuza mikono yote miwili kwa maji = 3 Alinawa mkono mmoja kwa sabuni = 4 Alinawa mikono yote miwili kwa sabuni = 5 Alisuuza mikono kwa maji ya sabuni = 6 Alioga = 7 Sikuona = 8	9	MBKKI
	Koma 2.4 na 2.5 walikuwa watu tofauti, kwa wapili jaza:		
2.7	Mara baada ya kugusa kinyesi mtu wa pili . . . Aliendelea na kazi zake = 1 Alisuuza mkono mmoja kwa maji = 2 Alisuuza mikono yote miwili kwa maji = 3 Alinawa mkono mmoja kwa sabuni = 4 Alinawa mikono yote miwili kwa sabuni = 5 Alisuuza mikono kwa maji ya sabuni = 6 Alioga = 7 Hakukuwa na mtu wa pili/Sikuona = 8	9	MBKKI
2.8	Kuna mtu aliondoa kinyesi cha mtoto baadaye? Hakuna = 1 Mama = 2 Dada = 3 Bibi/nyanya = 4 Mtu mwingine yoyote = 5	9	MBKK2
2.9	Mara baada ya kuondoa kinyesi mtu huyo . . . Aliendelea na kazi zake = 1 Alisuuza mkono mmoja kwa maji = 2 Alisuuza mikono yote miwili kwa maji = 3 Alinawa mkono mmoja kwa sabuni = 4 Alinawa mikono yote miwili kwa sabuni = 5 Alisuuza mikono kwa maji ya sabuni = 6 Alioga = 7 Sikuona = 8	9	MBKK3
2.10	Maji ya kunawia mikono (Mtu wa kwanza) yalitoka wapi? Hakunawa mikono = 1 Kutoka katika chungu/ndoo/tanki nyumbani = 2 Maji ya kufulia = 3 Bombani = 4 Sikuona = 5	9	MAKUM
2.11	Sabuni ya kunawia mikono ilitoka wapi? Sabuni haikutumika = 1 Sabuni iliyokuwa imewekwa karibu na chanzo cha maji = 2 Sabuni iliyokuwa mbali na chanzo cha maji = 3 Sikuona = 4	9	SAKMW

2.12	<p>Sabuni iliyotumika ilikuwa ni ya aina gani? Sabuni haikutumika = 01 Duck = 02 Imperial Leather = 03 Sunlight = 04 Canoe = 05 Rexona = 06 Lifebuoy = 07 Key = 08 Medimix = 09 Geisha = 10 Sweetie = 11 Johnson's Baby = 12 Ayu = 13 Safeguard = 14 Sa = 15 CB = 16 Guardian = 17 Harmony = 18 Village Fresh liquid = 19 Tempo = 20 Fa = 21 Premier = 22 Lux = 23 Orodhesha Sabuni za unga/poda = 64 Sabuni za maji ambazo hazikutambulishwa = 65 Sabuni za rangi ya kahawia ambazo hazikutambulishwa = 66 Sabuni za rangi ambazo hazikutambulishwa = 67 Sabuni za kienyeji ambazo hazikutambulishwa = 68 Sabuni nyinginezo = 77 Bainisha..... Sikuona = 88</p>	9	AISGN
------	--	---	-------

Sehemu ya 3. Kumlisha Mtoto Kielezo

3.1	<p>Je, mwangalizi wa mtoto alimlisha mtoto wakati wa uchunguzi? Ndiyo, nina uhakika = 1 Ndiyo, nadhani hivyo = 2 Hapana = 3</p>	9	MWAMU
	JAZA MASWALI YAFUATAYO IWAPO TU MTOTO KIELEZO ALILISHWA		
3.2	<p>Kwa aina ya kwanza ya chakula, nani alimlisha mtoto? Mama = 1 Dada = 2 Bibi/nyanya = 3 Mtu mwingine yoyote = 4.....</p>	9	AKCAM
3.3	<p>Ilikuwa ni chakula gani na mtoto alilishwaje? Mtoto alilishwa kwa kijiko = 1 Mtoto alilishwa kwa mkono = 2 Mtoto alilishwa chakula cha majimaji kwa kijiko/chupa = 3 Mtoto alilishwa chakula cha majimaji kwa mkono = 4 Mtoto alilishwa asusa kwa kijiko = 5 Mtoto alilishwa asusa kwa mkono = 6</p>	9	CHGMN
3.4	<p>Muda mfupi kabla ya kumlisha mtoto, mlishaji . . . Hakunawa mikono = 1 Alisuza mkono mmoja kwa maji = 2 Alisuza mikono yote miwili kwa maji = 3 Alinawa mkono mmoja kwa sabuni = 4 Alinawa mikono yote miwili kwa sabuni = 5 Alisuza mikono kwa maji ya sabuni = 6 Alioga = 7 Sikuona = 8</p>	9	MMFKM

Sehemu ya 4. Haja Kubwa kwa Mama

4.1	Je, mama alikwenda chooni wakati wa uchunguzi? Ndiyo, nina uhakika = 1 Ndiyo, nadhani hivyo = 2 Hapana = 3	9	MKWWU
	JAZA MASWALI HAYA IWAPO TU MAMA ALIKWENDA CHOONI		
4.2	Mama alikwenda haja kubwa wapi? Choo cha umma = 1 Choo nje ya uwanja = 2 Choo ndani ya uwanja = 3 Choo nje ya nyumba = 4 Kichakani = 5 Alitumia karatasi = 6 Sina uhakika = 7	9	MKWHJ
4.3	Mara tu baada ya haja kubwa mama . . . Aliendelea na kazi zake = 1 Alisuza mkono mmoja kwa maji = 2 Alisuza mikono yote miwili kwa maji = 3 Alinawa mkono mmoja kwa sabuni = 4 Alinawa mikono yote miwili kwa sabuni = 5 Alisuza mikono kwa maji ya sabuni = 6 Alioga = 7 Sikuona = 8	9	MTBKJ
4.4	Maji ya kunawia mikono yalitoka wapi? Hakunawa mikono = 1 Kutoka katika chungu/ndoo/tanki nyumbani = 2 Bombani = 3 Sikuona = 4	9	MKMYW
4.5	Sabuni ya kunawia mikono ilitoka wapi? Sabuni haikutumika = 1 Sabuni iliyokuwa imewekwa karibu na chanzo cha maji = 2 Sabuni iliyokuwa mbali na chanzo cha maji = 3 Sikuona = 4	9	SKMIW
4.6	Sabuni iliyotumika ilikuwa ni ya aina gani? Sabuni haikutumika = 01 Duck = 02 Imperial Leather = 03 Sunlight = 04 Canoe = 05 Rexona = 06 Lifebouy = 07 Key = 08 Medimix = 09 Geisha = 10 Sweetie = 11 Johnson's Baby = 12 Ayu = 13 Safeguard = 14 Sa = 15 CB = 16 Guardian = 17 Harmony = 18 Village Fresh liquid = 19 Tempo = 20 Fa = 21 Premier = 22 Lux = 23 Orodhesha Sabuni za unga/poda = 64 Sabuni za maji ambazo hazikutambulishwa = 65 Sabuni za rangi ya kahawia ambazo hazikutambulishwa = 66 Sabuni za rangi ambazo hazikutambulishwa = 67 Sabuni za kienyeji ambazo hazikutambulishwa = 68 Sabuni nyinginezo = 77 Bainisha Sikuona = 88	99	AISGN

Sehemu ya 5. Haja Kubwa kwa Mtoto mwenye Umri wa Kwenda Shule

CHUKUA TAARIFA ZA MTOTO MWENYE UMRI WA KWENDA SHULE WA KWANZA KUONEKANA

5.1	Je, ulimuona mtoto mwenye umri wa kwenda shule akienda haja kubwa wakati wa uchunguzi? Ndiyo, nina uhakika = 1 Ndiyo, nadhani hivyo = 2 Hapana = 3	9	MKSAH
JAZA MASWALI HAYA IWAPO TU MTOTO ALIKWENDA HAJA KUBWA			
5.2	Mtoto alikwenda haja kubwa wapi? Choo cha umma = 1 Choo nje ya uwanja = 2 Choo ndani ya uwanja = 3 Choo nje ya nyumba = 4 Kichakani = 5 Alitumia karatasi = 6 Sina uhakika = 7	9	MAHKW
5.3	Mara tu baada ya kupata haja kubwa mtoto. . . Aliendelea na kazi zake = 1 Alisuuza mkono mmoja kwa maji = 2 Alisuuza mikono yote miwili kwa maji = 3 Alinawa mkono mmoja kwa sabuni = 4 Alinawa mikono yote miwili kwa sabuni = 5 Alisuuza mikono kwa maji ya sabuni = 6 Alioga = 7 Sikuona = 8	9	MBKHM
5.4	Maji ya kunawia mikono yalitoka wapi? Mikono haikusuzwa = 1 Kutoka katika chungu/ndoo/tanki nyumbani = 2 Bombani = 3 Sikuona = 4	9	MKMYW
5.5	Sabuni ya kunawia mikono ilitoka wapi? Sabuni haikutumika = 1 Sabuni iliyokuwa imewekwa karibu na chanzo cha maji = 2 Sabuni iliyokuwa mbali na chanzo cha maji = 3 Sikuona = 4	9	SKMIW
5.6	Sabuni iliyotumika ilikuwa ni ya aina gani? Key = 01 Duck = 02 Imperial leather = 03....Orodhesha aina Sabuni za rangi ya kahawia ambazo hazikutambulishwa = 66 Sabuni za rangi ambazo hazikutambulishwa = 67 Sabuni za kienyeji ambazo hazikutambulishwa = 68 Sabuni nyinginezo = 88	99	AISGN

Sehemu ya 6. Mtoto mwenye Umri wa Kwenda Shule Aliyonekana Akila

ZINGATIA: CHUKUA TAARIFA ZA MTOTO MWENYE UMRI WA KWENDA SHULE WA KWANZA KUONEKANA AKILA, ANAWEZA KUWA TOFAUTI NA WA SEHEMU YA 5

6.1	Je, ulimuona mtoto mwenye umri wa kwenda shule akila wakati wa uchunguzi? Ndiyo = 1 Hapana = 2	9	UMAWU
JAZA MASWALI HAYA IWAPO TU UTAMWAONA MTOTO WA UMRI WA SHULE AKILA			
6.2	Muda mfupi kabla ya kula mtoto. . . Hakunawa mikono = 1 Alisuuza mkono mmoja kwa maji = 2 Alisuuza mikono yote miwili kwa maji = 3 Alinawa mkono mmoja kwa sabuni = 4 Alinawa mikono yote miwili kwa sabuni = 5 Alisuuza mikono kwa maji ya sabuni = 6 Alioga = 7 Sikuona = 8	9	MMFKK
6.3	Kilikuwa ni chakula gani na kililiwaje? Chakula kililiwa kwa kutumia kijiko = 1 Chakula kililiwa kwa mikono = 2 Chakula cha majimaji kililiwa kwa kutumia kijiko = 3 Chakula cha majimaji kililiwa kwa mikono = 4 Asusa ililiwa kwa kutumia kijiko = 5 Asusa ililiwa kwa mikono = 6	9	AICHK

Uchunguzi Pangilifu katika Vyoo vya Umma

Lengo la 1: Kupata idadi ya jumla ya watumiaji wa choo na idadi ya jumla ya watumiaji hao ambao hunawa mikono kwa sabuni.

Lengo la 2: Kuweka kumbukumbu ya hali ya vyoo vya umma.

Maelekezo

Wasili saa 11:55 alfajiri.

Keti mahali ambapo utaona watu wakiingia na kutoka na ambapo unaweza kuona watu wakinawa mikono, kama kitendo hicho kitakuwepo.

Chunguza.

Saa 3:00 tumia choo kisha jaza sehemu ya tatu.

Sehemu ya 1. Utambulisho

1.1	Namba ya utambulisho wa choo _ _ _ _ _		NUCHO
1.2	Namba ya utambulisho wa mchunguzi _ _ _ _ _		NUMCH
1.3	Jina la choo		JICHO
1.4	Anwani		ANWAN
1.5	Tarehe ya ziara _ _ _ · _ _ _ · _ _ _		TARZI
1.6	Muda wa kuwasili _ _ _ · _ _ _		MUDKU
1.7	Muda wa kuanza uchunguzi _ _ _ · _ _ _		MUKKU
1.8	Muda wa kumaliza uchunguzi _ _ _ · _ _ _		MUKUU

Sehemu ya 2. Hali ya Vyoo vya Umma

Zingatia: Baada ya kukamilisha uchunguzi, omba ruhusa ya kutumia choo kisha jaza sehemu hii.

Maswali yanahusu sehemu kubwa ya vyoo vinavyotumiwa na umma kwa jumla.

2.1	Kibanda cha choo kina vyumba vingapi vya wanaume? 01 02 03 04 05 06 07 08 09 10 11 12 13 14 15 16 17 18 19 20	99	KCVME
2.2	Kibanda cha choo kina vyumba vingapi vya wanawake? 01 02 03 04 05 06 07 08 09 10 11 12 13 14 15 16 17 18 19 20 (Kama hakuna mgawanyo wa ME&KE, jaza katika 2.1 tu) Je, kuna mlango maalum kwa ajili ya waheshimiwa? Ndiyo = 1 Hapana = 2	99	KCVKE
2.3	Bei ya kutumia choo kwa watu wazima ni shilingi ngapi? _ _ _ _ _ Tsh		

2.4	Bei ya kutumia choo kwa mtoto ni shilingi ngapi? _ _ _ _ _ Tsh		
2.5	Zipi ni gharama za ziada kwa ajili ya karatasi za msalani? _ _ _ _ _ Tsh		
2.6	Zipi ni gharama za ziada kwa ajili ya kunawa mikono? _ _ _ _ _ Tsh		
2.7	Miundombinu/vifaa vya choo viko katika hali gani? Kinapendeza, hutunzwa vizuri, kibanda kimeezekwa, kimepakwa rangi hivi karibuni = 1 Wastani, kina nyufa, kimepigwa rangi lakini si hivi karibuni = 2 Kuukuu, kimechakaa = 3	9	
2.8	Sakafu iko katika hali gani? Imara na safi sana = 1 Nyufa, haijasafishwa = 2 Imechakaa na ni chafu = 3	9	
2.9	Vyumba vya choo viko katika hali gani? Imara na safi sana = 1 Nyufa, haijasafishwa = 2 Imechakaa na ni chafu = 3	9	
2.10	Shimo/tundu liko katika hali gani? Sinki la maji machafu = 1 Shimo, halijajaa = 2 Shimo, linaonekana karibu litajaa = 3 Shimo, limejaa = 4 Shimo, limefurika = 5	9	
2.11	Umejisikiaje ulipotumia choo? Kinanuka sana na kinakera = 1 Kinanuka na kinakera = 2 Wastani = 3 Kisafi sana na hakinuki = 4	9	
2.12	Maoni mengine (wadudu, inzi, nyufa na kuta hatari, kinyesi sakafuni, nk)		
2.13	Kuna nyenzo zozote za kunawia mikono ndani ya jengo la choo? Ndiyo = 1 Hapana = 2		
2.14	Kuna nyenzo zozote za kunawia mikono mara tu baada ya kutoka ndani ya jengo la choo? Ndiyo = 1 Hapana = 2		
	Kama ni Hapana kwa 2.13 na 2.14 ruka hadi Q		
2.15	Chanzo cha maji ya kunawia mikono Hakuna = 1 Beseni lenye koki ya maji (inayofanya kazi) = 2 Stendi ya kunawia mikono yenye maji = 3 Bakuli/ kifaa chenye maji ambacho unatumbukiza mikono = 4 Kifaa chenye maji wanayopewa wateja = 5 Vinginevyo (Eleza)= 6.....	9	
2.16	Je, sabuni ya kunawia mikono inapakana? Ndiyo = 1 Hapana = 2		

2.17	<p>Ni aina gani ya sabuni hupatikana?</p> <p>Sabuni haikutumika = 01 Duck = 02 Imperial Leather = 03 Sunlight = 04 Canoe = 05 Rexona = 06 Lifebuoy = 07 Key = 08 Medimix = 09 Geisha = 10 Sweetie = 11 Johnson's Baby = 12 Ayu = 13 Safeguard = 14 Sa = 15 CB = 16 Guardian = 17 Harmony = 18 Village Fresh liquid = 19 Tempo = 20 Fa = 21 Premier = 22 Lux = 23 Orodhesha Sabuni za unga/poda = 64 Sabuni za maji ambazo hazikutambulishwa = 65 Sabuni za rangi ya kahawia ambazo hazikutambulishwa = 66 Sabuni za rangi ambazo hazikutambulishwa = 67 Sabuni za kienyeji ambazo hazikutambulishwa = 68 Sabuni nyinginezo = 77 Bainisha..... Sikuona = 88</p>		
------	--	--	--



**Sehemu ya 2. Uchunguzi wa
Walengwa Wakitoka Chooni**

Maelekezo: Jaza kwa watu wote wanaotoka chooni. Ukikosa hata kama walinawa mikono yao andika "sikuona".

Ni muhimu sana kuweka kumbukumbu za watu wote wanaotoka.

Mtu	Weka vema sehemu moja				Kwa matumizi ya ofisi
	Muda wa kutoka	Hakunawa	Alinawa kwa maji	Alinawa kwa sabuni	
1					
2					
3					
4					
5					
6					
7					
8					
9					
10					
11					
12					
13					
14					
15					
16					
17					
18					
19					
20					
21					
22					

Zana ya 3: Makundi Lengwa

Vifaa vya Kuchunguzia Tabia za Unawaji Mikono Mwongozo wa Majadiliano ya Makundi Lengwa

Maelekezo kwa Watafiti wa Uwandani:

Tabia kuu tunayoizingatia ni unawaji mikono kwa sabuni, mambo yanayochochea au kukwaza wanawake kuendeleza tabia hii. Mahususi kabisa, tunalenga unawaji mikono kwa sabuni baada ya haja kubwa, baada ya kutawadha mtoto, baada ya kutupa kinyesi cha mtoto, na kabla ya kulisha mtoto.

Wakati wa mahojiano na kikundi lengwa, unapaswa kudadisi sababu, mambo yanayopendwa na yasiyopendwa kwa kila tukio pekee la unawaji mikono, ukichunguza iwapo sabuni hutumika au la na kwa nini. Kimaandishi huweza ikawa vigumu kutofautisha iwapo watu wanazungumza kuhusu kuoga, unawaji mikono kwa kutumia maji pekee, au unawaji mikono kwa sabuni. Hivyo ni muhimu kuweka bayana washiriki wanazungumzia nini kati ya mambo hayo matatu katika kila tukio. Wakati tabia za uogaji za wanawake huweza kuwa za kusisimua na huweza kutufumbua macho kuhusu motisha ya tabia nyingine zaidi za usafi wa jumla, lengo la mahojiano mara zote live *unawaji mikono kwa sabuni*.

Aghalabu wahojiwa watarejelea dhana zenye vionjo binafsi kama vile usafi na uchafu. Ni muhimu kudadisi humaanisha nini wanapotumia dhana hizo na jinsi zilivyodhihirishwa, ukizingatia hususani, vidokezo vya fahamu (kugusa, kuona, kunusa, n.k.) vilivyotumika. Mara nyingi zitatajwa tabia, au wanawake hawatakuwa na uhakika ni kwa nini hunawa mikono kwa sabuni; jaribu kudadisi lini walianza kunawa mikono kwa sabuni, nani aliwafundisha, kwa nini na lini. Kila mara mshiriki anapotoa sababu ya tabia fulani, hususani unawaji mikono kwa sabuni jaribu kudadisi kwa undani kadiri iwezekanavyo, mara nyingi jibu la awali liwe msingi wa kupata taarifa zaidi, na lengo letu ni kuzipata hizo taarifa zaidi. Zipi ni faida kuu za unawaji mikono kwa sabuni?

Katika majadiliano ya kundi lengwa ni kawaida kwa washiriki fulani kutawala mjadala wakati wengine hukaa kimya. Tunataka kusikia mtazamo wa kila mmoja, hivyo jaribu kuhamasisha kila mmoja kuchangia. Vile vile ni muhimu kuwaruhusu wanawake wenyewe kuamua namna ya kuendesha mazoezi na majadiliano. Ukiwa mwezeshaji, usitawale sana mjadala: ni muhimu wanawake wajihisi kutawala kile wanachokifanya au kujadiliana.

Majadiliano

Kabla ya kuanza, waeleze wanawake kwamba hakuna jibu la kweli au la uongo na kwamba unachohitaji ni kujifunza kutoka kwao na kusikia kile wanachofikiria. Anza na utambulisho. Kila mwanamke ajitambulishe yeye mwenyewe (anaweza kutumia jina la utani/bandia), kazi yake, kazi ya mume wake, idadi ya watoto wake, na umri wa watoto wake.

Majadiliano yetu yatalenga mlolongo wa mazoezi ili kuhimiza maingiliano katika kikundi: maudhui ya msingi ya kila zoezi yameelezwa hapa chini:

Mazoezi

1. Kazi za Kila Siku/Maadili ya Maisha

- Waombe wanawake kueleza shughuli wanazozifanya kila siku, shughuli muhimu zijazwe kwenye karatasi tofauti tofauti.

- Baada ya kila mwanamke kuandika ufupisho wa shughuli za kila siku, waombe wapange kazi zao kwa mfuatano unaozingatia umuhimu na furaha inayotokana na kila shughuli. Wanaweza kuchanganya karatasi jambo ambalo husaidia kuchangamsha mawazo na mjadala.

- Waombe wanawake kuelezea sababu zilizowafanya kupangilia shughuli kama walivyofanya.

2. Uwekaji wa Matumizi ya Sabuni katika Madaraja

- Muombe kila mwanamke kueleza anatumia sabuni kwa kazi gani, akielezea kila matumizi katika karatasi tofauti.

- Baada ya kila mwanamke kuandika ufupisho wa matumizi makuu ya sabuni, waombe wapange kazi zao kwa mfuatano unaozingatia umuhimu, kwa nini hufanya hivyo na sababu za mpangilio waliouchagua.

3. Uwekaji wa Matukio ya Unawaji Mikono katika Madaraja

- Waulize wanawake ni wakati gani hunawa mikono, wakielezea kila tukio la unawaji mikono katika karatasi tofauti. Kwa kila hali waulize iwapo sabuni hutumika na andika jibu lake katika karatasi tofauti.

- Sambaza karatasi katika makundi mawili: kunawa kwa sabuni na kunawa bila sabuni.

- Kwa kila kundi, waulize wanawake matukio yapi ni muhimu zaidi kwa unawaji mikono na ni kwa nini unawaji mikono hufanyika.

- Kuhusiana na maji tu, uliza kwa nini sabuni haitumiki.

- Kuhusiana na sabuni tu, uliza kwa nini sabuni hutumika.

- *Zingatia—katika kujadili sababu za unawaji mikono (kwa sabuni na bila sabuni), udadisi wa kina ni muhimu ili kuelewa vidokezo muhimu zaidi. Maneno kama usafi na uchafu si sababu: sababu ya unawaji mikono huchukuliwaje? Vidokezo vya fahamu, hisia za maambukizi, ushuhudiaji wa watu wengine, ulinzi wa mtoto, n.k.*

4. Zoezi la Ugezaji

- Waombe wanawake waeleze sifa za watu hawa wawili:

1. Mtu ambaye, kwa kawaida, hunawa mikono yake kwa sabuni.
2. Mtu ambaye kamwe hanawi mikono kwa sabuni.

Dadisi: Mwonekano, mambo anayoyapendelea, mapenzi yake kwa muziki, kiwango cha elimu, nafasi yake katika jamii, mandhari ya nyumba yake, watu huwaonaje, n.k.

- Wanawake huwaonaje/huwafikiriaje watu hao wawili waliowaelezea?

5. Uwekeaji wa Dhana katika Madaraja

- Wasomee wanakikundi dhana moja moja (ukubalifu wa kijamii, hadhi, afya, malezi/watoto, usafi/maambukizi, uangalifu).

- Baada ya kila dhana, waombe wanawake wajadili jinsi wanavyojisikia kuhusiana na dhana hiyo na umuhimu wake kwao.

- Baada ya kila dhana kuwa imeshajadiliwa, wasilisha kila moja katika karatasi tofauti na waombe wanawake wazipange kwa mfuatano wa:

- Umuhimu
- Umajudi
- Upendeleo
- Maudhi

- Waombe waeleze sababu za mpangilio waliotoa.

- Mwisho waulize ni dhana gani huwaathiri sana na dhana gani wanadhani itawasaidia sana katika kujaribu kumshawishi mtu kujifunza tabia mpya kama ile ya unawaji mikono kwa sabuni kabla ya “Taja tukio”.

6. Njia za Mawasiliano

Waulize wanawake kuhusu vyanzo vyao vikuu vya habari za:

- Kimtaa
- Kitaifa
- Kimataifa
- Masuala ya afya
- Mara ngapi wao hupata habari kutoka kila chombo walichokitaja?
- Ni njia ipi kati ya hizi huipenda zaidi? Kwanini?
- Ni njia ipi kati ya hizi huiamini zaidi/wao huziamini sana?
- Ni matangazo gani ya biashara wameyaona/kusikia na kuyapenda baadaye sana? Kwanini waliyapenda? Je, matangazo hayo huwafanya wapende kununua bidhaa zinazotangazwa?

Zana ya 4: Vidokezo katika Kutafiti Watoto wenye Umri wa Kwenda Shule

Vyoo vya shule havitumiki tu kwa masuala ya kiusafi. Wasichana waliovinja ungo wakati mwingine hukutana huko ili kujipodoa, kuwajadili wavulana, na kupanga mipango ya baada ya shule; na wavulana huweza kuvuta sigara. Watoto huweza kuwa na misukumo tofauti ya kutumia vyoo, hasahasa kusengeny na kuwa na muda wa faragha na marafiki zao, mbali na macho ya walimu wao. Watoto huweza kukataa kunawa mikono yao wawapo shuleni, kwa sababu kuwa mwanafunzi mzuri huhusishwa na mikono yote kuwa na vumbi la chaki. Sifa nyingine muhimu sana ya shule ni ukweli kuwa watoto hawataki kupoteza hata dakika moja ya kucheza na marafiki zao. Mambo haya yanapaswa kukumbukwa wakati wa kutafiti watoto.

Vidokezo:

1. Utengaji kimakundi: Fikiri kama mtoto. Watoto wana ajenda zao ambazo ni muhimu kwao. Wakati ambapo umri wa balebhe kwa msichana mwenye umri wa miaka 12 aliyevunja ungo unaweza kuwa ni kichocheo cha usafi, asili ya uchezaji ya mtoto wa umri wa miaka sita huweza kuhitaji mkabala tofauti. Kama utengaji wa marika tofauti tofauti hautafanywa vyema, ni dhahiri kuwa uhanasishaji wa mabadiliko ya tabia hautakuwa madhubuti.

2. Kuwa mbunifu. Njia zilizozoeleka za makundi lengwa na hojaji huenda zisigundue ukweli. Kwa watoto wenye umri wa chini ya miaka 10, mahojiano, kama inawezekana, yazingatie ushuhudiaji na maigizo/michezo. Njia za utafiti zinazojumuisha vichocheo (picha za video, michoro, picha, michezo ya asili) hutoa ufahamu nzuri. Kujua nyimbo na michezo yote ya kienyeji inayotamba husaidia sana.

3. Watoto wabadilishane nafasi katika vikundi. Watoto hupenda kuwa katika vikundi na hawapendi kutenganishwa na marafiki zao. Njia za utafiti zinazojumuisha vikundi vya michezo na jozi za urafiki (kuwahoji marafiki wawili kwa wakati mmoja) huwezesha kupata ufahamu nzuri. Maswali huweza kuelekezwa tena kwao ili watoto waweze kuzungumza wao kwa wao.

4. Watenge watoto na watu wazima. Shuleni kuna mienendo ya hatari inayofanywa na watu wazima (walimu na walimu wakuu) ambayo watoto huifahamu na huweza kuogopa kuisema wakati wa utafiti unaofanywa katika mazingira ya shuleni (mathalani, kwa utaratibu maalum, walimu huweza kuchukua sabuni na kuzipeleka majumbani mwao). Njia tofauti tofauti zitahitajika ili kukusanya ufahamu kutoka katika makundi tofauti tofauti. Mlinzi wa shule katika mazingira fulani huheshimika sana na ni mtu muhimu miongoni mwa watoto.

5. Watoto huweza kuwa watafiti wakuu. Watoto huweza kuwa watafiti wakuu wakifanya utafiti katika makundi yao ya rika. Wanaweza kutofautisha kati ya ukweli na mambo ya kubuni. Fikra za ushindani mara nyingi huwachochea watoto kujieleza. Kuandaa shindano ili kuwafanya watoto kuelezea

kukata tamaa kwao kuhusiana na hali duni ya usafi shuleni mwao na kubainisha baadhi ya mambo yanayojirudiarudia. Jaribu kuwauliza wanafunzi kitu kimoja kwa namna tofauti tofauti ili kupata ukweli; mathalani, waombe wachore, kuandika, kutunga maneno, na kubuni vichekesho na katuni.

6. Anza na mwalimu mkuu. Mwalimu mkuu huweka mwelekeo wa shule yake na huamua iwapo usafi ni moja ya ajenda muhimu. Kumhoji mwalimu mkuu kisha kumpa ripoti ya utafiti kutakuhakikishia kupata baraka za mamlaka za elimu.

7. Tambua “Vinara wa mfano”. Vinara wa mfano au vinara wa maoni ni muhimu katika mazingira ya kijamii. Watoto hujiumba wenyewe kwa kuiga vinara wachache shuleni. Kuwatambua vinara hao ni muhimu katika kujua kipi ni safi, kipi kinapatikana, na ipi ni njia nzuri ya kushughulikia mtoto mwingine. Walimu huweza kuwatambua. Tazama uwezekano wa kuwafundisha vinara waliobainishwa ili kuendesha vikundi lengwa.

Mambo ya kuepuka:

1. Kutumia muda wa mapumziko kwa ajili ya hojaji. Watoto hupenda muda wao wa mapumziko. Ukiuchukua, majibu yao hayatafaa sana kwakuwa watakuwa wakiharakisha ili waende nje kukutana na marafiki zao. Ukipanga kufanya utafiti wakati huo, hakikisha kuwa ni kazi ya kikundi na kuwa watoto wanafurahia.

2. Kuwafanya watoto wajione wadogo zaidi kuliko walivyo. Kama kuna kitu kisichopendwa na watoto, basi ni kuwafanya wajione wadogo zaidi kuliko walivyo. Watoto huchukua kugeuzwa watoto wadogo. Ni muhimu kujua kwamba kinachokubaliwa na kila kikundi ni muhimu sana.

3. Kutotunza siri. Hakuna tofauti kati ya kutafiti watoto na watu wazima kuhusiana na utunzaji wa siri ya taarifa zilizotolewa. Watoto hutarajia hili.

4. Kuamini kila kinachosemwa na watoto. Jambo la msingi katika kutafiti watoto ni kile wasichoweza kukisema. Watoto wana fikra bayana kuhusiana na kile wanachofikiria kuwa mtafiti anataka kukisikia.

Hadidu za Rejea I: Utafiti wa Walengwa

1. Usuli

Ugonjwa wa kuhara hua takribani watoto milioni mbili kila mwaka. Kinyesi cha binadamu ni chanzo kikuu cha vijidudu vya ugonjwa wa kuhara na huenda wakati muhimu sana wa kunawa mikono kwa sabuni ni baada ya kugusa kinyesi cha binadamu na kabla ya kushika chakula. Mapitio mapya ya hivi karibuni ya ushahidi wote uliopo huonesha kuwa unawaji mikono kwa sabuni huweza kupunguza matukio ya ugonjwa wa kuhara kwa asilimia 42 hadi 46 na kuokoa maisha ya angalau watu milioni moja ulimwenguni kote.

Benki ya Dunia na Programu ya Maji na Usafi, Shule ya Usafi na Dawa za Kitropiki ya London, Akademia ya Maendeleo ya Elimu, na sekta binafsi, kwa kushirikiana na Shirika la Misaada la Marekani, Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto, na Ushirika wa Benki na Maji Uholanzi hutekeleza juhudi za kiulimwengu zinazolenga kuchochea matumizi ya unawaji mikono kwa sabuni katika nchi zinazoendelea. Ushirika ulianzishwa katika maeneo mawili ya majaribio mnamo mwaka 2001: Ghana na Kerala, India. Katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 03, juhudi zitapanuka hadi katika nchi angalau mbili zaidi.

Katika (*nchi*), (*shirika linaloongoza nchini*), Programu ya Maji na Usafi, na Benki ya Dunia kwa kushirikiana na washirika wengine wa sekta ya umma na ya binafsi, inapendekeza kuanzishwa kwa Juhudi za Unawaji Mikono za Ushirika wa Sekta ya Umma na ya Binafsi zikiwa na malengo ya jumla ya kuboresha afya ya watu dhidi ya hatari ya ugonjwa wa kuhara kupitia ushirika wa sekta ya umma na ya binafsi unaohamasisha unawaji mikono kwa sabuni.

Zingatia: andiko hili huhusika tu na utafiti msingi. Tafiti tofauti za ufuatiliaji na tathmini zitafanywa kwa lengo la kubainisha matokeo ya programu.

2. Uhalali wa unawaji mikono katika (*nchi*)

Uhalali wa kupendekeza juhudi za aina hizo katika nchi ni:

Magonjwa ya kuhara ni moja ya vyanzo vya magonjwa na vifo katika (*nchi*) kwa watoto wenye umri wa miaka chini ya mitano (chanzo).

Data za kuaminika kuhusiana na unawaji mikono kwa sabuni baada ya kutumia choo au baada ya kutawadha mtoto ni (*hazipatikani*) katika (*nchi*). Hata hivyo, . . .

Majadiliano yasiyo rasmi na wanawake na wanaume katika jumuiya yalionesha kuwa . . .

Hivi sasa inafahamika kuwa unawaji mikono ni njia nafuu ya kupunguza matukio ya ugonjwa wa kuhara ikilinganishwa na gharama za ujenzi wa programu za miundombinu (yaani maji na usafi). Hata hivyo, katika kipindi cha nyuma, juhudi za kuchochea usafi katika nchi zililenga utoaji zana za maji na usafi, njia bora za uhifadhi, kutibu maji lakini si unawaji mikono. Hivyo, ni masuala machache sana hufahamika kuhusiana na upatikanaji, uwezo wa kununua, na kupenda kutumia sabuni, hususani baada ya kugusa kinyesi, vijijini na katika miji midogo. Kuna haja ya kuoanisha kampeni za usafi/usambazaji wa huduma za maji na majitaka, kwa upande mmoja na uzalishaji na usambazaji wa sabuni za gharama nafuu, kwa upande mwingine. Viwanda vitarajie faida kutokana na mauzo zaidi ya sabuni kupitia upanuzi wa masoko yao kwa kaya nyingi zaidi na ufikiaji mzuri zaidi wa masoko kuelekea kwenye kaya maskini sana. Mashirika ya umma yatarajie faida kutokana na kushirikisha watengenezaji wa sabuni katika

programu zao yakilenga kuinua ubora wa maisha kwa njia ya kupunguza magonjwa yanayohusiana na mienendo mibaya ya usafi. (fanya iendane na wakati/ondoa inavyotakikana)

3. Malengo ya kazi yenyewe

Utafiti msingi utawawezesha washirika kubuni kampeni inayofaa ya unawaji mikono. Kwa hiyo, lengo kuu la utafiti huu ni kujenga utambuzi unaohitajika katika kubuni programu madhubuti ya mawasiliano ili kuhamasisha unawaji mikono kwa sabuni.

Malengo mahususi ya kazi ni:

- Kuweka kumbukumbu za tabia zilizopo hivi sasa ya unawaji mikono na mazingira yake;
- Kuelewa masuala yanayochochea na kuwezesha unawaji mikono katika jumuiya;
- Kubainisha walengwa; na
- Kuweka kumbukumbu ya njia za mawasiliano zilizopo hivi sasa.

4. Njia

Utafiti unahitaji matumizi ya njia zote mbili za utafiti ambazo ni kutafiti hali halisi na kutafiti tabia na huweza kujumuisha mahojiano na kundi lengwa, majaribio ya tabia, mahojiano rasmi, na uchunguzi pangilifu kwa ajili ya ukusanyaji wa data (kama ilivyooneshwa katika sehemu B ya kiambatisho), hali kadhalika uwekaji pamoja wa data za kila siku.

Utaratibu wa kina wa utafiti utapendekezwa na mtafiti aliyeteuliwa na kisha kukamilishwa kwa kushirikiana na mshauri wa ufundi (yaani mshauri wa shirika kuu lililoteuliwa kusimamia programu) pamoja na msaada wa kiufundi wa washirika. Njia kwa ajili ya mbinu za utafiti zimeelezwa katika vijitabu "Furaha, Afya na Usafi" (Shirika la Umoja wa mataifa la Kuhudumia Watoto na Juhudi za Unawaji Mikono za Ushirika wa Sekta ya Umma na ya Binafsi, 1998).

5. Majukumu ya mtafiti aliyeteuliwa

Mtafiti atawajibika na masuala yafuatayo: Pendekezo la utafiti lenye maelezo ya kina kwa kushirikiana na (Mtafiti mkuu) (yaani mteja) na washauri wao wa kiufundi.

Kuandaa na kusimamia utafiti.

Mipango ya utaratibu wa ugavi. Yaani usafiri, malazi, posho, mawasiliano, na vifaa vya ofisini.

Kuhakikisha ubora unakuwepo.

Uchambuzi wa matokeo.

Utoaji wa ripoti ya mwisho katika nakala kumi.

Ni wajibu wa wakala kuajiri, kutoa mafunzo, kuelimisha na kusimamia watendaji mahiri katika ngazi ya jamii.

Mtandao wa ushirikiano wa kimataifa utatoa msaada na ushauri wa kitaalaam kwa wakala katika hatua mahususi za kiutekelezaji. Msaada huo unaweza kujumuisha: kupitia na kutathmini taarifa zote za kitaalam zitakazowasilishwa na wakala; kupitia mapendekezo ya namna ya kufanya kazi, na miongozo itokanayo na uzoefu uliokwisha patikana; kusaidia mafunzo ya maafisa watekezaji hasa katika kipindi cha kupitia, kujaribu, krekebisha na kukamilisha rasimu zote; kusimamia na kutathmini ubora na mienendo ya shughuli na kurekebisha iwapo italazimika kufanya hivyo; kupitia taarifa ya awali na kutoa mapendekezo kwajili ya ukamilishaji wa taarifa ya mwisho.

6. Sifa na uteuzi wa mtafiti

Mtafiti atakuwa ni mlengwa mtaalamu au shirika la utafiti wa masoko likiwa na rekodi nzuri ya angalau miaka mitano katika utafiti wa wateja katika (nchi na/au kanda). Timu itahitaji kuonesha uzoefu wa wajumbe wake katika mbinu za utafiti wa hali halisi na utafiti wa tabia. Uzoefu wa kibiashara/kimasoko ni muhimu.

Sifa za timu iliyopendekezwa zitakuwa ni sehemu ya makabidhiano na zinapaswa kuwa kama ifuatavyo:

Mtakwimu mmoja na mtaalamu wa sayansi ya jamii au wa anthropolojia mwenye sifa zifuatazo:

- Rekodi nzuri katika utafiti mpana wa hali na tabia;
- Uzoefu katika uwanja husika;
- Uzoefu katika bidhaa za usafi; na
- Ujuzi wa lugha ya eneo husika.

Watafiti wa uwandani wanapaswa kuwa na sifa zifuatazo:

- Uzoefu wa angalau mwaka mmoja wa utafiti wa uwandani;
- Wawe wanawake; na
- Wawe na ujuzi wa lugha ya eneo husika (ujuzi unaoridhisha).

Kampuni itatoa mpango wenye maelezo ya kina ya uongozi na uhakikisho wa ubora wa utafiti na uthibitisho wa wafanyakazi.

7. Kazi ya mwisho

Kazi ya mwisho itajumuisha:

Seti za data za kielekitroniki zilizohakikiwa na kuwekewa marejeo na kuwekwa katika muundo uliokubaliwa pamoja na nakala halisi za fomu za kukusanyia data.

Karatasi zote za mahojiano ya kina pamoja na mahojiano katika vikundi lengwa zikiwa katika muundo wa kielekitroniki.

Andiko la kurasa hamsini likiwa katika nakala kumi za matokeo yenye maelezo ya kina.

Andiko la muhtasari, lililo kamili, lenye kurasa nane linalofaa kwa matumizi ya kawaida, na nakala ya kielekitroniki ya andiko la muhtasari linalofaa kuwekwa katika tovuti.

Uwasilishaji wa matokeo katika warsha ya wadau.

Ripoti kuu itajumuisha yafuatayo:

I. Mkabala

II. Njia

III. Ratiba ya utekelezaji

IV. Matokeo yaliyowekwa kwa kutumia kielelezo cha jedwali katika sehemu A ya kiambatisho

V. Hitimisho na mapendekezo

Ripoti itajumuisha michoro pale panapohitajika. Viambatisho vitajumuisha taarifa zote za usuli za utafiti ambazo si muhimu katika kiini cha utafiti.

8. Ratiba

Inatarajiwa kuwa kazi itakamilika katika wiki 13 kuanzia uteuzi hadi ripoti ya mwisho. Ratiba ya kila awamu imeoneshwa katika jedwali lifuatalo:

Tukio/shughuli	Wakati
Uandaaji na mafunzo	Wiki ya 1
Ripoti ya mwanzo ikiwa na njia na vifaa vilivyojari biwa kabla	Wiki ya 2
Utafiti wa uwandani	Wiki ya 3 hadi 10
Uchambuzi	Wiki ya 10
Ripoti ya mwanzo na warsha ya wadau	Wiki ya 11
Ripoti ya mwisho	Wiki ya 14

Sehemu A: Kiunzi cha masuala na mbinu za kukusanyia data

Maelezo yafuatayo yanaweka kiunzi cha utafiti msingi katika unawaji mikono na kimekusudiwa kutumika kama mwongozo kwa mtafiti katika kuandaa na kufanya utafiti.

Masuala	Chanzo cha Data/Njia	Maelezo
1. Ipi ni mienendo ya sasa ya unawaji mikono?		
<p>1.1 Ipi ni mienendo ya unawaji mikono ya walezi wa watoto (katika matukio makuu)?</p> <p>1.2 Ipi ni mienendo ya unawaji mikono ya wanafamilia wengine (katika matukio makuu)?</p> <p>1.3 Ni sabuni gani (kati ya ile ya kufulia na ya kuogea) au kitu kingine hutumika?</p> <p>1.4 Kipi ni chanzo cha maji?</p> <p>1.5 Sabuni huwekwa wapi?</p> <p>1.6 Watu hukaushaje mikono yao baada ya kunawa?</p>	<p>Sampuli wakilishi ya kiidadi kuhusu mienendo ya unawaji mikono kwa kutumia uchunguzi pangilifu</p>	<p>Zingatia 1: Rejea kiunzi cha Ufuatiliaji na Tathmini.</p> <p>Zingatia 2: Matukio mahususi ya unawaji mikono yatakayoandikwa hutegemea malengo halisi ya programu ya unawaji mikono.</p> <p>Zingatia la 3: Uchunguzi pangilifu unahitaji kubuniwa ili kujumuisha matukio yote ya unawaji mikono katika hatua kuu.</p>
2. Ni mambo gani huchochea na kuwezesha unawaji mikono?		
<p>2.1 <i>Vichocheo</i></p> <p>Ni mambo gani huchochea usafi wa nyumbani, uogaji, na unawaji mikono kwa sabuni?</p> <p>Ni baada ya nini unawaji mikono hufanywa?— Na/bila sabuni?</p> <p>Vidokezo mahususi na matukio ya watu kunawa mikono yao.</p> <p>Sababu za kutotumia sabuni kunawia mikono katika matukio makuu? Yaani vikwazo vya kijamii na kisaikolojia vya utumiaji sabuni— gharama, harufu, ukakamaishaji wa ngozi. . .</p> <p>Watu walijifunzaje na lini unawaji mikono?</p> <p>Zipi ni sifa za sabuni bora ya kunawia mikono?</p> <p>Upangiliaji wa sabuni na sifa zake kwa unawaji mikono (uliza ni kwa nini zimepangwa hivyo) na mienendo ya unawaji mikono.</p> <p>Upangiliaji wa vichocheo/dhana zilizodhaniwa (hadhi, malezi, maudhi, uzuri, mvuto).</p> <p>Mwonekano/imani kuhusiana na na usafi/uchafu, afya/mtu asiye na afya. . .</p> <p>kanuni za matumizi ya sabuni ndani ya kaya.</p>	<p>Majaribio ya tabia, mahojiano ya kina pamoja na watoto wenye umri wa kwenda shule (kiasi cha miaka 12)</p> <p>Majadiliano ya kikundi lengwa</p>	<p>Zingatia la 4: Kichocheo ni msukumo au kikwazo cha kijamii na kisaikolojia cha tabia za usafi na huweza kuwa chanya au hasi.</p> <p>Zingatia la 5: Unapochunguza vichocheo vya tabia ya usafi, ni muhimu kuchunguza vichocheo vya usafi wa jumla, uogaji, unawaji mikono (bila sabuni) na unawaji mikono kwa sabuni tofauti tofauti, hususani ukizingatia unawaji mikono kwa sabuni.</p> <p>Zingatia la 6: Dadisi maana ya “safi” na “chafu” je dhana hizi hufasiliwa kwa kuona, kuhisi, kunusa, au dhana ya usafi wa kimaadili?</p> <p><i>Mazingira</i> humaanisha hali za nje zinazoweza au kukwaza unawaji mikono kwa sabuni. Tazama zingatia lililoambatishwa kuhusu <i>Uchocheaji wa Unawaji Mikono</i> (Kiambatisho 3).</p> <p>Mafunzo ya uchocheaji na upangiliaji wa dhana unahitajika.</p>

<p>2.2 Mazingira</p> <p><i>Usambazaji maji:</i> Mahali, Aina, Upatikanaji, (gharama, umbali, mhusika), Uhifadhi.</p> <p><i>Vifaa vya Usafi:</i> Mahali, Aina na Upatikanaji (pia kwa watoto), Uwepo kinyesi uwanjani?</p> <p><i>Vifaa vya kunawia mikono:</i> Ni aina gani? (dadisi) Kiko wapi?/upatikanaji—Umbali kutoka chooni, Mahali pa kutunzia sabuni, Hali, Ufikiwaji.</p>	<p>Utafiti wa kaya</p> <p>Uchunguzi pangilifu</p> <p>Mahojiano ya kina</p> <p>Majadiliano ya kikundi lengwa</p>	
<p>3. Walengwa ni nani?</p>		
<p>3.1 Nani hununua sabuni?</p> <p>3.2 Nani huamua kuhusu ununuzi wa sabuni?</p> <p>3.3 Nani huwashawishi wanunuzi na wafanya maamuzi?</p>	<p>Majadiliano ya kikundi lengwa</p> <p>Mahojiano ya kina</p> <p>Utafiti wa kaya</p>	
<p>4. Walengwa huwasilianaje?</p> <p>Upatikanaji na ufikiwaji wa njia zote za mawasiliano za kisasa na za kienyeji.</p>		
<p>4.1 Muda unaotumika na wakati unaotumika kufuatilia habari katika chombo cha habari (data kuhusu kiasi).</p>	<p>Utafiti wa kaya</p> <p>Majadiliano ya kikundi lengwa/ Mahojiano ya kina</p> <p>Data zilizopo za vyombo vya habari vya kibiashara</p>	<p>Zingatia la 7: Ruhusu/idhinisha gharama za kuchunguza hazina ya data za kibiashara.</p>
<p>4.2 Mawanda ya njia zote za habari za kienyeji ?</p> <p>4.3 Mawanda ya njia za mwasiliano za serikali?</p> <p>4.4 Ni vipindi gani hupendelewa na kwa nini? Wanakumbuka nini? (data za tabia)</p> <p>4.5 Wanayafahamu na kuyapenda matangazo gani, na kwa nini?</p> <p>4.6 Ni njia gani za mawasiliano wanazoziamini sana sana?</p>	<p>Utafiti wa kaya</p> <p>Majadiliano ya kikundi lengwa/ Mahojiano ya kina</p>	<p>Zingatia la 8: Njia za kienyeji huweza kujumuisha makanisa, mashirika ya kijamii, makundi ya wanawake, masoko, matukio ya kienyeji, n.k. Njia za kiserikali hujumuisha upatikanaji wa huduma za afya (mfano chanjo, uzazi na matunzo baada ya uzazi), shule, huduma za kilimo, mamlaka za mitaa, n.k.</p>

Sehemu B: Fasili ya Zana za Utafiti

Utafiti wa Kaya: Hubuniwa kwa ajili ya sampuli wakilishi ya wazazi/waangalizi wa watoto na watoto wenye umri chini ya miaka mitano.

Mahojiano ya Kina: Mahojiano ya uso kwa uso ya ubora pamoja na maandishi yaliyoandikwa kikamilifu kwa kutumia mwongozo wa mahojiano.

Majaribio ya Tabia: Watu wa kujitolea huombwa kufanya kitendo cha unawaji mikono kwa sabuni kwa kipindi cha wiki mbili kisha huhojiwa.

Uchunguzi Pangilifu: Ni mbinu zilizopangiliwa kwa ajili ya kuchunguza na kuweka kumbukumbu za tabia mahususi ili kuzihesabu moja kwa moja na kufuatilia matokeo ya programu. Inahitaji upangaji makini, majaribio kamili, mafunzo, ufuatiliaji na udhibiti wa ubora.

Orodha ya Kuchunguzia: Orodha ya tabia zote zinazowaweka watoto katika hatari ya homa ya kuhara. Orodha inapashwa kuzingatia tabia (nani, nini, lini, wapi) zilizochunguzwa. Matokeo hutumika kubunia vifaa vya utafiti.

Majadiliano ya Makundi Lengwa: Mahojiano na vikundi vidogo vidogo vya watu wenye sifa zinazofanana huombwa kujibu maswali ya mhajaji, kutoa maoni yao, kusikiliza wanakikundi wengine husema nini na kuzingatia uchunguzi wao. Kunahitajika mwezesaji mwenye stadi madhubuti ili kuongoza majadiliano, kupitia maoni ya kila mshiriki, na kuhakikisha kuwa kunakuwa na ushiriki sawa kwa kila mshiriki.

Zingatia: Vifaa vyote lazima vitafsiriwe na vijaribiwe.

Marejeleo: "Furaha, Afya na Usafi" (Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto na Juhudi za Unawaji Mikono za Ushirika wa Umma na Sekta Binafsi, 1998).

Sehemu C: Zingatia kuhusu Uchocheo wa Unawaji Mikono

Utafiti uliotangulia unaonesha kuwa tabia ya unawaji mikono huchochewa na vichocheo vya kisaikolojia, desturi, na mazingira (Curtis, 2001). Vichocheo huweza kuwa chanya au hasi.

Vichocheo chanya mara nyingi hujumuisha:

Malezi: Hamu ya kulea watoto. Hali hii mara nyingi inahusika na afya, kama inavyoelezwa hapa chini.

Hadhi: Hamu ya kuwa msafi kwa ajili ya hadhi ya kijamii na utu.

Uzuri: Hamu ya kuonekana na kunukia vizuri, ili kuvutia wengine, na kujiridhisha mwenyewe.

(Zingatia: Vichocheo hivi viwili vya mwisho hususani huweza kuonwa kama vinahusiana).

Maudhi: Silika ya kukwepa na kuondoa kitu chochote kinachoudhi, ikijumuisha vidokezo (kunusa, kugusa, kuona: kama vile kuona madoa, hisia za mnato/kunata mikononi, harufu mbaya, au hisia za maambukizi, vyote vikiwa ni hali halisi au ni mawazo tu). Ni muhimu kujua ni kidokezo gani kati ya hivi huchukua nafasi kubwa katika silika ya kuudhi ili kuelekeza ujumbe wa uchocheaji wa unawaji mikono. Inaonekana kuwa kuna uhusiano wa karibu kati ya msingi wa maudhi na vyanzo vya maambukizi na magonjwa yaliyowakumba mababu zetu, hivyo silika ya maudhi huweza kuhusiana kwa karibu, kwa mujibu wa Curtis (2001).

Afya: Mara nyingi walengwa huelezea unawaji mikono kama ni hamu ya kukwepa vijidudu na magonjwa. Hata hivyo, faida ya maelezo haya katika programu za mabadiliko ya tabia si bayana (tazama zingatia). Mara nyingi dhana za afya njema huhusishwa na silika ya malezi/makuzi na hamu ya kukinga watoto dhidi ya magonjwa.

Zingatia kuwa kichocheo chake huweza kuwa cha kuweka uhai unaopelekea katika mafanikio na ustawi badala ya tabia inayotazamwa kwa ufahamu wa kitaalamu wa mbinu ambapo vijidudu maalumu husababisha magonjwa mahususi. Vijidudu pia hudhaniwa kuwa ni vimelea visivyonekana vinavyoudhi hivyo hupaswa kuondolewa.

Vichocheo hasi hujumuisha uvivu, hamu ya kufanya jambo fulani linalopingana na unawaji mikono, msukumo wa kukwepa sabuni kwa sababu ya manukato, imani katika vidokezo vya kiufahamu, na uwepo wa "vijidudu" na magonjwa yenye vijidudu.

Desturi ni tabia za kila siku ambazo mara nyingi hujengwa utotoni na hujitokeza zenyewe. Mazingira ya nje huwezesha au hukwaza unawaji mikono. Mathalani, pale ambapo sabuni na maji hupatikana, unawaji mikono kwa sabuni utafanyika, wakati kama choo kipo mbali na nyumbani na vifaa vya kunawia mikono, unawaji mikono baada ya kutoka chooni huweza kusifanyike.

1. Curtis, V.A., S. Cairncross, na R. Yonli (2000), Domestic hygiene and diarrhea, pinpointing the problem. *Tropical Medicine and International Health* 5 (1): 22-32.

2. Curtis, V. (2001), Hygiene: how myths, monsters and mothers-in-law promote behavior change. *Journal of Infection* 43: 75-81.

3. Curtis, V. and A. Biran (2001), Dirt, disgust and disease—Is hygiene in our genes? *Perspectives in Biology & Medicine* v. 1: 17-31.

4. Luby, S.P., M. Agboatwalla, J. Painter na wenzake, (2004). Effect of intensive handwashing promotion on childhood diarrhea in high-risk communities in Pakistan, a randomized controlled trial. *Journal of the American Medical Association* 291 (21): 2547-54.

Hadidu za Rejea 2: Mratibu wa Unawaji Mikono

Mratibu wa Unawaji Mikono wa Ushirika wa Sekta ya Umma na ya Binafsi nchini Peru

Hadidu za rejea

1. Usuli

Serikali ya Peru, kwa msaada wa Programu ya Maji na Usafi pamoja na wengine, inaanza juhudi mpya za kuchochea unawaji mikono kwa sabuni chini ya ushirika wa sekta ya umma na ya binafsi kukiwa na lengo la kupunguza magonjwa ya kuhara miongoni mwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano. Uzoefu wa ushirika wa sekta ya umma na ya binafsi Amerika ya Kati umeonesha matokeo chanya ya tabia ya unawaji mikono na matokeo ya magonjwa ya kuhara. Benki ya Dunia, Programu ya Maji na Usafi, Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto, na Shirika la Misaada la Marekani yamebuni, kwa kushirikiana na makampuni makubwa matatu ya utengenezaji wa sabuni, Juhudi za Kiulimwengu kwa ajili ya ushirika wa sekta ya umma na ya binafsi katika unawaji mikono. Majaribio mawili huko Kerala, India na Ghana yanatekeleza ushirika wa sekta ya umma na ya binafsi. Peru ni mshiriki mwingine anayepanua juhudi hizi za ushirika wa sekta ya umma na ya binafsi. Mratibu wa kitaifa kwa ajili ya shughuli hii mpya yenye matumaini anahitajika.

Uhalali wa Juhudi za Unawaji Mikono:

- Magonjwa ya kuhara hua watoto kati ya milioni mbili na milioni tatu kila mwaka ulimwenguni, na hushika nafasi ya tatu katika vyanzo vya magonjwa nchini Peru na ni chanzo cha asilimia 35 ya magonjwa ya watoto wenye umri chini ya miaka mitano.
- Magonjwa mengi ya kuhara husababishwa na kula kinyesi.
- Kuhara kunaweza kuzuiwa kwa kuzuia ulaji wa kinyesi kwa kutumia kanuni bora za usafi na unawaji mikono.
- Unawaji mikono kwa sabuni pekee unaweza kupunguza matukio ya kuhara yaliyoripotiwa kwa asilimia 35.

Data za kuaminika kuhusu unawaji mikono kwa sabuni baada ya kutumia choo au baada ya kutawadha mtoto hazipatikani nchini Peru. Juhudi za kuchochea usafi zimeelekezwa katika utoaji wa vifaa vya maji na usafi, njia bora za uhifadhi na kutibu maji lakini si katika unawaji mikono, hivyo ni mambo machache tu hufahamika kuhusiana na upatikanaji, unafuu wa gharama, na mahitaji ya sabuni, hususani kwa matumizi baada ya kugusa kinyesi, katika maeneo ya vijijini na miji midogo. Kuna haja ya kuunganisha elimu ya usafi/utoaji wa vifaa vya maji na usafi, kwa upande mmoja na uzalishaji na usambazaji wa sabuni za gharama nafuu, kwa upande mwingine. Viwanda vitarajie kufaidika na mauzo makubwa ya sabuni kupitia upanuzi wa masoko yao hadi kuzifikia kaya nyingi zaidi na kupitia ufikiwaji wa masoko kuelekea katika kaya masikini zaidi. Mashirika ya umma yatarajie kufaidika na ushirikishaji wa watengenezaji

wa sabuni katika programu zao katika kuboresha maisha kwa njia ya kupunguza magonjwa yanayohusiana na mienendo mibaya ya usafi.

2. Malengo ya Ushauri

Kusaidia DIGESA, Programu ya Maji na Usafi pamoja na washirika katika kuanzisha ushirika madhubuti wa sekta ya umma na ya binafsi kwa ajili ya juhudi zenye ufanisi za unawaji mikono. Mratibu anatarajiwa kuratibu shughuli zote za ushirika na kusimamia upangaji na utekelezaji wa shughuli zilizokubaliwa wakati wa awamu ya mwanzo ya mchakato. Matokeo ya mwisho ya awamu hii ya kwanza ni kukabidhi mpango ulioidhinishwa wa kazi na mkakati wa mawasiliano.

3. Mawanda ya Huduma

Mshauri mtaalamu atatoa huduma zifuatazo:

- Kuchochea uhusiano wa ushirika madhubuti kati ya sekta binafsi, umma, mashirika yasiyo ya kiserikali, na mawakala wa nje kuhusu juhudi za unawaji mikono, mkazo ukiwekwa katika uaminifu na ukusanyaji wa nyenzo za kiufundi kutoka kwa sekta binafsi.
- Kushirikiana na timu ya kiulimwengu ili kupata taarifa na utaalumu wa kutoka katika juhudi za kiulimwengu na nchi nyingine.
- Kutafiti usuli wa tafiti zilizopo za usafi na ripoti kuhusu uchocheaji wa programu za usafi (hususani mienendo ya unawaji mikono) nchini Peru.
- Kukusanya taarifa za ziada kuhusu hali ya soko, mkazo ukiwa katika kundi la watu maskini sana.
- Kubainisha mashirika muhimu ya utafiti na kuunganisha mipango, uteuzi wa washauri, na utekelezaji wa utafiti wa walengwa.
- Ukamilishaji wa uchambuzi wa hali kwa njia ya kujumuisha matokeo ya tafiti tatu (usuli, masoko, na biashara).
- Kuandaa mswada wa mpango wa kazi na mkakati wa mawasiliano ikiwa ni mchakato unaojirudiarudia, katika kutafuta nyenzo kutoka kwa washirika.
- Kukusanya fedha za kugharimia shughuli za mpango wa kazi.
- Kukusanya maoni na kuwasilisha mpango wa mwisho ulioidhinishwa pamoja na bajeti.

4. Mkabala

Mshauri mtaalamu atafanya kazi kwa ushirikiano wa karibu na wafanyakazi wa Programu ya Maji Safi na Salama (PMSS) na DIGESA pamoja na washirika wengine kupata mwafaka kuhusiana na mwelekeo na mawanda ya mradi wa ushirikiano wa sekta ya umma na ya binafsi kwa njia ya mipango shirikishi.

Kwanza, mshauri mtaalamu atajijengea imani na uaminifu kwa wadau kwa kukutana nao mmoja baada ya mwingine. Mikakati ifaayo ni vyema ikatumiwa ili kuibua na kuendeleza matakwa na maslahi ya wadau wote katika mradi wa ushirikiano wa sekta ya umma na ya binafsi.

5. Majukumu

Mshauri mtaalamu anatarajiwa:

- Kuwasilisha ripoti ya hali ya programu za uhamasishaji kuhusu soko la sabuni na usafi zinazowalenga watu maskini, zinazoendeshwa na Asasi Zisizo za Kiserikali, na sekta za umma nchini Peru;
- Kuandaa mikutano na kuratibu Kamati Elekezi ya Ushirika wa Sekta ya umma na ya binafsi (muundo utapangwa na PMSS na DIGESA);
- Kutoa usimamizi ili kuhakikisha ubora wa utafiti wa mlengwa;
- Kuwasilisha rasimu ya mpango wa kazi; na
- Kuwasilisha mpango wa mwisho wa kazi uliozingatia maoni na mapendekezo ya washirika.

6. Majukumu ya Mteja

PMSS itampatia mshauri mtaalamu ofisi pamoja na zana muhimu za mawasiliano ili aweze kutekeleza majukumu yake. Mshauri mtaalamu anatarajiwa kuwa na kompyuta yake mwenyewe. PMSS na DIGESA zitamtambulisha mshauri mtaalamu katika mtandao wa anwani za mawasiliano pamoja na kumpatia kila msaada ili kuendeleza na kuimarisha uhusiano baina ya mashirika.

7. Kuripoti

Mshauri mtaalamu anapaswa kutoa taarifa kwa Mratibu wa

Taifa wa PMSS na kufanya kazi kwa ushirikiano wa karibu na Mkurugenzi wa DIGESA na wafanyakazi wake. Nakala za ripoti zote lazima zipelekwe DIGESA. Mshauri mtaalamu atakabidhi ripoti fupi ya kila mwezi ya maendeleo ya mpango wa kazi na mpango wa kazi kwa mwezi unaofuata.

8. Kiwango cha Jitihada na Muda wa Kazi

Katika kipindi cha miezi kumi ya kukamilisha mchakato wa awamu ya ushirika wa sekta ya umma na ya binafsi, mshauri mtaalamu atahusishwa kwanza kwa muda wa miezi sita ya kazi. Kazi hiyo inaweza kuendelea hadi awamu inayofuata kutegemeana na utendaji kazi na upatikanaji wa fedha.

9. Sifa

Mshauri mtaalamu anapaswa awe na uzoefu thabiti wa kufanya kazi na sekta binafsi katika eneo la masoko au maendeleo ya biashara, upendeleo uwe kwa mwenye uzoefu wa masoko ya bidhaa zinazouzika chapuchapu. Mshauri mtaalamu anapaswa awe na utaalamu thibitifu wa kuandaa mipango ya masoko na mikakati ya mawasiliano yenye lengo la kubadili tabia. Uzoefu wa kujishughulisha na mashirika ya utafiti wa masoko na ya mawasiliano ni wa lazima. Kwa kuongezea, mshauri mtaalamu anapaswa awe na stadi bora za mawasiliano baina ya mtu na mtu na uwezo wa kufanya kazi na wadau wote ili awe kichocheo madhubuti. Itakuwa ni manufaa sana kwa mshauri mtaalamu kuwa na ujuzi wa kuwasiliana kwa lugha ya Kiingereza.

10. Mchakato wa Uteuzi

Washauri watakaonekana kuwa na vigezo vilivyotajwa wataitwa kwa ajili ya kufanyiwa usaili na wafanyakazi wa PMSS na DIGESA. Uteuzi wa mwisho utazingatia sifa za mshauri mtaalamu, mkabala uliopendekezwa wa kazi, pamoja na pendekezo la fedha.



ABBREVIATIONS

BASICS	Basic Support for Child Survival Project
CI	Consumer interviews
DALY	Disability Adjusted Life Year
DANIDA	Danish International Development Agency
DCC	Direct consumer contact
DFID	United Kingdom Department for International Development
DHS	Demographic and Health Surveys
EHP	Environmental Health Project
FGD	Focus group discussion
IRR	Internal rate of return
ISTMA	Indian Soap and Toiletries Manufacturers' Association
LSHTM	London School of Hygiene & Tropical Medicine
MDG	Millennium Development Goals
M&E	Monitoring and evaluation
NGO	Non-governmental organizations
NPV	Net present value
PPP	Public-private partnership
PPPHW	Public-Private Partnership Handwashing Initiative
PR	Public relations
SDC	Swiss Development Cooperation
SO	Structured observations
TOR	Terms of reference
UNICEF	United Nations Children's Fund
UNICEF/WES	United Nations Children's Fund/Water and Environmental Sanitation
USAID	United States Agency for International Development
WES	Water, environment and sanitation
WSP	Water and Sanitation Program
WSSCC	Water Supply & Sanitation Collaborative Council

The World Bank Group
1818 H Street, NW
Washington DC, 20433
USA
Ph: +1 202 473-1000
email: feedback@worldbank.org
www.worldbank.org

Task Team Leaders
Parameswaran Iyer, Jennifer Sara

Chief Contributors
Valerie Curtis, Beth Scott, Jason Cardosi

The Global Public Private Partnership for Handwashing
www.globalhandwashing.org

Production
Vandana Mehra

Created by Write Media and printed at
PS Press Services Pvt. Ltd.

